UCHAMBUZI WA MAWASILIANO YA UHIFADHI WA MAZINGIRA KATIKA VIPINDI VYA *SHAMBA SHAPE-UP* NA *CITIZEN PLANET* VYA RUNINGA YA CITIZEN NCHINI KENYA

NJAU WAMBUI JOYCE

1063428

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya kuhitimu Shahada ya Uzamili ya Lugha, Fasihi na Mawasiliano katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki-Langata

JULAI, 2026

TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa babangu, Joseph Njau na marehemu mamangu, Bi. Hellen Muthoni kwa kunilea kwa mapenzi, kunipa msingi wa elimu na kwa ushauri wao wa kunihimiza siku zote nifanye bidii masomoni.

UNGAMO

Tasnifu hii ya utafiti ni kazi yangu mwenyewe na imetolewa kwa mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Lugha, Fasihi na Mawasiliano, katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki-Langata na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya uzamili katika chuo chochote kingine.

Sahihi: 

Tarehe: 12th July 2026

NJAU WAMBUI JOYCE

Nambari ya Usajili: 1063428

IDHINI

Tasnifu hii imetolewa kwa ruhusa yetu kama wasimamizi wa mradi huu wa utafiti katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki-Langata.

Sahihi:  Tarehe 12th July 2026

Daktari Rose Mavisi

Sahihi:  **Tarehe 12th July 2026**

Daktari Douglas Nkumbo

SHUKRANI

Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema, hekima, afya na ulinzi wake ulionisindikiza katika safari yangu yote ya masomo na utekelezaji wa utafiti huu kuhusu mchango wa Runinga ya Citizen katika uhifadhi wa mazingira nchini Kenya, kwa kurejelea uchanganuzi wa vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Ninathamini nguvu na uwezo wa kiakili alionijalia ambao umenisaidia kufanikisha hatua hii muhimu ya kitaaluma.

Kwa namna ya pekee, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wa utafiti huu, Dkt. Rose Mavisi na Dkt. Douglas Nkumbo, kwa uongozi wao mahiri, mwongozo wa kitaaluma, ushauri wa kina na marekebisho ya kitaaluma yaliyosaidia kuimarisha ubora wa kazi hii. Ninawashukuru pia wahadhiri wote wa Idara ya Lugha na Mawasiliano, wakiwemo Dkt. Harryson Ogutu, Dkt. Mary Malenya, Bw. Bogonko na wengine wote ambao wemekuwa katika kikao cha kutetea utafiti huu, kwa mchango wao muhimu wa kunijenga kitaaluma katika ngazi ya uzamili.

Shukrani za dhati ziwaendee wanashirika wa Jumuiya ya Watawa wa Kiume wa Mtakatifu Fransisco wa Assisi, Prof. Jane Rarieya AKU na Prof. Mbugua Ngari kwa mchango wao wa kifedha wakati nilipokuwa nimelemewa na karo za shule pamoja na wanajumuiya yangu ya Shirika la Maria Immaculata wa Gulu kwa upendo wao, sala na msaada wao wa kifedha ulioniwezesha kufanikisha masomo yangu ya uzamili. Pia, ninawashukuru wanakozi wenzangu wote kwa kushirikiana na kusaidiana nami wakati wa masomo ya kozi hii ya uzamili. Kwa ujumla, shukrani zangu za dhati zinaelekezwa kwa yeyote aliyenisaidia kufanikisha utafiti huu.

IKISIRI

Utafiti huu ulichambua mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya**.** Utafiti ulilenga kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, kuchanganua changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na kuchunguza mikakati ya kimawasiliano inayotumiwa katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhakiki- Ikolojia ambayo ilianza kujengeka katika miaka ya 1970 na William Rueckert. Baadaye, nadharia hii iliendelezwa na wataalamu mbalimbali, wakiwemo Cheryll Glotfelty na Fromm (1996)**,** inayosisitiza kuchunguza uhusiano na utegemeano kati ya binadamu na mazingira, athari za shughuli za binadamu kwa mifumo ikolojia na wajibu wa binadamu katika uhifadhi wa mazingira. Utafiti ulitumia mkabala wa kimaelezo na muundo wa uchambuzi wa nyaraka na maudhui**,** huku sampuli ya makusudi ikitumika kuteua vipindi vyenye maudhui ya kimazingira. Matokeo yalibainisha kuwa vipindi hivyo vinawasilisha masuala ya uhifadhi wa misitu na upandaji miti, uhifadhi wa udongo na maji, kilimo hifadhi, bioanuwai, usimamizi wa taka, nishati endelevu na mabadiliko ya tabianchi. Pia vilibainisha changamoto za ukataji miti, uchafuzi, mmomonyoko wa udongo, ukame, kupungua kwa rutuba ya udongo na upotevu wa bioanuwai. Mikakati ya mawasiliano iliyobainika ni pamoja na lugha rahisi, mahojiano ya wataalamu, maonesho ya vitendo, ushuhuda wa jamii, simulizi, picha na vielelezo**.** Utafiti ulihitimisha kuwa vipindi hivi ni majukwaa muhimu ya mawasiliano ya mazingira na unapendekeza kuimarishwa kwa maudhui ya mazingira, ushiriki wa jamii na ushirikiano kati ya vyombo vya habari, wataalamu na taasisi za mazingira ili kukuza uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za asili nchini Kenya.

ABSTRACT

This study annalyzed environmental conservation communication in the television programmes *Shamba Shape-Up* and *Citizen Planet* broadcast by Runinga ya Citizen in Kenya**.** The study aimed to identify the environmental conservation issues presented, analyse the environmental challenges highlighted, and examine the communication strategies used to convey environmental conservation messages. The study was guided by the Ecocriticism Theory, which began to develop in the 1970s through the work of William Rueckert and was later advanced by various scholars, including Cheryll Glotfelty and Fromm (1996)**.** The theory emphasizes the examination of the relationship and interdependence between human beings and the environment, the impacts of human activities on ecosystems, and human responsibility for environmental conservation. The study adopted a descriptive approach and a document and content analysis design**,** with purposive sampling used to select programmes containing environmental content. The findings revealed that the programmes present various environmental conservation issues, including forest conservation and tree planting, soil and water conservation, conservation agriculture, biodiversity conservation, waste management, sustainable energy, and climate change**.** The programmes also highlighted challenges such as deforestation, pollution, soil erosion, drought, declining soil fertility, and biodiversity loss. The communication strategies identified included the use of simple language, expert interviews, practical demonstrations, community testimonies, narratives, images, and illustrations**.** The study concludes that these programmes are important platforms for environmental communication and recommends strengthening environmental content, community participation, and collaboration among media organisations, experts, and environmental institutions to promote environmental conservation and sustainable use of natural resources in Kenya.

AKRONIMU NA VIFUPISHO

UNESCO: United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization

UNEP: United Nations Environment Programme

IFPRI: International Food Policy Research Institute

ADB: African Development Bank

IPCC: Intergovernmental Pannel on Climate Change

EAC: East Africa Cmmunity

GMO: Genetically Modified Organism

M Mtaalamu

V: Video

JEDWALI LA MISIMBO

Msimbo	**Maana ya Msimbo**
M-01-V-SSU	Mtaalamu wa kwanza Video ya *Shamba Shape-Up*
M-01-V-CP	Mtaalamu wa kwanza Video ya *Citizen Planet*
M-02-V-SSU	Mtaalamu wa pili Video ya *Shamba Shape-Up*
M-02-V-CP	Mtaalamu wa pili Video ya *Citizen Planet*
M-03-V-SSU	Mtaalamu wa tatu Video *Shamba Shape-Up*
M-04-V-SSU	Mtaalamu wa nne Video ya *Shamba Shape-Up*
M-03-V-CP	Mtaalamu wa tatu Video ya *Citizen Planet*
M- 05- V-SSU	Mtaalamu wa tano Video ya *Shamba Shape-Up*
M-06-V-SSU	Mtaalamu wa sita Video ya *Shamba Shape-Up*
M-07-V-SSU	Mtaalamu wa saba Video ya *Shamba Shape-Up*
M-04-V-CP	Mtaalamu wa nne Video ya *Citizen Planet*
M-05-V-CP	Mtaalamu wa tano Video ya *Citizen Planet*
M-07-V-SSU	Mtaalamu wa saba Video *Shamba Shape-Up*
M-06-V-CP	Mtaalamu wa sita Video ya *Citizen Planet*
M-07-V-CP	Mtaalamu was aba Video ya *Citizen Planet*
M-08-V-CP	Mtaalamu wa nane Video ya *Citizen Planet*
M-08-V-SSU	Mtaalamu wa nane Video ya *Shamba Shape-Up*
M-09-V-SSU	Mtaalamu wat isa Video ya *Shamba Shape-Up*
M-09-V-CP	Mtaalamu wa tisa Video ya *Citizen Planet*
M-10-V-CP	Mtaalamu wa kumi Video ya *Citizen Planet*
M-11-V-CP	Mtaalamu wa kumi na moja Video ya *Citizen Planet*
M-10-V-SSU	Mtaalamu wa kumi Video ya *Shamba Shape-Up*
M-12-V-CP	Mtaalamu wa kumi na mbili Video ya *Citizen Planet*
M-11-V-SSU	Mtaalamu wa kumi na moja Video ya *Shamba Shape-Up*
M-12-V-SSU	Mtaalamu wa kumi na mbili Video ya *Shamba Shape-Up*

UFAFANUZI WA ISTILAHI

Mazingira: Jumla ya vitu vyote vinavyotuzunguka na kuathiri maisha ya viumbe hai.

Tabianchi: Hali ya hewa ya muda mrefu katika eneo fulani**,** kwa kawaida hupimwa kwa kipindi cha miaka mingi kama miaka 30 au zaidi.

Bioanuai: Uwepo wa aina mbalimbali za viumbe hai katika eneo fulani au duniani kwa ujumla.

Mawasiliano: Mawasiliano ni mchakato wa kubadilishana na kuwasilisha taarifa, mawazo au ujumbe kati ya mtumaji na mpokeaji kwa kutumia njia mbalimbali ili kujenga uelewa.

YALIYOMO

UNGAMO..... Error! Bookmark not defined.
SHUKRANI..... **iii**
IKISIRI ..... **v**
ABSTRACT..... **vi**
AKRONIMU NA VIFUPISHO..... **vii**
JEDWALI LA MISIMBO ..... **viii**
UFAFANUZI WA ISTILAHI ..... **ix**
YALIYOMO..... **x**
SURA YA KWANZA 1
UTANGULIZI..... 1
1.1 Utangulizi..... 1
1.2 Usuli wa Mada 1
1.3 Tatizo la Utafiti 4
1.4 Malengo ya Utafiti 5
1.5 Maswali ya Utafiti..... 5
1.6 Umuhimu wa Utafiti..... 5
1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti..... 7
SURA YA PILI..... 8
MAPITIO YA MAANDISHI NA MSINGI WA NADHARIA 8
2.1 Utangulizi..... 8
2.2 Masuala ya Uhifadhi wa Mazingira katika Vyombo vya Habari..... 8
2.3 Changamoto Zinazoibuka Kutokana na Kutohifadhi Mazingira 24
2.4 Mikakati ya kimawasiliano Inayotumika katika Vipindi Teule 33
2.5 Msingi wa Nadharia 44
2.5.1 Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia 44
2.5.2 Mihimili ya Nadharia..... 45
2.5.3 Uhusiano wa Nadharia ya Uhakiki-ikolojia na Utafiti Huu 46
SURA YA TATU..... 49
MBINU ZA UTAFITI..... 49
3.1 Utangulizi..... 49
3.2 Muundo wa Utafiti 49
3.3 Eneo la Utafiti 49
3.4 Kundi Lengwa..... 50
3.5 Uteuzi wa Sampuli na Usampulishaji 51
3.6 Mbinu za Kukusanya Data 51
3.7 Uchanganuzi wa Data..... 51
3.8 Vifaa vya Utafiti..... 52
3.9 Maadili ya Utafiti 53

SURA YA NNE 54

UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA 54

4.0 Utangulizi 54
4.1 Masuala ya Uhifadhi wa Mazingira 54
4.1.1 Uhifadhi wa Udongo 55
4.1.2 Upandaji wa Miti na Uhifadhi wa Misitu 57
4.1.3 Uhifadhi wa Bioanuai 59
4.1.4 Matumizi ya Nishati Safi 62
4.1.5 Uhifadhi wa Maji 64
4.1.6 Kilimo Hai na Matumizi ya Mbolea Asilia 65
4.1.7 Usimamizi Endelevu wa Taka Ngumu kupitia Urejelezaji 67
4.2 Changamoto Zinazoibuka Kutokana na Kutohifadhi Mazingira 69
4.2.1 Changamoto za Mmomonyoko wa Udongo 70
4.2.2 Changamoto za Ukame na Uhaba wa Maji 72
4.2.3 Changamoto za Kupungua kwa Rutuba ya Udongo 74
4.2.4 Changamoto za Mabadiliko ya Tabianchi 77
4.2.5 Changamoto za Kupotea kwa Bioanuwai 79
4.2.6 Changamoto za Kuongezeka kwa Uchafuzi wa Mazingira 82
4.3 Mikakati ya Kimawasiliano Inayotumika katika Vipindi vya Shamba Shape-Up na Citizen Planet 86
4.3.1 Mikakati ya Matumizi ya Maonesho ya Vitendo 87
4.3.2 Mikakati ya Matumizi ya Elimu-Burudani 93
4.3.3 Mikakati ya Matumizi ya Mifano Halisi 97
4.3.4 Mikakati ya Matumizi ya Mahojiano ya Jamii 99
4.3.5 Mikakati ya Matumizi ya Taswira na Video 101
4.4 Hitimisho 104

SURA YA TANO 105

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 105

5.0 Utangulizi 105
5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti 105
5.1.1. Masuala ya Uhifadhi wa Mazingira katika Kipindi cha Shamba Shape-Up na Citizen Planet 106
5.1.2. Changamoto Zinazoibuka Kutokana na Kutohifadhi Vazingira katika Vipindi vya Shamba Shape-Up na Citizen Planet. 107
5.1.3. Mikakati ya Kimawasiliano Inayotumiwa katika Vipindi vya Shamba Shape-Up na Citizen Planet. 107
5.3 Mapendekezo ya Utafiti 108

MAREJELEO 110

VIAMBATISHO 116

Kiambatisho I: Kibali cha Utafiti cha Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki. 116
Kiambatisho II: Kibali cha Utafiti cha NACOSTI 117

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Sura hii ilitanguliza utafiti huu ambao ulilenga uchambuzi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya. Katika kuchanganua mada hii, sura hii iliangazia usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na kisha upeo na mipaka ya utafiti.

1.2 Usuli wa Mada

Katika karne ya ishirini na moja, uhifadhi wa mazingira ulikuwa miongoni mwa masuala muhimu katika mijadala ya maendeleo kutokana na changamoto zilizokuwa zikiathiri mifumo ya ikolojia na ustawi wa jamii. Changamoto hizo zilihusisha mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mifumo ya asili, upotevu wa bioanuwai, uchafuzi wa mazingira, uhaba wa maji na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za asili. Ripoti ya *Global Environment Outlook 6* ilionesha kuwa hali ya mazingira duniani ilikuwa ikiendelea kudorora na kwamba mazingira yenye afya yalikuwa msingi wa afya, ustawi wa binadamu na maendeleo ya kiuchumi (United Nations Environment Programme [UNEP], 2019). Aidha, Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC, 2021) ilibainisha kuwa mabadiliko ya tabianchi yalikuwa yameleta athari katika mifumo ya asili na jamii, hivyo kuongeza umuhimu wa hatua za kukabiliana na changamoto hizo.

Kutokana na hali hiyo, mawasiliano ya mazingira yalipata umuhimu katika kuwasaidia watu kuelewa changamoto za kimazingira na nafasi yao katika kukabiliana nazo. Hansen (1991) alieleza kuwa vyombo vya habari vilishiriki katika ujenzi wa kijamii wa masuala ya mazingira kwa kuamua namna masuala hayo yalivyowasilishwa katika anga ya umma. Cox (2013) naye alieleza mawasiliano ya mazingira kama mchakato uliowezesha jamii kuelewa, kujadili na kuchukua hatua kuhusu masuala ya mazingira. Kwa hivyo, ujumbe wa mazingira haukuhusisha maelezo ya tatizo pekee, bali pia ulihusisha namna mazingira, binadamu na mahusiano yao yalivyowakilishwa.

Runinga ilikuwa miongoni mwa vyombo vilivyokuwa na uwezo wa kuwasilisha ujumbe wa mazingira kwa kutumia lugha, sauti, picha, mandhari, mahojiano na maonyesho ya vitendo. Hansen na Machin (2013) walisisitiza kuwa uchambuzi wa mawasiliano ya mazingira ulihitaji

kuzingatia vipengele vya kuona pamoja na lugha. Kwa mtazamo huo, ujumbe kuhusu ukame, uharibifu wa misitu, uchafuzi wa maji au uhifadhi wa udongo ungeweza kujengwa kupitia maelezo ya mtangazaji, picha za mazingira, mahojiano na vitendo vilivyooneshwa. Hivyo, namna televisheni ilivyowasilisha mazingira ilikuwa muhimu katika kuelewa maana iliyojengwa kuhusu uhusiano kati ya binadamu na mazingira.

Katika bara la Afrika, changamoto za mazingira zilikuwa na uhusiano wa karibu na maisha ya jamii na shughuli za kiuchumi zilizotegemea rasilimali za asili. Kilimo, ufugaji, uvuvi na matumizi ya misitu vilikuwa miongoni mwa shughuli zilizokuwa zikiathiriwa na mabadiliko ya tabianchi na matukio ya hali mbaya ya hewa. African Development Bank (2022) ilibainisha kuwa mabadiliko ya tabianchi yaliendelea kuwa changamoto kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi barani Afrika. Hali hiyo iliongeza umuhimu wa mawasiliano yaliyoweza kuhusisha jamii katika kuelewa changamoto za mazingira na hatua za kukabiliana nazo.

Katika mazingira hayo, vyombo vya habari vilikuwa na nafasi ya kuwasilisha taarifa kuhusu mazingira pamoja na maarifa na hatua za uhifadhi. Mawasiliano hayo yalikuwa muhimu kwa sababu changamoto za mazingira hazikuhusu mazingira pekee, bali pia zilihusisha maisha, uzalishaji na matumizi ya rasilimali za jamii. Kwa hivyo, uchunguzi wa mawasiliano ya mazingira ulihitaji kuangalia namna shughuli za binadamu, changamoto za kimazingira na hatua za uhifadhi zilivyowasilishwa.

Nchini Kenya, ardhi, maji, misitu, wanyamapori na rasilimali nyingine za asili zilikuwa na umuhimu mkubwa katika maisha ya jamii na shughuli za kiuchumi. Changamoto zilizohusiana na mabadiliko ya tabianchi, upatikanaji wa maji, uharibifu wa mazingira na matumizi ya rasilimali ziliifanya ajenda ya uhifadhi kuwa muhimu katika mijadala ya maendeleo. Katika muktadha huu, vyombo vya habari vilikuwa miongoni mwa majukwaa yaliyoweza kuwasilisha changamoto hizo, maarifa ya wataalamu na hatua zilizochukuliwa na jamii katika kukabiliana nazo.

Utafiti wa Wefwafwa (2025) uliangalia namna televisheni ilivyowasilisha uhifadhi wa mazingira ya asili nchini Kenya kupitia kipindi cha *Culture Quest* cha KTN. Utafiti huo ulionyesha umuhimu wa televisheni katika kuwasilisha maarifa ya uhifadhi wa mazingira. Hata hivyo, utafiti huo ulijikita katika *Culture Quest* na uhifadhi wa mazingira ya asili. Hivyo, bado kulikuwa na haja ya kuchunguza namna vipindi vya vituo vingine vya televisheni vilivyowasilisha uhifadhi wa mazingira, hasa pale ambapo vipindi hivyo vilikuwa na miundo na malengo tofauti.

Katika muktadha huo, Runinga ya Citizen ilikuwa jukwaa muhimu la kuchunguza mawasiliano ya mazingira nchini Kenya. Miongoni mwa vipindi vilivyotoa fursa ya uchunguzi huo vilikuwa *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. *Shamba Shape-Up* kilitumia muundo wa elimu-burudani na kubadilisha muonekano wa mashamba kuwasilisha maarifa ya kilimo na suluhisho kwa wakulima. Taarifa za Mediae zilionesha kuwa kipindi hicho kilirushwa kupitia Runinga ya Citizen na kilihusisha mada zilizogusa uhifadhi wa udongo, uzalishaji wa kilimo na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (Mediae, 2021, 2022).

Ingawa kipindi cha *Shamba Shape-Up* kililenga zaidi kilimo, baadhi ya maudhui yake yalikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na uhifadhi wa mazingira. Maudhui kuhusu uhifadhi wa udongo, uvunaji wa maji, mboji, miti na mbinu za kilimo zilizozingatia mabadiliko ya tabianchi yalihusisha uhusiano kati ya uzalishaji wa chakula na matumizi endelevu ya rasilimali. Kwa hiyo, kipindi hicho kilitoa nafasi ya kuchunguza namna ujumbe wa kilimo ulivyoweza kuwasilisha pia masuala ya uhifadhi wa mazingira.

Kwa upande mwingine, *Citizen Planet* kilitoa nafasi ya kuchunguza mazingira kutoka katika mtazamo wa moja kwa moja zaidi wa uhifadhi. Vipindi vyake vilihusisha masuala ya mazingira na juhudi za jamii katika kukabiliana na changamoto za kimazingira. Tofauti ya mwelekeo kati ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* ilitoa msingi wa kuvichunguza pamoja ili kubaini namna ujumbe wa uhifadhi ulivyowasilishwa katika vipindi vyenye mwelekeo tofauti.

Namna mazingira na uhusiano wake na binadamu vilivyowasilishwa katika vipindi hivyo ilihitaji mtazamo uliowezesha kuchunguza mahusiano hayo. Kwa msingi huo, utafiti uliongozwa na Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia. Glotfelty na Fromm (1996) walitoa msingi muhimu wa nadharia hii kwa kuhusisha uchunguzi wa mahusiano kati ya fasihi na mazingira ya kimaumbile. Ingawa nadharia hiyo ilijikita katika uchambuzi wa fasihi, msingi wake uliweza kutumika kuchunguza namna mazingira na mahusiano kati ya binadamu na ulimwengu wa kimaumbile yalivyowakilishwa katika maudhui ya vyombo vya habari. Katika utafiti huu, nadharia hiyo ilitumika kuchunguza namna *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vilivyowakilisha mazingira, shughuli za binadamu na wajibu wa jamii katika uhifadhi. Mtazamo huo uliwezesha utafiti kuangalia si tu masuala ya mazingira yaliyowasilishwa, bali pia maana iliyojengwa kuhusu uhusiano kati ya binadamu na mazingira.

Pamoja na tafiti zilizokuwa zimefanyika kuhusu mawasiliano ya mazingira na uwasilishaji wa uhifadhi kupitia televisheni, bado kulikuwa na pengo katika kuchunguza kwa pamoja maudhui

ya mazingira, changamoto za kiikolojia, uhusiano kati ya binadamu na mazingira, mikakati ya mawasiliano na suluhisho za uhifadhi katika vipindi vya Runinga ya Citizen. Utafiti wa Wefwafwa (2025) ulijikita katika *Culture Quest* ya KTN, hivyo haukushughulikia namna *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen vilivyowasilisha uhifadhi wa mazingira. Pengo hilo liliweka msingi wa kufanya utafiti huu.

Kwa msingi huo, utafiti huu ulichunguza mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya. Utafiti ulijikita katika kuchanganua maudhui ya mazingira yaliyowasilishwa, changamoto za kimazingira zilizoibuliwa, namna uhusiano kati ya binadamu na mazingira ulivyowakilishwa, pamoja na mikakati ya mawasiliano iliyotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia.

Kwa hivyo, utafiti haukulenga kupima athari za vipindi hivyo kwa watazamaji, bali ulichanganua namna vipindi hivyo vilivyowasilisha uhifadhi wa mazingira kupitia maudhui na mikakati ya mawasiliano. Mtazamo huo uliuwezesha utafiti kutoa uelewa kuhusu nafasi ya televisheni katika kuwasilisha changamoto za kimazingira, suluhisho za uhifadhi na wajibu wa jamii katika matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira.

1.3 Tatizo la Utafiti

Kuongezeka kwa changamoto za kimazingira nchini Kenya, kama vile mabadiliko ya tabianchi, ukame na uhaba wa maji, ukataji wa miti, uharibifu wa ardhi na upotevu wa bioanuwai**,** kumeongeza umuhimu wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira. Runinga ya Citizen kupitia *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* imekuwa ikiwasilisha masuala kama kilimo endelevu, uhifadhi wa udongo na maji, upandaji miti na usimamizi wa taka. Kwa mfano, *Shamba Shape-Up* huonesha mbinu za kilimo na suluhisho za changamoto za wakulima, huku vipindi vyake vikijumuisha pia mada za uhifadhi wa mazingira. Hata hivyo, bado haijachunguzwa kwa kina namna maudhui haya yanavyowasilisha uhusiano kati ya binadamu na mazingira na kujenga ujumbe wa uhifadhi**.**

Pamoja na tafiti zilizopo kuhusu vyombo vya habari na mazingira, bado kuna pengo katika kuchanganua maudhui na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa na vipindi hivi katika kuwasilisha uhifadhi wa mazingira. Kwa mfano, haijabainishwa vya kutosha namna mahojiano ya wataalamu, maonyesho ya vitendo, picha na simulizi za jamii zinavyotumika kuwasilisha masuala kama uhifadhi wa maji, udongo na bioanuwai. Kwa hivyo, utafiti huu ulichanganua

Shamba Shape-Up na *Citizen Planet* ili kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa, kwa kuongozwa na Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia.

1.4 Malengo ya Utafiti

1. Kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira katika kipindi cha *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika Runinga ya Citizen.
2. Kujadili changamoto zinazoibuka kutokana na kutohifadhi mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika Runinga ya Citizen.
3. Kutathmini mikakati ya kimawasiliano inayotumiwa katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika Runinga ya Citizen.

1.5 Maswali ya Utafiti

1. Ni masuala gani ya uhifadhi wa mazingira yanayoangaziwa katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*?
2. Ni changamoto zipi zinazojitokeza kutokana na kutohifadhi mazingira kama zinavyoonyeshwa katika vipindi hivi?
3. Ni mikakati ipi ya kimawasiliano inayotumiwa katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utaongeza maarifa katika taaluma za mawasiliano, Isimujamii na masuala ya mazingira kwa kubainisha nafasi ya runinga katika kuhamasisha uhifadhi wa mazingira kupitia maudhui na mikakati mbalimbali ya kimawasiliano.

Pia, utafiti huu utapanua uelewa kuhusu matumizi ya vyombo vya habari katika kukuza maendeleo endelevu**,** kwa kuonesha namna runinga inavyoweza kutumia maudhui ya kimazingira kuwasilisha maarifa, kuhimiza matumizi endelevu ya rasilimali na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira.

Aidha, matokeo ya utafiti huu yalitoa maarifa muhimu kwa vituo vya runinga na watayarishaji wa vipindi vya mazingira kuhusu namna ya kuimarisha uwasilishaji wa maudhui ya uhifadhi wa mazingira. Matokeo hayo yanaweza kutumika katika kuchagua maudhui yanayohusiana na

changamoto za mazingira, kutumia lugha inayoeleweka, pamoja na kuhusisha mbinu shirikishi na maonyesho ya vitendo katika uwasilishaji wa ujumbe.

Utafiti huu pia ulitoa taarifa muhimu kwa serikali, mashirika ya mazingira na wadau wengine kuhusu namna runinga inavyoweza kutumika kama chombo cha mawasiliano katika kuwasilisha masuala ya uhifadhi wa mazingira. Maarifa yaliyopatikana yanaweza kusaidia katika uandaaji wa sera, programu na mikakati ya mawasiliano ya mazingira inayozingatia matumizi ya vyombo vya habari katika kueneza taarifa kuhusu changamoto za kimazingira na hatua za kuzitatua. Hivyo, utafiti umeweka msingi wa kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za serikali, mashirika ya mazingira na vyombo vya habari katika kuendeleza mawasiliano yanayounga mkono uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu.

Vilevile, utafiti huu ulionesha namna vipindi vya runinga vinavyochangia kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira, matumizi endelevu ya rasilimali na mbinu bora za kilimo kinacholenga kuhifadhi mazingira.

Utafiti huu ulitoa uelewa kuhusu nafasi ya mawasiliano ya runinga katika kuchochea uelewa na mabadiliko chanya kuhusu uhifadhi wa mazingira. Kwa kuchambua maudhui na mikakati ya kimawasiliano inayotumika katika vipindi teule, utafiti ulionesha namna ujumbe wa kimazingira unavyoweza kuwasilishwa kwa njia inayosisitiza umuhimu wa kulinda na kutumia rasilimali za mazingira kwa uendelevu. Maarifa haya yanaweza kuwa msingi wa kuboresha uundaji na uwasilishaji wa vipindi vya mazingira ili kuimarisha mawasiliano ya uhifadhi na kuchangia maendeleo endelevu.

Kwa kuhitimisha, utafiti huu ulionesha umuhimu wa kuimarisha mawasiliano ya mazingira kupitia uwasilishaji wa maudhui unaoeleweka, unaovutia na unaolenga kutoa maarifa ya vitendo kuhusu uhifadhi wa mazingira. Matokeo yake yanaweza kutumiwa na watayarishaji wa vipindi na vyombo vya habari kuboresha namna masuala ya mazingira yanavyowasilishwa, kwa kuzingatia matumizi ya lugha rahisi, mifano halisi na maonyesho ya vitendo. Kwa mtazamo huo, utafiti huu ulichangia kuimarisha mawasiliano ya mazingira na kuweka msingi wa matumizi bora ya runinga katika kuunga mkono juhudi za uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu.

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulichanganua mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya. Utafiti ulijikita katika kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, kuchanganua changamoto zinazotokana na uharibifu wa mazingira kama zinavyowakilishwa katika vipindi hivyo, na kuchunguza mikakati ya kimawasiliano inayotumiwa kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Kijiografia, utafiti ulizingatia muktadha wa Kenya, huku kimuda ukijikita katika maudhui ya *Shamba Shape-Up* ya mwaka 2020–2026 na *Citizen Planet* ya mwaka 2025–2026.

Hata hivyo, utafiti huu ulikuwa na mipaka kadhaa. Kwanza, haukuchunguza vipindi vyote vilivyopeperushwa na Runinga ya Citizen, bali ulijikita katika vipindi tajwa pekee. Pili, haukuhusisha ukusanyaji wa data za msingi kutoka kwa watazamaji, watayarishaji au wadau wengine, bali ulitegemea uchanganuzi wa data za sekondari kama vile maudhui ya vipindi, tafiti zilizochapishwa na nyaraka husika. Hivyo, utafiti haukutoa mitazamo ya moja kwa moja ya washiriki, bali uliegemea uchambuzi wa kitaaluma wa maudhui yaliyopo. Aidha, vipengele vya kiufundi vya utayarishaji wa runinga havikuchunguzwa kwa kina isipokuwa pale vilipohusiana moja kwa moja na mawasiliano ya kimazingira. Kwa msingi huo, upeo na mipaka hii iliwekwa ili kuruhusu uchunguzi wa kina na mahususi kuhusu mchango wa runinga katika mawasiliano ya mazingira nchini Kenya.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA MSINGI WA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii iliwasilisha mapitio ya maandishi na mkabala wa kinadharia uliouongoza utafiti kuhusu mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya. Lengo kuu la sura hii lilikuwa kujenga msingi wa kitaaluma wa kuelewa namna runinga inavyoweza kutumika kama chombo cha mawasiliano ya kimazingira katika kuibua na kuwasilisha masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto zinazotokana na uharibifu wa mazingira na mikakati ya kimawasiliano inayotumiwa kufikisha ujumbe wa uhifadhi**.** Aidha, sura hii iliongozwa na Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia, iliyosaidia kuchanganua namna maudhui ya runinga yanavyowakilisha uhusiano kati ya binadamu na mazingira, matumizi ya rasilimali za asili, uharibifu wa mazingira na umuhimu wa uhifadhi na uendelevu.

2.2 Masuala ya Uhifadhi wa Mazingira katika Vyombo vya Habari

Utafiti wa *UNESCO (2021)* kuhusu *Global Media and Information Literacy Week* una umuhimu katika kuelewa nafasi ya vyombo vya habari katika mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira**,** kwa kusisitiza umuhimu wa taarifa sahihi na uelewa wa masuala ya mazingira katika kujenga jamii inayoweza kushiriki katika uhifadhi wa rasilimali za asili. Utafiti huo unaonesha kuwa vyombo vya habari vinaweza kuwasilisha masuala kama mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa mazingira, uharibifu wa ardhi na upotevu wa bioanuwai, na hivyo kutoa jukwaa la kujadili changamoto za kimazingira na njia za kukabiliana nazo. Mtazamo huu unaendana na utafiti huu kwa sababu *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* pia hutumia mawasiliano ya televisheni kuwasilisha masuala ya mazingira na suluhisho zake. Hata hivyo, UNESCO inajadili nafasi ya vyombo vya habari kwa mtazamo mpana, wakati utafiti huu unalenga uchambuzi wa maudhui na mikakati ya mawasiliano katika vipindi viwili mahususi vya Runinga ya Citizen nchini Kenya**.**

Tofauti hiyo inaonesha pengo la kimuktadha ambalo utafiti huu unalenga kulijaza. UNESCO (2021) haikujikita katika kuchanganua kwa kina namna *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* zinavyowasilisha uhifadhi wa udongo, maji, misitu, bioanuwai, usimamizi wa taka na matumizi endelevu ya rasilimali, wala haikuchunguza kwa undani mikakati ya mawasiliano inayotumika katika vipindi hivyo. Kwa hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kwa kuchanganua nini kinawasilishwa kuhusu uhifadhi wa mazingira, changamoto zipi zinaibuliwa na ni kwa namna

gani ujumbe huo unawasilishwa kupitia lugha, picha, mahojiano, simulizi na maonyesho ya vitendo. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia, utafiti unaenda zaidi ya kubainisha uwepo wa maudhui ya mazingira kwa kuchunguza namna vipindi hivyo vinavyowakilisha uhusiano kati ya binadamu na mazingira, matumizi ya rasilimali za asili, uharibifu wa mazingira na umuhimu wa uendelevu**.** Hivyo, utafiti huu unaziba pengo la ukosefu wa uchambuzi mahsusi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika muktadha wa Kenya.

Utafiti wa *United Nations Environment Programme (UNEP, 2021) katika GEO-6 for Youth* unasisitiza umuhimu wa kuwawezesha vijana kupata maarifa kuhusu hali ya mazingira na kuwahamasisha kuchukua hatua zinazochangia uendelevu wa mazingira. Chapisho hilo lililenga vijana wa umri wa miaka 15–24 na liliandaliwa kwa kutumia lugha inayofikika kwa vijana pamoja na vipengele shirikishi kama video, infografiki na shughuli mbalimbali za kujifunza. Lengo kuu lilikuwa si kutoa taarifa kuhusu matatizo ya mazingira pekee, bali pia kuwaonesha vijana kwamba wanaweza kuwa mawakala wa mabadiliko kupitia maamuzi na vitendo vya kila siku, shughuli za pamoja na uchaguzi wa shughuli za kiuchumi zinazozingatia mazingira.

UNEP inaunganisha masuala kama ardhi, bioanuwai, maji safi, bahari, hewa, tabianchi, chakula, nishati na taka, hivyo kuonesha kuwa uhifadhi wa mazingira unahitaji mabadiliko katika mifumo ya uzalishaji, matumizi na usimamizi wa rasilimali. Mtazamo huu una uhusiano na utafiti huu kwa sababu unatambua mawasiliano kama sehemu ya mchakato wa kujenga uelewa na kuchochea hatua za kimazingira. Hata hivyo, UNEP (2021) haikulenga kuchanganua kwa kina namna vipindi mahususi vya televisheni nchini Kenya vinavyowasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Badala yake, GEO-6 for Youth ina mtazamo mpana wa kimataifa unaolenga kutafsiri maarifa ya kisayansi kuhusu mazingira katika lugha na mifumo inayoweza kueleweka na kutumiwa na vijana. Chapisho hilo pia linatoa mifano ya miradi inayoongozwa na vijana na jamii pamoja na hatua zinazoweza kuchukuliwa katika ngazi ya mtu binafsi na ya pamoja.

Kwa upande mwingine, utafiti huu unalenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza maudhui ya mazingira yanayowasilishwa kupitia vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya. Tofauti na mtazamo mpana wa UNEP, utafiti huu unachanganua kwa kina aina za changamoto za kimazingira zinazoibuliwa katika vipindi hivyo, suluhisho zinazopendekezwa, pamoja na mbinu za mawasiliano zinazotumiwa kufikisha ujumbe kwa hadhira. Hivyo, utafiti huu hauishii katika kuangalia kama vijana au jamii wanapaswa kuchukua hatua za mazingira, bali unachunguza namna televisheni inavyowasilisha, kuunda na kusambaza

maarifa hayo kwa hadhira kupitia maudhui na mbinu mbalimbali za mawasiliano. Aidha, tofauti nyingine inajitokeza katika muktadha wa kijiografia na kijamii.

UNEP (2021) inatoa mifano kutoka maeneo mbalimbali duniani na inalenga hadhira ya vijana kwa mtazamo wa kimataifa. Utafiti huu unazingatia muktadha wa Kenya na kuchunguza vipindi vinavyowasilisha changamoto zinazowakabili wananchi katika mazingira yao halisi, kama ukame na uhaba wa maji, mmomonyoko wa udongo, kupungua kwa rutuba ya udongo, upotevu wa bioanuwai, uchafuzi wa mazingira, usimamizi wa taka na uharibifu wa misitu. Hivyo, utafiti huu una nafasi ya kuonesha namna ujumbe mpana wa mazingira unavyotafsiriwa katika mazingira ya Kenya kupitia maudhui yanayohusiana na maisha ya kila siku ya jamii. Pamoja na mchango wa UNEP (2021) katika kueleza umuhimu wa maarifa, mawasiliano na ushiriki wa vijana katika kushughulikia changamoto za mazingira, pengo linalojitokeza ni ukosefu wa uchambuzi wa kimuktadha unaochunguza kwa kina namna televisheni za Kenya zinavyowasilisha masuala ya uhifadhi wa mazingira na kuwafikishia wananchi ujumbe wa kimazingira. GEO-6 for Youth inaonesha umuhimu wa kutumia mawasiliano rafiki kwa vijana, video, infografiki na mifano ya vitendo ili kuongeza uelewa na kuchochea hatua, lakini haichanganui maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kama mifano maalumu ya vipindi vya televisheni nchini Kenya. Kwa msingi huo, utafiti huu unaziba pengo la kimuktadha na kimawasiliano kwa kuchanganua vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* ili kubainisha masuala ya mazingira yanayowasilishwa, changamoto za kimazingira zinazojitokeza, mikakati ya mawasiliano inayotumiwa katika kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Kwa kufanya hivyo, utafiti unaongeza maarifa kuhusu namna televisheni inaweza kutumika si tu kama chanzo cha taarifa, bali pia kama chombo cha elimu, uhamasishaji na kuchochea hatua za jamii katika uhifadhi wa mazingira.

Aidha, utafiti wa *Intergovernmental Panel on Climate Change* (IPCC) (2021**)** unaweka msingi wa kisayansi kuhusu changamoto za mabadiliko ya tabianchi na athari zake kwa mifumo ya ikolojia, rasilimali za asili na ustawi wa jamii. Ripoti hii inaonesha kuwa mabadiliko ya tabianchi yanahusishwa na ongezeko la ukame, mafuriko, uharibifu wa ardhi, upotevu wa bioanuai na shinikizo kwa rasilimali za maji, hivyo kuhitaji hatua za kukabiliana na athari hizo katika ngazi mbalimbali za jamii. Kwa msingi huo, utafiti wa IPCC unakubaliana na utafiti huu kwa kutambua umuhimu wa kuelimisha na kuwasiliana na jamii kuhusu changamoto za mazingira na hatua za uhifadhi, na masuala haya yanaweza kuonekana katika maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika eneo la uchambuzi kwa sababu utafiti wa IPCC unajikita katika kutoa ushahidi wa kisayansi kuhusu mabadiliko ya tabianchi na hatua za

kukabiliana nayo. Kwa upande mwingine, utafiti huu unajikita katika uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira kupitia vipindi maalumu vya televisheni nchini Kenya. Kwa hiyo, IPCC inaonesha mabadiliko ya tabianchi yanaathiri mifumo ya ikolojia na jamii na yanahitaji hatua za kukabiliana na athari zake, ilhali utafiti huu unalenga kubainisha jinsi masuala hayo ya mazingira yanavyowasilishwa kupitia televisheni, changamoto zinazosisitizwa na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa kufikisha ujumbe wa uhifadhi**.** Pengo linalojitokeza katika utafiti wa IPCC ni kwamba, licha ya kutoa ushahidi mpana wa kisayansi kuhusu changamoto za mazingira, haujachanganua jinsi ujumbe huo wa mazingira unavyowasilishwa kupitia vipindi mahususi vya televisheni kama *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika muktadha wa Kenya. Utafiti huu unaziba pengo hilo kwa kuchanganua mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, kwa kubainisha masuala ya mazingira yanayowasilishwa, changamoto za uhifadhi zinazojitokeza na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa na Runinga ya Citizen katika kufikisha ujumbe huo kwa watazamaji nchini Kenya. Kwa hivyo, mchango wa utafiti huu ni kuunganisha maarifa ya kisayansi kuhusu changamoto za mazingira yanayotolewa na IPCC na namna masuala hayo yanavyotafsiriwa na kuwasilishwa kupitia maudhui ya televisheni.

Utafiti wa Guenther et al. (2024) katika *Communicating Climate Change*: *Why Frames Matter for Public Engagement* una mchango muhimu katika kuelewa nafasi ya namna ujumbe wa mabadiliko ya tabianchi unavyowasilishwa katika kujenga uelewa wa umma kuhusu masuala ya mazingira. Nisbet anaeleza kuwa namna taarifa za mazingira zinavyowekwa katika mifumo mbalimbali ya uwasilishaji, inaweza kuathiri jinsi masuala ya mazingira yanavyoeleweka na kutafsiriwa na umma. Kwa msingi huo, utafiti huu unakubaliana na utafiti wa uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa kutambua umuhimu wa namna ujumbe wa mazingira unavyowasilishwa, hasa uchaguzi wa masuala, mifano, lugha na mbinu zinazotumika katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Hata hivyo, unatofautiana katika eneo na mbinu ya uchambuzi**.** Guenther et al. (2024) anajadili kwa upana dhana ya uundaji wa mtazamo katika mawasiliano ya mabadiliko ya tabianchi, wakati utafiti huu unachanganua maudhui halisi ya vipindi viwili vya Runinga ya Citizen katika muktadha wa Kenya, ukiangalia masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto zinazowasilishwa na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa. Kwa hivyo, utafiti wa Guenther et al. unaonesha kwamba namna ujumbe wa tabianchi unavyowasilishwa ni muhimu katika mawasiliano na ushirikishwaji wa umma, wakati utafiti huu unalenga kuonesha jinsi kanuni hizo za mawasiliano zinavyojitokeza katika maudhui ya vipindi

vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Pengo linalojitokeza katika utafiti wa Guenther et al. ni kwamba haujachanganua kwa kina mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi mahususi vya televisheni nchini Kenya, hasa namna *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vinavyowasilisha changamoto za mazingira na mikakati ya kukabiliana nazo. Vilevile, utafiti wa Guenther et al haujachanganua kwa pamoja vipindi hivi viwili ili kubaini mfanano na tofauti katika mikakati yao ya mawasiliano. Utafiti huu unaziba pengo hilo kwa kuchanganua maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* ili kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, changamoto za kimazingira zinazojitokeza na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa na Runinga ya Citizen katika kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Kwa hivyo, mchango wa utafiti huu ni kutoa ushahidi wa kimuktadha kuhusu jinsi mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira yanavyotekelezwa katika maudhui halisi ya televisheni**.**

Utafiti wa CGIAR (2023) kuhusu *Shamba Shape-Up: The TV Show Reshaping Agriculture in East Africa* una mchango muhimu katika kueleza nafasi ya televisheni katika kusambaza maarifa kuhusu kilimo endelevu, uhifadhi wa mazingira na matumizi bora ya rasilimali za asili katika Afrika Mashariki. Utafiti huu unakubaliana na utafiti huu kwa kutambua kuwa *Shamba Shape-Up,* kipindi kinachopeperushwa kupitia Runinga ya Citizen, kinawasilisha masuala yanayohusiana na uhifadhi wa mazingira, yakiwemo uhifadhi wa udongo, matumizi bora ya maji, upandaji wa miti, utunzaji wa vyanzo vya maji na mbinu za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Tafiti zote mbili, kwa hiyo, zinatambua umuhimu wa mawasiliano ya televisheni katika kuwasilisha maarifa na ujumbe unaohusiana na matumizi endelevu ya rasilimali na uhifadhi wa mazingira. Hata hivyo, zinatofautiana katika eneo la uchambuzi na upeo wa utafiti. CGIAR (2023) imejikita zaidi katika *Shamba Shape-Up* kama chombo cha kuwasilisha maarifa ya kilimo na kuboresha uelewa wa wakulima kuhusu mbinu endelevu za uzalishaji, wakati utafiti huu unachunguza kwa upana zaidi mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi viwili, yaani *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*.

Kwa hiyo, utafiti wa CGIAR (2023) unahusu zaidi mchango wa *Shamba Shape-Up* katika usambazaji wa maarifa ya kilimo na mbinu zinazoweza kusaidia uzalishaji endelevu, ilhali utafiti huu unalenga kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, changamoto za kimazingira zinazojitokeza na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi. Pengo linalojitokeza ni kwamba CGIAR (2023) haijachanganua kwa kina *Citizen Planet* na haijaweka pamoja vipindi hivi viwili ili kubaini mfanano na tofauti katika namna vinavyowasilisha mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Aidha, utafiti huo

haujajikita katika uchambuzi wa vipengele vya mawasiliano vinavyotumiwa katika vipindi hivyo kama vile lugha, picha, maelezo ya wataalamu, mifano ya vitendo na mbinu za elimu na burudani kwa mtazamo wa uhifadhi wa mazingira. Kwa hivyo, utafiti huu unaziba pengo hilo kwa kufanya uchambuzi linganishi wa *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* ili kubainisha maudhui ya uhifadhi wa mazingira, changamoto za kimazingira na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa na Runinga ya Citizen katika kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Hivyo, mchango wa utafiti huu ni kupanua mjadala ulioanzishwa na CGIAR (2023) kutoka katika mkazo wa mawasiliano ya kilimo endelevu kuelekea uchambuzi mpana wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi viwili vya televisheni, huku ukitoa ushahidi wa kimuktadha kuhusu namna ujumbe wa mazingira unavyoundwa na kuwasilishwa kupitia Runinga ya Citizen.

Utafiti wa Marles, V. (2022). *Shamba Shape-Up Series 12: Impact of Viewing on Farmers' Knowledge, Attitudes and Practices* una mchango muhimu katika kueleza uhusiano kati ya maudhui ya televisheni na maarifa, mitazamo na matendo ya watazamaji kuhusu kilimo na matumizi endelevu ya rasilimali za asili. Utafiti huo unakubaliana na utafiti huu kwa kuonesha kuwa *Shamba Shape-Up* huwasilisha maarifa yanayohusiana na uhifadhi wa mazingira, yakiwemo uvunaji wa maji ya mvua, uhifadhi wa udongo, kilimo mseto, upandaji wa miti na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Tafiti zote mbili, hivyo, zinatambua umuhimu wa *Shamba Shape-Up* katika kuwasilisha maudhui yanayohusiana na matumizi endelevu ya rasilimali na uhifadhi wa mazingira. Hata hivyo, zinatofautiana katika lengo, mbinu na eneo la uchambuzi. Marles (2022) ilijikita katika kutathmini maarifa, mitazamo na matendo ya wakulima baada ya kutazama kipindi, wakati utafiti huu unajikita katika uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa ndani ya vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Kwa hiyo, utafiti wa Marles (2022) unaonesha uhusiano kati ya kutazama kipindi na mabadiliko katika maarifa, mitazamo na baadhi ya matendo ya watazamaji, ilhali utafiti huu haupimi athari za vipindi kwa watazamaji bali unachunguza maudhui na namna ujumbe wa uhifadhi unavyowasilishwa.

Pengo linalojitokeza katika utafiti wa Marles (2022) ni kwamba haujachanganua kwa kina muundo na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira, wala haujalinganisha *Shamba Shape-Up* na kipindi kingine cha mazingira kama *Citizen Planet*. Aidha, haujatoa uchambuzi mpana wa masuala mbalimbali ya uhifadhi yanayowasilishwa katika vipindi hivyo, kama vile uchafuzi wa mazingira, upotevu wa bioanuai, uharibifu wa misitu, usimamizi wa taka, uhifadhi wa maji na athari za shughuli za binadamu kwa mazingira. Utafiti huu unaziba pengo hilo kwa kuchanganua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* ili kubainisha

masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, changamoto za kimazingira zinazojitokeza na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa na Runinga ya Citizen katika kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Kwa hivyo, mchango wa utafiti huu ni kuchanganua maudhui na mchakato wa mawasiliano wenyewe, na hivyo kutoa uelewa mpana zaidi wa namna Runinga ya Citizen inavyowasilisha ajenda ya uhifadhi wa mazingira kupitia vipindi hivi viwili.

Mediae (2021), katika utafiti unaoitwa Mediae *Shamba Shape-Up Series 11: Knowledge, Attitude and Practices Report*, anaeleza mchango wa kipindi cha *Shamba Shape-Up* katika kuongeza maarifa na uelewa wa watazamaji kuhusu mbinu za kilimo zinazohusiana na matumizi endelevu ya rasilimali za asili na uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Utafiti huu unakubaliana na utafiti huu kwa kubainisha kuwa *Shamba Shape-Up* huwasilisha maudhui yanayohusiana na uhifadhi wa udongo, matumizi bora ya maji, upandaji wa miti, matumizi ya mbinu endelevu za kilimo na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Tafiti zote mbili, kwa hiyo, zinatambua umuhimu wa kipindi katika kuwasilisha ujumbe unaohusiana na uhifadhi wa mazingira kupitia televisheni. Hata hivyo, zinatofautiana katika lengo na mbinu ya utafiti. Mediae (2021) ilijikita katika kuchunguza maarifa, mitazamo na matendo ya watazamaji kuhusiana na kipindi, wakati utafiti huu unalenga kuchanganua mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*.

Kwa hivyo, utafiti huu unachanganua maudhui na namna ujumbe wa uhifadhi wa mazingira unavyowasilishwa. Pengo la utafiti wa Mediae (2021) ni kwamba umejikita zaidi katika uhusiano wa kipindi na maarifa, mitazamo na matendo yanayohusiana na kilimo, bila kuchanganua kwa kina muundo wa mawasiliano, masuala mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira na mikakati inayotumiwa katika kuwasilisha ujumbe huo. Aidha, haujachunguza *Citizen Planet* wala kulinganisha namna vipindi hivyo viwili vinavyowasilisha masuala ya mazingira. Hivyo, eneo ambalo bado halijafanyiwa utafiti wa kutosha ni uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi viwili vya Runinga ya Citizen kwa muktadha wa Kenya**.** Utafiti huu unaziba pengo hilo kwa kuchanganua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* ili kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, changamoto za kimazingira zinazojitokeza na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa katika kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Kwa hivyo, mchango wa utafiti huu ni kupanua uelewa uliotolewa na Mediae (2021) kutoka katika mtazamo wa maarifa, mitazamo na matendo ya watazamaji hadi katika uchambuzi wa maudhui na mchakato wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira.

Utafiti wa Mediae (2022) International *Food Policy Research Institute (IFPRI) kwa kushirikiana na Wageningen University* unaojulikana kama *Edutainment's Positive Influence on Social Norms and Behaviours* una mchango muhimu katika kueleza nafasi ya mawasiliano ya elimu-burudani katika kuwasilisha maarifa yanayohusiana na matumizi endelevu ya rasilimali za asili na masuala ya mazingira. Utafiti huu unakubaliana na utafiti huu kwa kuonesha umuhimu wa vipindi vya televisheni, hususan *Shamba Shape-Up*, katika kuwasilisha maarifa kuhusu matumizi endelevu ya ardhi, uhifadhi wa maji, utunzaji wa rutuba ya udongo, upandaji wa miti na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Tafiti zote mbili zinatambua kuwa elimu burudani ni mkakati muhimu wa mawasiliano unaoweza kufanya ujumbe wa mazingira na kilimo kuwa rahisi kueleweka na kufikika kwa hadhira pana. Hata hivyo, zinatofautiana katika lengo, mbinu na aina ya ushahidi unaotumika. Utafiti wa IFPRI na Wageningen University (2022) ulijikita katika kutathmini mabadiliko ya mitazamo, kanuni za kijamii na tabia zinazohusishwa na kutazama maudhui ya *Shamba Shape-Up*, wakati utafiti huu unalenga kuchanganua mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira yanayojitokeza katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*.

Kwa hivyo, utafiti huu unachanganua maudhui na namna ujumbe wa uhifadhi unavyowasilishwa katika vipindi. Pengo la utafiti huo ni kwamba haujachanganua kwa kina maudhui ya mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira yenyewe, wala haujalinganisha *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* ili kubaini tofauti na mfanano wa masuala ya mazingira na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa katika vipindi hivyo. Aidha, haujaweka mkazo wa kutosha katika muktadha wa mawasiliano ya mazingira nchini Kenya, hasa katika vipindi vinavyolenga masuala mapana kama uchafuzi wa mazingira, uhifadhi wa misitu, upotevu wa bioanuai na usimamizi wa taka. Utafiti huu unaziba pengo hilo kwa kuchanganua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* ili kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, changamoto za kimazingira zinazojitokeza na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa na Runinga ya Citizen katika kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Hivyo, mchango wa utafiti huu ni kuchanganua maudhui na mchakato wa mawasiliano wenyewe, na hivyo kutoa uelewa wa kimuktadha kuhusu namna ujumbe wa uhifadhi wa mazingira unavyoundwa na kuwasilishwa kupitia vipindi hivi viwili.

Utafiti wa Mediae (2020) unaoitwa *Shamba Shape-Up Series 10: Knowledge, Attitude and Practices Survey Report* una mchango muhimu katika kueleza nafasi ya kipindi cha *Shamba Shape-Up* katika kuwasilisha maarifa kuhusu kilimo endelevu na matumizi ya rasilimali za asili nchini Kenya. Utafiti huu unakubaliana na utafiti huu kwa kubainisha kuwa *Shamba Shape-Up* huwasilisha masuala yanayohusiana na uhifadhi wa mazingira, yakiwemo uhifadhi wa udongo

dhidi ya mmomonyoko, matumizi bora na uvunaji wa maji ya mvua, matumizi ya mbinu rafiki kwa mazingira, upandaji wa miti na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Tafiti zote mbili, kwa hivyo, zinatambua nafasi ya televisheni katika kuwasilisha maarifa na ujumbe unaohusiana na matumizi endelevu ya rasilimali za asili na uhifadhi wa mazingira. Hata hivyo, zinatofautiana katika lengo, mbinu na aina ya data.

Mediae (2020) ilijikita katika kuchunguza maarifa, mitazamo na matendo ya watazamaji wa *Shamba Shape-Up*, wakati utafiti huu unalenga uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Kwa hivyo, utafiti huu unachanganua maudhui na namna ujumbe wa uhifadhi wa mazingira unavyowasilishwa. Pengo katika utafiti wa Mediae (2020) ni kwamba umejikita zaidi katika kutathmini maarifa, mitazamo na matendo yanayohusiana na kilimo, bila kufanya uchambuzi wa kina wa maudhui ya mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira, changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa katika vipindi hivyo. Aidha, haujachunguza *Citizen Planet* wala kulinganisha vipindi hivyo viwili katika kuwasilisha masuala ya mazingira nchini Kenya. Hivyo, eneo ambalo bado halijafanyiwa utafiti wa kutosha ni uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi viwili vya Runinga ya Citizen kwa kuzingatia muktadha wa Kenya. Utafiti huu unaziba pengo hilo kwa kuchanganua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* ili kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, changamoto za kimazingira zinazojitokeza na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa katika kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Kwa hivyo, mchango wa utafiti huu ni kuongeza uelewa kuhusu mchakato wa uwasilishaji wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira, na hivyo kupanua mjadala wa kitaaluma hadi katika maudhui na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa na Runinga ya Citizen.

Langat (2021), *katika utafiti wake kuhusu Communicating Agricultural Information Using Electronic Media*: The Case of "*Shamba Shape-Up*" *Programme on Citizen Television in Kenya,* anaonyesha kuwa *Shamba Shape-Up* ni chombo muhimu cha kuwasilisha taarifa za kilimo endelevu na matumizi bora ya rasilimali za asili. Utafiti wake unaonyesha kuwa kipindi huwasilisha maarifa kuhusu uhifadhi wa udongo, uvunaji wa maji ya mvua, upandaji wa miti, kilimo mseto, matumizi ya mbolea za asili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Matokeo haya yanaendana na utafiti huu kwa kuonyesha umuhimu wa *Shamba Shape-Up* katika kuwasilisha ujumbe unaohusiana na matumizi endelevu ya mazingira. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika mbinu na eneo la uchunguzi. Langat (2021) alichunguza mawasiliano ya taarifa za kilimo na athari zake kwa watazamaji, wakati utafiti huu umetumia uchanganuzi wa

nyaraka na maudhui ya vipindi. Utafiti huu, unachunguza maudhui yanayowasilishwa katika vipindi na namna ujumbe wa uhifadhi wa mazingira unavyojengwa na kuwasilishwa.

Kwa upande mwingine, utafiti wa Langat ulijikita zaidi katika mawasiliano ya kilimo na haukuchambua kwa upana masuala kama uchafuzi wa mazingira, usimamizi wa taka, ukataji miti, upotevu wa bioanuai na masuala mengine mapana ya uhifadhi. Aidha, haukuhusisha *Citizen Planet*. Hivyo, pengo linaloendelea kuwepo ni ukosefu wa uchambuzi mpana wa maudhui ya mazingira yanayowasilishwa kupitia vipindi mbalimbali vya Runinga ya Citizen. Utafiti huu unaongezea maarifa kwa kuchambua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kama vyanzo vya mawasiliano ya mazingira, kubainisha masuala na changamoto za uhifadhi zinazowasilishwa, kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika na kubainisha ushirikiano wa Runinga ya Citizen na washika dau mbalimbali. Hivyo, utafiti huu unajengwa kutokana na ule wa Langat (2021), lakini unapanua mjadala kutoka mawasiliano ya taarifa za kilimo na athari zake kwa watazamaji hadi uchambuzi wa maudhui na mikakati ya mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira nchini Kenya.

Salawu (2021), katika A*frican Media and Environmental Sustainability: Challenges and Opportunities*, anachunguza nafasi ya vyombo vya habari katika mawasiliano ya mazingira na uendelevu barani Afrika**.** Utafiti unaonesha kuwa vyombo vya habari huwasilisha masuala mbalimbali ya kimazingira, yakiwemo mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa misitu, uchafuzi wa mazingira na upotevu wa bioanuwai. Matokeo haya yanaendana na utafiti huu kwa kuwa yote yanatambua mawasiliano ya mazingira kama eneo muhimu la kuwasilisha changamoto za kimazingira na njia za uhifadhi**.** Hata hivyo, Salawu (2021) anajadili suala hili kwa mtazamo mpana wa vyombo vya habari barani Afrika, wakati utafiti huu unajikita katika uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi maalumu vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya**.**

Tofauti hiyo inaonesha pengo ambalo utafiti huu unalenga kulijaza, kwa kuwa Salawu (2021) hakuingia kwa kina katika kuchanganua maudhui mahsusi ya vipindi hivi, changamoto za mazingira zinazowakilishwa na mikakati ya kimawasiliano inayotumiwa kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi**.** Utafiti huu unaendeleza mjadala huo kwa kuchanganua namna vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vinavyowasilisha masuala kama uhifadhi wa udongo na maji, kilimo endelevu, uhifadhi wa misitu, bioanuwai na usimamizi wa taka**.** Aidha, utafiti unachunguza namna lugha, picha, mahojiano, simulizi na maonyesho ya vitendo vinavyotumika katika kujenga ujumbe wa mazingira. Kwa mtazamo wa Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia, uchambuzi huu unaangalia pia

namna vipindi hivyo vinavyowakilisha uhusiano kati ya binadamu na mazingira, matumizi ya rasilimali za asili na umuhimu wa uendelevu. Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kwa kuhamisha mjadala kutoka katika mtazamo mpana wa vyombo vya habari barani Afrika hadi katika uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi mahususi vya televisheni nchini Kenya.

Utafiti wa African Development Bank (ADB, 2022), *African Economic Outlook 2022: Supporting Climate Resilience and a Just Energy Transition in Africa* unaonyesha umuhimu wa mawasiliano ya mazingira katika kuongeza uelewa wa jamii kuhusu changamoto za kimazingira. Ripoti inaainisha mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa misitu, upotevu wa bioanuai, uchafuzi wa maji na hewa, pamoja na uharibifu wa ardhi kuwa miongoni mwa changamoto muhimu barani Afrika. Matokeo haya yanakubaliana na utafiti huu kwa kuonyesha kuwa mawasiliano kupitia vyombo vya habari yanaweza kutoa elimu kuhusu mazingira na kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali. Tafiti zote zinaonyesha pia umuhimu wa kuwasilisha changamoto za mazingira pamoja na hatua za kukabiliana nazo. Hata hivyo, zinatofautiana katika upeo wa uchunguzi. ADB (2022) inatoa mtazamo mpana wa mazingira barani Afrika. Utafiti huu unajikita katika muktadha wa Kenya. Aidha, ADB haichambui kwa kina maudhui ya vipindi maalumu kama *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*.

Ripoti hiyo inaonyesha kwamba mawasiliano bora ya mazingira ni muhimu katika kuongeza uelewa na kuhamasisha jamii kuhusu hatua za uhifadhi. Hata hivyo, eneo ambalo halijafanyiwa utafiti wa kutosha ni namna vipindi vya televisheni nchini Kenya vinavyowasilisha masuala hayo. Bado haijabainishwa kwa kina ni masuala gani ya uhifadhi yanapewa kipaumbele na ni mikakati gani ya mawasiliano inayotumika. Aidha, utafiti huu unachanganua maudhui ya vipindi na nyaraka zinazohusiana navyo. Utafiti huu unaongezea maarifa kwa kuchambua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika muktadha wa Kenya. Unabainisha masuala na changamoto za mazingira zinazowasilishwa. Pia, unachunguza mikakati ya mawasiliano inayotumiwa kufikisha ujumbe wa uhifadhi. Hivyo, utafiti huu unapanua mjadala wa ADB (2022) kutoka mtazamo mpana wa mawasiliano ya mazingira barani Afrika hadi uchambuzi mahsusi wa maudhui na mikakati ya mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya Runinga ya Citizen nchini Kenya**.**

Tshabangu et al (2021) katika *Indigenous-Language Media Research in Africa: Gains, Losses, Towards a New Research Agenda,* anaeleza nafasi ya vyombo vya habari katika kuongeza uelewa wa jamii kuhusu mazingira. Utafiti huo unaonyesha kuwa vyombo vya habari huibua masuala kama uharibifu wa misitu, mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa mazingira na upotevu wa

bioanuai. Matokeo haya yanakubaliana na utafiti huu kwa kuonyesha kuwa vyombo vya habari vina nafasi katika kuwasilisha elimu ya mazingira na kukuza uelewa kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali. Tafiti zote zinaonyesha pia umuhimu wa mawasiliano ya mazingira katika kuibua changamoto na suluhisho za uhifadhi. Hata hivyo, zinatofautiana katika upeo wa utafiti. Tshabangu et al (2021) anajadili nafasi ya vyombo vya habari kwa mtazamo mpana wa Afrika. Utafiti huu unajikita katika vipindi maalumu vya Runinga ya Citizen nchini Kenya. Aidha, Nyamnjoh hajachambua kwa kina *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kama vipindi vya mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira.

Kwa hivyo, utafiti wake unaonyesha kwamba vyombo vya habari vinaweza kusaidia kujenga uelewa wa jamii kuhusu mazingira na kuunga mkono maendeleo endelevu. Hata hivyo, bado kuna pengo katika kuelewa ni maudhui gani ya mazingira yanawasilishwa na ni mikakati gani ya mawasiliano inayotumiwa katika vipindi maalumu vya televisheni nchini Kenya. Pia, Nyamnjoh hajabainisha kwa kina ushirikiano kati ya vyombo vya habari na washika dau wa mazingira katika kuendeleza uhifadhi. Utafiti huu unaongezea maarifa kwa kuchambua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika muktadha wa Kenya. Unabainisha masuala na changamoto za mazingira zinazowasilishwa. Pia, unachunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi. Hivyo, utafiti huu unapanua mjadala wa Tshabangu (2021) kutoka mtazamo mpana wa Afrika hadi uchambuzi mahsusi wa maudhui na mikakati ya mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya Runinga ya Citizen nchini Kenya.

Siyao (2021*). Sources of Climate Change Information Used by Newspaper Journalists in Tanzania* anachunguza namna vyombo vya habari vya utangazaji vinavyowasilisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi na changamoto zinazohusiana na mazingira katika Afrika Mashariki. Utafiti unaonesha kuwa vyombo kama runinga na redio huwasilisha masuala yanayohusiana na ukame, mafuriko, uharibifu wa misitu, uchafuzi wa maji na hewa pamoja na upotevu wa bioanuwai**.** Matokeo haya yanaendana na utafiti huu kwa kuwa yote yanazingatia mawasiliano ya mazingira na namna vyombo vya habari vinavyowasilisha changamoto za kimazingira. Hata hivyo, Siyao (2021) anajadili mawasiliano ya mabadiliko ya tabianchi kwa mtazamo mpana wa Afrika Mashariki, wakati utafiti huu unalenga uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi teule vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya.

Pamoja na mchango wa Siyao (2021), bado kuna pengo katika kuchanganua maudhui mahususi ya uhifadhi wa mazingira na namna ujumbe huo unavyoundwa na kuwasilishwa katika vipindi

teule vya televisheni nchini Kenya. Utafiti wa Siyao haujajikita katika kuchanganua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* wala mikakati ya kimawasiliano inayotumika katika vipindi hivyo. Utafiti huu unalenga kuziba pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, changamoto zinazohusishwa na uharibifu wa mazingira na mikakati ya mawasiliano kama matumizi ya lugha, picha, mahojiano, simulizi na maonyesho ya vitendo. Aidha, kwa kuzingatia Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia, utafiti huu unachanganua namna maudhui ya vipindi hivyo yanavyowakilisha uhusiano kati ya binadamu na mazingira, matumizi ya rasilimali za asili, athari za shughuli za binadamu katika mifumo ya ikolojia na umuhimu wa uhifadhi**.** Hivyo, utafiti huu unaendeleza mjadala wa Siyao (2021) kutoka katika mtazamo mpana wa mawasiliano ya tabianchi Afrika Mashariki hadi uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi teule vya Runinga ya Citizen nchini Kenya**.**

Utafiti wa Chemarum (2023)**,** *Coverage of Environmental Issues by the Kenyan Media: A case study of Citizen Televisio*n unaeleza nafasi ya mawasiliano ya umma katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha uhifadhi wa mazingira. Mkakati huo unaonyesha kuwa vyombo vya habari, elimu kwa umma na kampeni za uhamasishaji vinaweza kusaidia jamii kuelewa changamoto kama ukame, mafuriko, uharibifu wa ardhi, uhaba wa maji na upotevu wa bioanuai. Matokeo haya yanakubaliana na utafiti huu kwa kuonyesha kuwa mawasiliano ni muhimu katika kuwasilisha changamoto za mazingira na hatua za kukabiliana nazo. Tafiti zote pia zinasisitiza umuhimu wa kuongeza uelewa wa jamii kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za asili. Hata hivyo, zinatofautiana katika upeo wa uchunguzi. Chemarum (2023) inazingatia mawasiliano ya mabadiliko ya tabianchi kwa mtazamo wa kikanda. Utafiti huu unalenga maudhui ya vipindi maalumu vya Runinga ya Citizen nchini Kenya. Chemarum pia haichambui kwa kina *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* wala mikakati ya mawasiliano inayotumika katika vipindi hivyo. Kwa ujumla, mkakati huo unahimiza kwamba mawasiliano ya mazingira na ushirikiano wa kikanda ni muhimu katika kuongeza uelewa na kuchochea hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, bado kuna pengo la utafiti kuhusu namna mikakati hiyo inavyotekelezwa kupitia vipindi maalumu vya televisheni nchini Kenya. Pia, haijaelezwa kwa kina ni masuala gani ya uhifadhi yanapewa kipaumbele na vipindi hivyo. Utafiti huu unaongezea maarifa kwa kuchambua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika muktadha wa Kenya. Unabainisha masuala na changamoto za mazingira zinazowasilishwa. Pia unachunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi. Hivyo, utafiti huu unapanua mjadala wa Chemarum (202) kutoka mkakati wa mawasiliano wa kikanda hadi uchambuzi wa maudhui na

mikakati ya mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya Runinga ya Citizen nchini Kenya.

Utafiti wa Shobande et al (2022), *The Critical Role of Education and ICT in Promoting Environmental Sustainability in Eastern and Southern Africa* ambao unachunguza nafasi ya runinga katika kuongeza uelewa wa umma kuhusu uendelevu wa mazingira. Shobande et al wanaonyesha kuwa runinga huwasilisha masuala kama mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa misitu, uchafuzi wa maji na hewa, upotevu wa bioanuai na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali. Matokeo haya yanakubaliana na utafiti huu kwa kuonyesha kuwa runinga ni chombo muhimu cha kuwasilisha ujumbe wa mazingira. Tafiti zote zinaonyesha kuwa maudhui ya mazingira yanaweza kusaidia kujenga uelewa kuhusu changamoto za uhifadhi na umuhimu wa matumizi endelevu ya rasilimali. Hata hivyo, zinatofautiana katika upeo wa uchunguzi**.** Shobande et al (2022) wanatoa mtazamo mpana wa Afrika Mashariki. Utafiti huu unajikita katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* nchini Kenya. Shobande et al pia hawajachambua kwa kina maudhui maalumu ya vipindi hivi wala mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi.

Kwa hivyo, utafiti wake unaunyesha kwamba runinga inaweza kuwa nyenzo muhimu ya kuongeza uelewa wa umma kuhusu uendelevu wa mazingira. Hata hivyo, bado kuna pengo kuhusu maudhui yanayowasilishwa na vipindi maalumu vya Runinga ya Citizen na namna ujumbe huo unavyowasilishwa. Utafiti huu unaongezea maarifa kwa kuchambua maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Unabainisha changamoto za mazingira zinazowasilishwa. Pia unachunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi. Hivyo, utafiti huu unapanua mjadala wa Shobande et al (2022) kutoka mtazamo mpana wa Afrika Mashariki hadi uchambuzi mahsusi wa uchambuzi wa mawasiliano wa mazingira katika vipindi teule vya Runinga ya Citizen nchini Kenya.

Monyenye et al. (2023) katika utafiti wao wa *Mass Media and Environmental Conservation Awareness in Kenya*, wanatoa mchango muhimu katika kuelewa nafasi ya vyombo vya habari katika kuimarisha uelewa wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya kupitia ongezeko la ufahamu wa jamii kuhusu changamoto za kimazingira na wajibu wao katika kulinda mifumo ya ikolojia. Monyenye et al wanaeleza kuwa vyombo vya habari, hususan runinga, vina uwezo mkubwa wa kuathiri mitazamo ya jamii kuhusu masuala ya mazingira kama vile mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa maji na hewa, uharibifu wa misitu, upotevu wa bioanuwai na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za asili. Matokeo haya yanakubaliana na utafiti huu kwa kuonyesha kuwa

runinga ni chombo muhimu cha kuelimisha jamii kuhusu changamoto za mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali.

Tafiti zote pia zinasisitiza umuhimu wa mawasiliano ya mazingira katika kukuza uelewa kuhusu uhifadhi. Hata hivyo, zinatofautiana katika upeo na namna ya uchambuzi**.** Monyenye et al wanachunguza vyombo vya habari kwa mtazamo mpana nchini Kenya. Utafiti huu unajikita katika vipindi maalumu vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Monyenye et al pia hajachambua kwa kina maudhui ya vipindi hivyo na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi. Kwa hivyo, utafiti wao unafikia hoja kwamba vyombo vya habari vinaweza kuwa nyenzo muhimu ya kuongeza uelewa na kuhamasisha jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira. Hata hivyo, bado kuna pengo la utafiti kuhusu maudhui mahsusi ya mazingira yanayowasilishwa katika vipindi vya Runinga ya Citizen. Pia, haijachunguzwa kwa kina namna vipindi hivyo vinavyotumia mikakati mbalimbali ya mawasiliano na kushirikiana na washika dau katika kuendeleza uhifadhi. Utafiti huu unaongezea maarifa kwa kuchambua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa pamoja. Unabainisha masuala na changamoto za mazingira zinazowasilishwa. Pia unachunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi. Hivyo, utafiti huu unajenga juu ya Monyenye et al (2023) kwa kuendeleza mjadala kuhusu nafasi ya vyombo vya habari katika masuala ya mazingira, lakini unautofautisha kwa kuuelekeza katika uchambuzi mahsusi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira**.** Utafiti huu unachanganua maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya, kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa katika kuwasilisha ujumbe huo. Kwa msingi huo, utafiti unaongeza maarifa kuhusu namna vipindi teule vya televisheni vinavyowakilisha uhusiano kati ya binadamu na mazingira, matumizi ya rasilimali za asili na umuhimu wa uhifadhi, kwa kuzingatia mtazamo wa Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia.

Utafiti wa *National Environment Management Authority (2022)* katika *State of Environment Report Kenya* unatoa tathmini ya kina kuhusu hali ya mazingira nchini Kenya na mchango wake katika kuelewa umuhimu wa kuimarisha uhifadhi wa mazingira kupitia usimamizi endelevu wa rasilimali za asili. Ripoti hii inaeleza kuwa Kenya inakabiliwa na changamoto kubwa za kimazingira kama vile uharibifu wa misitu, upotevu wa bioanuwai, uchafuzi wa maji na hewa, uharibifu wa ardhi, pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi kama ukame na mafuriko, hali inayotishia ustawi wa mifumo ya ikolojia na maisha ya binadamu. Ripoti ya National Environment Management Authority (NEMA) inaonyesha kuwa uelewa wa umma kuhusu hali ya mazingira ni

muhimu katika kuimarisha uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za asili nchini Kenya. Mtazamo huu unakubaliana na utafiti huu kwa kuonyesha umuhimu wa elimu na uhamasishaji wa mazingira.

Pia, unaendana na maudhui ya *Shamba Shape-Up*, ambayo huwasilisha maarifa kuhusu matumizi endelevu ya ardhi, maji na rasilimali nyingine. Hata hivyo, NEMA na utafiti huu vinatofautiana katika lengo na chanzo cha data. NEMA inalenga kutoa taarifa kuhusu hali na changamoto za mazingira nchini. Utafiti huu unachanganua maudhui ya vipindi vya Runinga ya Citizen. Kwa hivyo, ripoti ya NEMA inahitimisha kwamba uelewa wa umma ni sehemu muhimu ya juhudi za uhifadhi. Hata hivyo, haijaonyesha kwa kina namna vyombo vya habari vinavyowasilisha ujumbe huo. Pia, haijachambua vipindi maalumu kama *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Hili linaonyesha pengo la utafiti katika kuelewa maudhui ya mazingira yanayowasilishwa na vipindi hivyo na mikakati inayotumiwa kufikisha ujumbe kwa watazamaji. Utafiti huu unaongezea maarifa kwa kuchambua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kama vyanzo vya mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira. Unabainisha masuala na changamoto za mazingira zinazowasilishwa. Pia unachunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi. Hivyo, utafiti huu unajenga juu ya taarifa za NEMA na kuongeza mtazamo wa kimawasiliano kuhusu namna uhifadhi wa mazingira unavyowasilishwa kupitia vipindi vya Runinga ya Citizen nchini Kenya.

Agalo et al (2024). *Media framing of climate change contents in news coverage in Kenya* katika utafiti wa *The Role of Television Media in Promoting Environmental Sustainability in Kenya*, anachunguza nafasi ya runinga katika kukuza uendelevu wa mazingira nchini Kenya. Utafiti unaonyesha kuwa runinga huibua masuala kama mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa misitu, uchafuzi wa maji na hewa, upotevu wa bioanuai na uharibifu wa ardhi. Matokeo haya yanakubaliana na utafiti huu kwa kuonyesha kuwa runinga ni chombo muhimu cha kuelimisha jamii kuhusu changamoto za mazingira. Tafiti zote zinaonyesha pia umuhimu wa mawasiliano katika kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali na hatua za uhifadhi. Hata hivyo, zinatofautiana katika upeo wa uchambuzi. Agalo et al (2025) wanajadili nafasi ya runinga kwa mtazamo mpana nchini Kenya. Utafiti huu unajikita katika vipindi maalumu vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Agalo et al pia hawajachambua kwa kina maudhui ya vipindi hivyo na mikakati inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi. Kwa hivyo, utafiti wake unabainisha kwamba runinga inaendelea kuwa nyenzo muhimu katika kuongeza uelewa wa mazingira na kukuza uwajibikaji wa jamii katika uhifadhi. Hata hivyo, bado kuna pengo kuhusu maudhui

mahsusi yanayowasilishwa katika vipindi vya Runinga ya Citizen. Pia, haijachunguzwa kwa kina namna vipindi hivyo vinavyotumia mikakati mbalimbali ya mawasiliano. Utafiti huu unaongezea maarifa kwa kuchambua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa pamoja. Unabainisha masuala na changamoto za mazingira zinazowasilishwa. Pia unachunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi. Hivyo, utafiti huu unajenga juu ya Agalo et al (2025), lakini unapanua mjadala kutoka mtazamo mpana wa nafasi ya runinga hadi uchambuzi mahsusi wa maudhui, changamoto na mikakati ya mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya Runinga ya Citizen nchini Kenya**.**

2.3 Changamoto Zinazoibuka Kutokana na Kutohifadhi Mazingira

Utafiti wa Carabajal et al (2024) kuhusu *Social and Economic Impact Analysis of Solar Mini-Grids in Rural Africa* unaonyesha umuhimu wa nishati safi katika kuboresha maisha ya jamii za vijijini na kupunguza utegemezi wa vyanzo vya nishati vinavyoweza kuathiri mazingira. Mtazamo huu unakubaliana na utafiti huu kwa kusisitiza umuhimu wa elimu na matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira. Pia, unaendana na hoja ya Agevi (2023) kwamba vyombo vya habari vinaweza kutoa elimu ya vitendo inayohusiana na maisha ya kila siku. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana na utafiti huu katika eneo la uchunguzi. Carabajal na wenzake wanazingatia zaidi athari za kijamii na kiuchumi za nishati ya jua. Utafiti huu unachanganua maudhui ya uhifadhi wa mazingira katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Tafiti hizo pia hazichambui kwa kina mikakati ya mawasiliano inayotumiwa na vipindi hivyo. Kwa ujumla, tafiti hizi zinaonyesha kuwa elimu pekee haitoshi kuhakikisha matumizi ya teknolojia na mbinu endelevu. Gharama, miundombinu na mazingira ya kijamii yanaweza kuathiri utekelezaji wa maarifa yanayopatikana. Hata hivyo, eneo ambalo halijafanyiwa utafiti wa kutosha ni namna vipindi vya Runinga ya Citizen vinavyowasilisha elimu kuhusu nishati safi na masuala mengine ya uhifadhi. Pia, haijachambuliwa kwa kina namna ujumbe huo unavyowasilishwa kupitia vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Utafiti huu unaongezea maarifa kwa kuchambua masuala ya uhifadhi yanayowasilishwa katika vipindi hivi. Pia unabainisha changamoto za mazingira na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe. Aidha, unaangalia ushirikiano wa Runinga ya Citizen na washika dau mbalimbali. Hivyo, utafiti huu unajenga juu ya tafiti zilizotangulia, pia unapanua mjadala kutoka matumizi ya nishati safi na elimu ya mazingira hadi uchambuzi wa maudhui na mikakati ya mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira kupitia vipindi vya Runinga ya Citizen nchini Kenya**.**

Potts et al. (2024) katika utafiti wao "*Global Biodiversity Threats & Protected Areas Expansion (30x30 Agenda)"* wanaeleza kuwa ongezeko la watu, mabadiliko ya matumizi ya ardhi na

mabadiliko ya tabianchi ni miongoni mwa tishio kuu kwa bioanuwai duniani. Watafiti hao wanakubaliana na utafiti huu unaosisitiza umuhimu wa elimu, uhamasishaji na ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi wa mazingira. Aidha, wanabainisha kuwa kufikia lengo la kuhifadhi asilimia 30 ya ardhi na bahari ifikapo mwaka 2030 kunahitaji ushirikiano wa jamii, serikali na wadau wengine. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika msisitizo. Potts et al. (2024) wanajikita zaidi katika upanuzi wa maeneo yaliyohifadhiwa na vitisho kwa bioanuwai, ilhali utafiti utafiti huu unahusu vyombo vya habari huzingatia zaidi nafasi ya mawasiliano katika kuongeza uelewa na kubadili mitazamo ya jamii. Tafiti hizi zimeafikiana kuwa elimu na ushirikishwaji wa jamii ni muhimu, lakini maarifa pekee hayatoshi bila sera madhubuti, motisha za kiuchumi na utekelezaji wa mikakati ya uhifadhi.

Pamoja na mchango huo, bado kuna pengo la utafiti kuhusu jinsi televisheni inavyowasilisha masuala ya bioanuwai na uhifadhi wa mazingira kwa jamii katika muktadha wa Kenya**.** Hasa, haijafafanuliwa kwa kina jinsi maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* yanavyowasilisha changamoto za uhifadhi, suluhisho zinazopendekezwa na mbinu za mawasiliano zinazotumiwa kuwafikia watazamaji. Utafiti huu unaziba pengo hilo kwa kuchunguza maudhui ya mazingira katika vipindi hivyo, kubainisha mbinu za mawasiliano zinazotumika na kuonesha namna washika dau wanavyoshirikishwa katika kuendeleza uhifadhi wa mazingira nchini Kenya.

Narura et al. (2024) katika utafiti The *Environmental Conservation Strategies Used in Secondary Schools Align with Guidelines of United Nations Environmental Program: Evidence from a Cross-Sectional Study in a City Setting*, wanaonesha kuwa elimu ya mazingira ni muhimu katika kujenga uelewa, mitazamo chanya na tabia endelevu miongoni mwa wanafunzi. Watafiti hao wanakubaliana na utafiti huu unaonesha kuwa elimu ya mazingira inaweza kuhamasisha vitendo kama upandaji miti, uhifadhi wa vyanzo vya maji na usimamizi bora wa taka. Hata hivyo, kuna tofauti katika mtazamo wa tafiti hizi. Narura et al. (2024) wanazingatia zaidi elimu rasmi ya mazingira shuleni, wakati utafiti huu unahusu vyombo vya habari vinavyotilia mkazo elimu inayotolewa kwa jamii kupitia maudhui ya televisheni. Utafiti huo umethibitisha kuwa, pamoja na kuwepo kwa mikakati ya elimu ya mazingira, bado kuna upungufu wa maarifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi na bioanuwai miongoni mwa wanafunzi. Aidha, changamoto za kiuchumi, ukosefu wa rasilimali na tofauti za kijamii hupunguza ufanisi wa elimu hiyo katika kuchochea mabadiliko ya tabia.

Kwa kuzingatia mchango wa utafiti huo, bado kuna pengo kuhusu nafasi ya vyombo vya habari katika kuwasilisha elimu ya mazingira kwa jamii pana nje ya mfumo rasmi wa shule. Utafiti wa

Narura et al. (2024) haujachunguza kwa kina namna maudhui ya televisheni yanavyowasilisha changamoto za mazingira, suluhisho zake na ujumbe wa uhifadhi. Pia, haujaeleza mikakati ya mawasiliano inayoweza kufanya ujumbe wa mazingira uwe rahisi kueleweka na kutekelezwa katika maisha ya kila siku. Utafiti huu unaziba pengo hilo kwa kuchunguza nafasi ya Runinga ya Citizen kupitia *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika kuwasilisha masuala ya uhifadhi wa mazingira. Hivyo, utafiti unaongeza maarifa kuhusu namna televisheni inavyoweza kutumika kama njia ya elimu ya mazingira kwa jamii pana.

Vyas et al (2024). *Impact of Shamba Shape-Up and iShamba on livestock and climate resilience*. *CGIAR Initiative on Livestock and Climate, Technical Report,* wanaonyesha umuhimu wa vyombo vya habari katika kutoa elimu kuhusu kilimo endelevu na uhifadhi wa mazingira. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa nafasi ya Runinga ya Citizen katika uhifadhi wa mazingira nchini Kenya kwa kuonyesha kuwa vipindi vya televisheni vinaweza kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya mbinu zinazolinda mazingira. Tafiti zote zinagusa masuala kama uhifadhi wa udongo, kilimo endelevu, matumizi bora ya pembejeo na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Pia, zote zinatambua umuhimu wa kutumia mawasiliano ya vitendo katika kuwasilisha ujumbe wa mazingira. Hata hivyo, zinatofautiana katika mkazo wa uchunguzi. Vyas et al. (2024) walijikita zaidi katika athari za *Shamba Shape-Up* na iShamba kwa uelewa na matumizi ya mbinu za kilimo miongoni mwa wakulima. Utafiti huu, kwa upande mwingine, unachunguza masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet***,** changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumika kuwasilisha ujumbe huo**.** Kwa hivyo, tafiti zote zinathibitisha kwamba televisheni inaweza kuwa chombo muhimu cha elimu na uhamasishaji wa uhifadhi wa mazingira, ingawa Vyas et al. walisisitiza zaidi matokeo ya ushauri wa kilimo kwa wakulima.

Licha ya mchango wa Vyas et al. (2024), bado kuna pengo la utafiti kuhusu namna maudhui ya uhifadhi wa mazingira yanavyowasilishwa kupitia vipindi vya Runinga ya Citizen, hasa kwa kuzingatia *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa pamoja. Utafiti huo haujachunguza kwa kina aina za masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayojitokeza katika vipindi hivyo, changamoto za mazingira zinazowasilishwa, wala mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe kwa watazamaji. Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kwa kuchanganua maudhui ya uhifadhi wa mazingira, kubainisha changamoto za kimazingira zinazowasilishwa na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika vipindi hivyo**.** Kwa kufanya hivyo, utafiti huu unapanua uelewa

wa nafasi ya televisheni katika uhifadhi wa mazingira kutoka katika kutoa ushauri wa kilimo hadi katika kuwasilisha ujumbe mpana wa uhifadhi wa mazingira kwa jamii ya Kenya.

Olago et al. (2024), katika utafiti wao wa "*Nature-Based Solutions in the Savanna Belt of Africa* wanaonyesha umuhimu wa kutumia mbinu za asili katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa nafasi ya Runinga ya Citizen katika uhifadhi wa mazingira nchini Kenya kwa kubainisha umuhimu wa upandaji miti, urejeshaji wa malisho, uhifadhi wa maji, udhibiti wa mmomonyoko wa udongo na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Masuala haya yanaonekana pia katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kupitia ujumbe unaohamasisha matumizi endelevu ya ardhi na rasilimali za mazingira. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika mtazamo wa uchunguzi**.** Olago et al. (2024) wanajikita katika ufanisi wa suluhisho za asili katika kukabiliana na uharibifu wa ardhi, huku utafiti huu ukijikita katika namna masuala hayo ya uhifadhi yanavyowasilishwa kupitia televisheni. Aidha, utafiti huu unachunguza pia changamoto za kimazingira zinazoibuliwa katika vipindi hivyo na mikakati ya mawasiliano inayotumika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi**,** jambo ambalo halikuwa lengo kuu la Olago et al. (2024). Kwa hivyo, tafiti zote zinafikia hitimisho kwamba mbinu endelevu za uhifadhi zinaweza kusaidia kupunguza uharibifu wa mazingira, lakini utafiti huu unaangalia pia nafasi ya mawasiliano katika kufikisha maarifa hayo kwa jamii.

Utafiti wa Olago et al. (2024), bado kuna pengo kuhusu namna vyombo vya habari, hususan televisheni, vinavyowasilisha suluhisho za uhifadhi wa mazingira katika mazingira ya Kenya. Utafiti huo haujachunguza maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala haujabainisha kwa kina changamoto za mazingira zinazopewa uzito katika vipindi hivyo. Pia, haujachunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika kufanya ujumbe wa mazingira ueleweke. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika vipindi hivyo, kuchanganua changamoto za kimazingira zinazojitokeza na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi. Hivyo, utafiti huu unaongeza uelewa kuhusu jinsi televisheni inavyoweza kuwasilisha maarifa ya uhifadhi kwa njia ya maudhui ya vitendo na yanayohusishwa na changamoto halisi za mazingira nchini Kenya.

Xu, et al (2023), katika utafiti *"Eco-economic Methodology for Maasai Mara Conservation,"* wanaonyesha umuhimu wa kuunganisha masuala ya kiuchumi na kiikolojia katika uhifadhi wa mazingira ya Maasai Mara. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa nafasi ya Runinga ya Citizen katika uhifadhi wa mazingira nchini Kenya kwa kuonyesha umuhimu wa kulinda bioanuai, rasilimali za asili na mifumo ya ikolojia dhidi ya shughuli zinazoweza kusababisha uharibifu wa

mazingira. Masuala haya yanaendana na maudhui yanayojitokeza katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, hasa uhifadhi wa rasilimali za asili, mabadiliko ya tabianchi na matumizi endelevu ya mazingira. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika mtazamo na mbinu ya uchunguzi. Xu, et al (2023) wanatumia zaidi modeli za kiuchumi na kiikolojia kueleza uhusiano kati ya shughuli za binadamu, uchumi na uhifadhi wa Maasai Mara. Kwa upande mwingine, utafiti huu unachunguza namna masuala ya uhifadhi wa mazingira yanavyowasilishwa kupitia televisheni**,** changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe huo kwa watazamaji. Kwa hivyo, tafiti zote zinaafikiana kwamba uelewa wa changamoto za mazingira ni muhimu kwa uhifadhi endelevu, lakini utafiti huu unaweka mkazo zaidi katika mawasiliano ya mazingira kupitia televisheni**.**

Matokeo ya Xu, et al (2023), bado kuna pengo kuhusu namna televisheni inavyowasilisha masuala ya uhifadhi wa mazingira nchini Kenya**.** Utafiti wao haujachunguza maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala haujabainisha changamoto za kimazingira zinazotolewa katika vipindi hivyo. Pia, haujachunguza kwa kina mikakati ya mawasiliano inayotumika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi kwa watazamaji. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika vipindi hivyo, kuchanganua changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi**.** Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu nafasi ya televisheni kama njia ya kuwasilisha elimu ya mazingira na kuunganisha masuala ya uhifadhi na changamoto halisi zinazokabili jamii nchini Kenya.

Petersen, M., & Nüsser, M. (2022). *Using an unmanned aerial system to analyse environmental impacts of charcoal production on tropical savanna ecosystems in northwestern Kenya.* Environmental Monitoring and Assessment wanaonyesha umuhimu wa teknolojia katika kuimarisha uhifadhi wa wanyamapori na mazingira. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa nafasi ya Runinga ya Citizen katika uhifadhi wa mazingira nchini Kenya kwa kuonyesha umuhimu wa kutumia njia bunifu katika kukabiliana na changamoto za mazingira. Tafiti zote zinahusu juhudi za kulinda mazingira, wanyamapori na makazi yao, pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya mazingira. Hata hivyo, zinatofautiana katika njia ya kushughulikia uhifadhi**.**

Petersen, M., & Nüsser, M. (2022) wanajikita katika matumizi ya teknolojia ya UAV katika kufuatilia wanyamapori, uharibifu wa makazi na mabadiliko ya matumizi ya ardhi. Kwa upande mwingine, utafiti huu unachunguza masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet***,** changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya

mawasiliano inayotumika kuwasilisha ujumbe huo kwa watazamaji**.** Kwa hivyo, tafiti zote zinakubaliana kwamba mbinu bunifu zinaweza kusaidia katika kukabiliana na changamoto za mazingira, lakini zinatofautiana kwa kuwa Christie et al. wanasisitiza teknolojia ya ufuatiliaji, wakati utafiti huu unasisitiza mawasiliano ya mazingira kupitia televisheni.

Kwa kuzingatia mchango wa Petersen, M., & Nüsser, M. (2022) bado kuna pengo kuhusu namna televisheni inavyotumia mawasiliano kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Utafiti huo haujachunguza maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, changamoto za kimazingira zinazopewa uzito katika vipindi hivyo, wala mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi kwa watazamaji. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, kuchanganua changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika vipindi hivyo. Kwa kufanya hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu nafasi ya televisheni katika kutoa elimu ya mazingira kwa kutumia mawasiliano yanayorahisisha uelewa wa changamoto za mazingira na mbinu za kuzitatua.

Bashir, M. A., & Wanyonyi, E. (2024), katika utafiti "*Winning Space for Conservation: Growth of Wildlife Conservancies in Kenya,"* wanaonyesha umuhimu wa maeneo ya hifadhi katika kulinda bioanuai na kupunguza uharibifu wa mazingira nchini Kenya. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa nafasi ya Runinga ya Citizen katika uhifadhi wa mazingira kwa kuonyesha umuhimu wa kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi wa bioanuai, matumizi endelevu ya ardhi na kulinda makazi ya wanyamapori. Masuala haya yanaendana na maudhui yanayojitokeza katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, hasa uhifadhi wa mazingira, upandaji miti na matumizi endelevu ya rasilimali za asili. Tafiti zote zinaonyesha kuwa uhifadhi unakabiliwa na changamoto kama mabadiliko ya matumizi ya ardhi, upanuzi wa shughuli za kilimo na shinikizo la ongezeko la watu**.** Hata hivyo, zinatofautiana katika mtazamo wa uchunguzi. Bashir & Wanyonyi, E. (2024) wanajikita katika ukuaji wa hifadhi za jamii na changamoto zake, wakati utafiti huu unachunguza masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi kwa watazamaji**.**

Katika muktadha wa Bashir & Wanyonyi, E. (2024), bado kuna pengo kuhusu namna televisheni inavyowasilisha masuala ya uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Utafiti wao haujachunguza maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala haujabainisha kwa kina changamoto za kimazingira zinazowasilishwa katika vipindi hivyo na namna ujumbe wa uhifadhi unavyofikishwa

kwa watazamaji. Pia, haujachunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika uwasilishaji wa ujumbe huo. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira, kuchanganua changamoto za kimazingira na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika vipindi hivyo. Kwa hivyo, tafiti zote zinahitimisha kwamba uhifadhi wa mazingira ni muhimu kwa kulinda bioanuai na rasilimali za asili, lakini utafiti huu unaongeza uelewa kuhusu nafasi ya televisheni katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira kupitia maudhui na mikakati mbalimbali ya mawasiliano.

Western et al. (2024) zinaonyesha kwa pamoja umuhimu wa elimu, taarifa na matumizi ya mbinu endelevu katika kukabiliana na changamoto za mazingira**.** Utafiti wa Western et al. unaonyesha kuwa changamoto kama matumizi yasiyofaa ya ardhi na migogoro ya umiliki wa ardhi huathiri juhudi za uhifadhi. Kwa upande mwingine, Western et al. (2024) wanaonyesha kuwa kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa udongo, matumizi bora ya maji na mbegu zinazostahimili ukame vinaweza kupunguza uharibifu wa mazingira. Hoja hizi zinafanana na maudhui yanayojitokeza katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, hasa uhifadhi wa udongo na maji, kukabiliana na ukame na mabadiliko ya tabianchi, pamoja na matumizi endelevu ya rasilimali. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana na utafiti huu katika eneo la uchunguzi. Western et al. (2024) wamejikita katika hifadhi za wanyamapori na matumizi ya ardhi, huku utafiti huu umejikita katika matumizi ya kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi. Utafiti huu, kwa upande wake, unachunguza masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumika kuwasilisha ujumbe huo**.** Kwa hivyo, tafiti zote zinafikia hitimisho kwamba taarifa na elimu kuhusu mbinu endelevu ni muhimu katika kukabiliana na changamoto za mazingira, lakini hazijajikita katika kuchanganua namna ujumbe huo unavyowasilishwa kupitia vipindi vya televisheni.

Pamoja na mchango wa tafiti hizi, bado kuna pengo katika kuelewa namna Runinga ya Citizen inavyowasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira kwa watazamaji nchini Kenya**.** Tafiti hizo hazijachanganua kwa kina maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, aina za changamoto za kimazingira zinazopewa uzito katika vipindi hivyo, wala mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika vipindi hivyo, kuchanganua changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika uwasilishaji wa ujumbe. Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu nafasi ya televisheni katika kutoa elimu ya

mazingira kwa kutumia mbinu za mawasiliano zinazofanya ujumbe wa uhifadhi ueleweke na kuhusishwa na changamoto halisi zinazokabili jamii nchini Kenya.

Utafiti wa McPhearson et al (2023) unaojulikana kama *nature-based solutions for sustainable, resilient, and equitable cities* wanaonyesha umuhimu wa maeneo ya kijani katika kukuza uendelevu wa mazingira. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa nafasi ya Runinga ya Citizen katika uhifadhi wa mazingira nchini Kenya kwa kuonyesha umuhimu wa upandaji miti, uhifadhi wa maeneo ya kijani, kupunguza uchafuzi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi**.** Masuala haya yanaonekana pia katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kupitia ujumbe unaohamasisha utunzaji wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali. Tafiti zote zinaonyesha pia kuwa uharibifu wa mazingira unatokana na changamoto kama ukuaji wa miji, shinikizo la matumizi ya ardhi na uelewa mdogo wa masuala ya mazingira. Hata hivyo, zinatofautiana katika eneo la uchunguzi. McPhearson et al (2023) wamejikita katika umuhimu wa maeneo ya kijani mijini na changamoto za uendelevu wake, wakati utafiti huu unachunguza masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet***,** changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi**.** Hivyo, tafiti zote zinafikia hitimisho kwamba uelewa wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali ni muhimu katika kulinda mazingira, lakini utafiti huu unaangalia kwa kina namna ujumbe huo unavyowasilishwa kupitia televisheni.

Aidha, mchango wa McPhearson et al (2023), bado kuna pengo kuhusu namna televisheni inavyowasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira katika muktadha wa Kenya**.** Utafiti huo haujachunguza maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet,* wala haujabainisha kwa kina aina za changamoto za mazingira zinazowasilishwa katika vipindi hivyo. Pia, haujachunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayojitokeza katika vipindi hivyo, kuchanganua changamoto za kimazingira zinazowasilishwa na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika uwasilishaji wa ujumbe huo. Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu nafasi ya televisheni katika kutoa elimu ya mazingira.

Ouma et al. (2024), katika utafiti *Towards environmental sustainability: Further evidences from decarbonization projects in Kenya's Blue Economy*.wanaonyesha umuhimu wa kupunguza uzalishaji wa kaboni katika kulinda rasilimali za baharini na kuimarisha uendelevu wa mazingira. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa nafasi ya Runinga ya Citizen katika uhifadhi wa mazingira nchini Kenya kwa kuonyesha umuhimu wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa

mazingira, uharibifu wa mifumo ya ikolojia na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za asili. Masuala haya yanaendana na ujumbe wa mazingira unaojitokeza katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, hasa kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika eneo na mtazamo wa uchunguzi**.** Ouma et al. (2024) wamejikita katika uchumi wa buluu, kupunguza uzalishaji wa kaboni na uhifadhi wa mazingira ya baharini. Utafiti huu, kwa upande mwingine, unachunguza masuala mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet***,** changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi. Kwa hiyo, tafiti zote zinafikia hitimisho kwamba elimu na uelewa wa mazingira ni muhimu katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira, lakini Ouma et al. wanajikita katika uchumi wa buluu, wakati utafiti huu unachunguza nafasi ya televisheni katika mawasiliano ya uhifadhi.

Vilevile, mchango wa Ouma et al. (2024), bado kuna pengo kuhusu namna televisheni inavyowasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Utafiti huo haujachunguza maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala haujabainisha kwa kina aina za changamoto za mazingira zinazowasilishwa katika vipindi hivyo. Pia, haujachunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi kwa watazamaji. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayojitokeza katika vipindi hivyo, kuchanganua changamoto za kimazingira zinazowasilishwa na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika uwasilishaji wa ujumbe wa mazingira. Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu nafasi ya televisheni katika kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi kwa kutumia mawasiliano yanayorahisisha uelewa wa changamoto za mazingira na mbinu za kukabiliana nazo.

Mediae (2024), katika ripoti *Shamba Shape-Up Series 14: Knowledge, Attitude and Practice (KAP) Report),* inaonyesha mchango wa televisheni katika kuongeza maarifa kuhusu kilimo endelevu na uhifadhi wa mazingira. Utafiti huu unakubaliana moja kwa moja na utafiti wa nafasi ya Runinga ya Citizen katika uhifadhi wa mazingira nchini Kenya kwa kuonyesha kuwa *Shamba Shape-Up* huwasilisha masuala kama uhifadhi wa udongo, upandaji miti, matumizi bora ya mbegu na kilimo kinachozingatia mazingira**.** Tafiti zote zinaonyesha pia kuwa elimu-burudani ni njia muhimu ya kuwasilisha maarifa ya mazingira kwa lugha na mifano inayoeleweka kwa watazamaji. Hata hivyo, zinatofautiana katika mkazo wa uchunguzi. Mediae (2024) inajikita zaidi katika kupima maarifa, mitazamo na matendo ya watazamaji baada ya kutazama *Shamba Shape-Up*.

Utafiti huu, kwa upande mwingine, unajikita katika uchambuzi wa maudhui ya vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Unachunguza masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe huo. Kwa hivyo, tafiti zote zinaonesha kwamba *Shamba Shape-Up* ina mchango katika kutoa elimu ya mazingira na kuhamasisha matumizi ya mbinu endelevu, lakini utafiti huu unaangalia zaidi maudhui na namna ujumbe huo unavyowasilishwa.

Matokeo, ya Mediea (2024), yanaonesha bado kuna pengo katika kuchunguza kwa pamoja maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa mtazamo wa uhifadhi wa mazingira. Ripoti hiyo imejikita zaidi katika matokeo ya maarifa, mitazamo na matendo ya watazamaji wa *Shamba Shape-Up*. Haijachanganua kwa kina aina mbalimbali za masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto za kimazingira na mikakati ya mawasiliano inayotumika katika vipindi hivyo viwili. Hivyo, utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, kuchanganua changamoto za kimazingira zinazojitokeza na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Hivyo, utafiti huu unaongeza uelewa kuhusu namna Runinga ya Citizen inavyounda na kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira.

2.4 Mikakati ya kimawasiliano Inayotumika katika Vipindi Teule

Kaul et al (2020), katika utafiti wao kuhusu mawasiliano ya mazingira kwa vijana kupitia video na mahojiano katika kampeni ya *Earth Overshoot Day* kwenye *YouTube*, wanaonyesha umuhimu wa mahojiano, ushuhuda wa wahusika halisi na video katika kuwasilisha ujumbe wa mazingira**.** Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa nafasi ya Runinga ya Citizen katika uhifadhi wa mazingira nchini Kenya kwa kuonyesha kuwa matumizi ya wahusika halisi na maelezo yanayotokana na uzoefu wa moja kwa moja yanaweza kufanya ujumbe wa mazingira ueleweke kwa urahisi. Mkakati huu pia unaonekana katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kupitia mahojiano, ushuhuda, maelezo ya wataalamu na maonyesho ya vitendo kuhusu masuala kama uhifadhi wa maji, udongo, upandaji miti na matumizi endelevu ya rasilimali**.** Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika muktadha na eneo la uchunguzi. Kaul et al. (2020) walijikita katika mawasiliano ya mazingira kupitia YouTube na hadhira ya vijana, wakati utafiti huu unachunguza vipindi vya televisheni vinavyolenga hadhira pana nchini Kenya. Pia, utafiti huu hauchunguzi mahojiano pekee, bali unachanganua masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto za kimazingira na mikakati mbalimbali ya mawasiliano inayotumika katika vipindi hivyo. Kwa hivyo, tafiti zote zinakubaliana kwamba mawasiliano yanayotumia video na uzoefu wa wahusika

halisi yanaweza kuongeza uelewa wa masuala ya mazingira, lakini utafiti huu unaangalia matumizi ya mikakati hiyo katika muktadha wa televisheni nchini Kenya.

Pamoja na mchango wa Kaul et al. (2020), bado kuna pengo la utafiti kuhusu namna vipindi vya televisheni nchini Kenya vinavyotumia mawasiliano kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira**.** Utafiti wao haujachunguza *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala haujabainisha kwa kina masuala ya uhifadhi na changamoto za kimazingira zinazowasilishwa katika vipindi hivyo. Pia, haujachanganua kwa pamoja mikakati ya mawasiliano inayotumika katika uwasilishaji wa ujumbe wa mazingira. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, kuchanganua changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet***.** Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu namna Runinga ya Citizen inavyotumia mahojiano, ushuhuda wa wahusika, maonyesho ya vitendo, lugha rahisi na vielelezo vya kuona katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya.

Ademosu et al. (2026), katika utafiti "*Symbolic Representations of the Environment Using Texts and Visuals in Television Programs,"* wanaonyesha umuhimu wa picha, maandishi na alama za kimazingira katika kuwasilisha ujumbe wa mazingira kupitia televisheni. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini kenya kwa kuonyesha kuwa vielelezo vya kuona vinaweza kurahisisha uelewa wa masuala ya mazingira na kuongeza mvuto wa ujumbe. Mbinu hii inaonekana pia katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kupitia picha za mazingira, ardhi, maji, mimea na shughuli za binadamu. Vielelezo hivyo husaidia kuonyesha changamoto kama mmomonyoko wa udongo, ukataji wa miti, uhaba wa maji, uchafuzi na mabadiliko ya tabianchi, pamoja na mikakati ya kukabiliana nazo. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika upeo wa uchunguzi**.** Ademosu et al. (2026) walijikita katika matumizi ya maandishi, picha na alama kama mbinu za uwasilishaji wa ujumbe wa mazingira. Utafiti huu, kwa upande mwingine, unachunguza kwa upana zaidi masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto za kimazingira na mikakati ya mawasiliano inayotumika katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Kwa hivyo, tafiti zote zinaafikiana kwamba matumizi ya vielelezo vya kuona yanaweza kufanya ujumbe wa mazingira ueleweke na kukumbukwa kwa urahisi, lakini utafiti huu unaangalia vielelezo hivyo pamoja na mikakati mingine ya mawasiliano inayotumika katika vipindi husika.

Utafiti wa Ademosu et al. (2026), bado una pengo kuhusu namna vipindi vya Runinga ya Citizen vinavyotumia kwa pamoja picha, maandishi na mikakati mingine ya mawasiliano katika

kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya**.** Utafiti wao haukulenga *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala haujachanganua kwa kina changamoto za kimazingira zinazowasilishwa katika vipindi hivyo. Pia, haujaonyesha kwa kina jinsi vielelezo vya kuona vinavyounganishwa na mahojiano, usimulizi, lugha, maonyesho ya vitendo na elimu-burudani katika kufikisha ujumbe wa mazingira. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, kuchanganua changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika vipindi hivyo. Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu namna Runinga ya Citizen inavyotumia mchanganyiko wa picha, maandishi, mahojiano, maonyesho ya vitendo na usimulizi kufanya ujumbe wa uhifadhi wa mazingira ueleweke kwa wanajamii nchini Kenya.

Vaughan na Johns (2021), katika utafiti *"Beyond Frame Analysis: Environmental Video Messaging,"* wanaonyesha umuhimu wa video katika kuwasilisha ujumbe wa mazingira kwa kuchanganya picha, sauti, maandishi na simulizi. Utafiti huu unakubaliana na utafiti uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini kenya kwa kuonyesha kuwa video inaweza kurahisisha uelewa wa changamoto za mazingira na kuwasilisha njia za kukabiliana nazo. Mbinu kama matumizi ya picha halisi, mahojiano, ushuhuda wa wahusika na maelezo ya wataalamu zinaendana na mikakati inayoweza kubainika katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Mikakati hiyo husaidia kuwasilisha masuala kama uhifadhi wa maji na udongo, upandaji miti, kilimo endelevu na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika upeo wa uchunguzi. Vaughan na Jones (2021) walijikita katika ujumbe wa mazingira unaowasilishwa kupitia video kwa ujumla. Utafiti huu, kwa upande mwingine, unachunguza masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe huo. Kwa hivyo, tafiti zote zinafikia hitimisho kwamba video ni njia yenye uwezo wa kuwasilisha ujumbe wa mazingira kwa njia inayoeleweka na kuvutia, lakini utafiti huu unaweka mkazo katika matumizi ya video ndani ya vipindi maalumu vya televisheni nchini Kenya.

Kwa kuchunguza utafiti wa Vaughan na Jones (2021), bado kuna pengo kuhusu namna vipindi vya televisheni nchini Kenya vinavyotumia mikakati mbalimbali ya mawasiliano katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira**.** Utafiti wao haujachunguza *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala haujabainisha kwa kina masuala ya uhifadhi na changamoto za kimazingira zinazowasilishwa katika vipindi hivyo. Pia, haujachanganua jinsi picha, sauti, maandishi,

mahojiano, ushuhuda, usimulizi na maonyesho ya vitendo vinavyotumika kwa pamoja katika kufikisha ujumbe wa mazingira. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira, kuchanganua changamoto za kimazingira na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya runinga katika kuwasilisha elimu ya mazingira kwa kutumia mawasiliano ya kuona na kusikia pamoja na mifano halisi inayohusisha changamoto na suluhisho za uhifadhi wa mazingira nchini Kenya.

Hoppe et al. (2026), katika utafiti "*Climate Change on Television Reaches the Engaged but Misses Distant Audiences,"* wanaonyesha kuwa televisheni ni chombo muhimu cha kuwasilisha ujumbe wa mabadiliko ya tabianchi na kuongeza uelewa wa masuala ya mazingira. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira nchini Kenya kwa kuonyesha kuwa televisheni inaweza kufikisha ujumbe wa mazingira kwa hadhira kubwa. Tafiti zote zinatambua umuhimu wa mahojiano, simulizi, picha halisi, ushuhuda na mifano ya vitendo katika kurahisisha uelewa wa masuala ya mazingira. Mikakati hiyo inaonekana pia katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika kuwasilisha masuala kama mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa maji na udongo, upandaji miti na matumizi endelevu ya rasilimali**.** Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika upeo wa uchunguzi. Hoppe et al. (2026) wamejikita katika namna ujumbe wa mabadiliko ya tabianchi unavyowafikia watazamaji wenye viwango tofauti vya uelewa. Utafiti huu, kwa upande mwingine, unachunguza masuala mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe huo. Kwa hiyo, tafiti zote zinafikia hitimisho kwamba televisheni ina uwezo wa kutoa elimu ya mazingira, lakini utafiti huu unaangalia kwa upana zaidi maudhui ya uhifadhi, changamoto na namna ujumbe huo unavyowasilishwa.

Pamoja na mchango wa Hoppe et al. (2026), bado kuna pengo kuhusu namna vipindi maalumu vya Runinga ya Citizen vinavyowasilisha ujumbe mpana wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya**.** Utafiti huo umejikita zaidi katika mabadiliko ya tabianchi na ufikishaji wa ujumbe kwa hadhira, bila kuchanganua *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Pia, haujabainisha kwa kina aina za changamoto za kimazingira zinazowasilishwa katika vipindi hivyo wala mikakati mbalimbali ya mawasiliano inayotumika kuzifafanua na kuwasilisha suluhisho**.** Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, kuchanganua changamoto

za kimazingira na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet***.** Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu uchambuzi wa mawasiliano ya mazingira kwa kuonyesha namna mahojiano, simulizi, picha, lugha, maonyesho ya vitendo na elimu-burudani vinavyotumika kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira kwa jamii nchini Kenya.

Ademosu et al. (2026), katika utafiti "*Symbolic Representations of the Environment Using Texts and Visuals in Three Environmental Programs on Nigerian Television Stations,"* wanaonyesha umuhimu wa picha, maandishi na alama za kimazingira katika kuwasilisha ujumbe wa mazingira kupitia televisheni. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira nchini Kenya kwa kuonyesha kuwa vielelezo vya kuona husaidia watazamaji kuelewa changamoto za mazingira na umuhimu wa uhifadhi. Masuala kama uharibifu wa misitu, uchafuzi wa maji, ukame, upandaji miti, uhifadhi wa maji na mabadiliko ya tabianchi yanaweza pia kuhusishwa na maudhui yanayojitokeza katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika muktadha na upeo wa uchunguzi**.** Ademosu et al. (2026) walijikita katika matumizi ya maandishi, picha na alama katika vipindi vitatu vya mazingira nchini Nigeria. Utafiti huu, kwa upande mwingine, unachunguza masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe huo. Kwa hiyo, tafiti zote zinafikia hitimisho kwamba vielelezo vya kuona vinaweza kurahisisha uelewa wa ujumbe wa mazingira, lakini utafiti huu unapanua uchunguzi kwa kuangalia maudhui ya uhifadhi, changamoto na mikakati mbalimbali ya mawasiliano katika vipindi vya Runinga ya Citizen.

Licha na mchango wa Ademosu et al. (2026), bado kuna pengo kuhusu namna televisheni nchini Kenya inavyotumia mchanganyiko wa mikakati ya mawasiliano kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira**.** Utafiti wao haujachunguza *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala haujabainisha kwa kina changamoto za kimazingira zinazowasilishwa katika vipindi hivyo. Pia, ulijikita zaidi katika picha, maandishi na alama, bila kuchanganua kwa kina mikakati mingine ya mawasiliano kama mahojiano, usimulizi, maonyesho ya vitendo na matumizi ya lugha**.** Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa, kuchanganua changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet***.** Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu namna Runinga ya Citizen inavyotumia picha, maandishi, mahojiano, usimulizi na maonyesho ya vitendo katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya.

Tella (2024), katika utafiti "*The Use of Social Media in Communicating Environmental Governance: A Review of Two Social Media Platforms in South Africa and Kenya,"* anaonyesha umuhimu wa vyombo vya habari katika kuwasilisha ujumbe wa mazingira kwa jamii. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa uchambuzi wa mawasiliano ya Runinga ya uhifadhi wa mazingira nchini Kenya kwa kuonyesha kuwa matumizi ya video, picha, simulizi na mahojiano yanaweza kurahisisha uelewa wa changamoto za mazingira na kuongeza mvuto wa ujumbe. Mikakati hii pia inaonekana katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika kuwasilisha masuala kama uhifadhi wa maji na udongo, upandaji miti, uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi**.** Tafiti zote zinafikia hitimisho kwamba mawasiliano yenye kutumia maudhui ya kuona na simulizi yanaweza kuongeza uelewa wa jamii kuhusu mazingira. Hata hivyo, zinatofautiana katika aina ya chombo cha habari kinachochunguzwa**.** Tella (2024) amejikita katika mitandao ya kijamii, wakati utafiti huu unachunguza televisheni kupitia *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Aidha, utafiti huu hauchunguzi mawasiliano ya mazingira kwa ujumla pekee, bali unalenga kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto za kimazingira na mikakati ya mawasiliano inayotumika katika vipindi hivyo**.**

Pamoja na mchango wa Tella (2024), bado kuna pengo katika utafiti kuhusu namna televisheni nchini Kenya inavyowasilisha kwa kina ujumbe wa uhifadhi wa mazingira**.** Tella hakuchunguza *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala hakubainisha aina za masuala ya uhifadhi na changamoto za kimazingira zinazowasilishwa katika vipindi hivyo. Pia, hakuchanganua kwa kina namna mikakati kama mahojiano, picha, simulizi, lugha, maandishi na maonyesho ya vitendo inavyotumika katika kuwasilisha ujumbe wa mazingira kupitia televisheni. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kuchanganua maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa kuzingatia masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto zinazojitokeza na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe huo**.** Kwa hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya shamba shape na *Citizen Planet* ya Runinga ya Citizen kwa kuonyesha namna televisheni inavyoweza kutumia mikakati mbalimbali ya mawasiliano kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi nchini Kenya.

Ong'ong'a (2023), katika utafiti "*Caring for Water, Plastics, and Trees: Community Radio and Digital Media in Kenya's Environmental Movements,"* anaonyesha kuwa vyombo vya habari vina nafasi muhimu katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya kwa kubainisha kuwa mawasiliano ya

mazingira yanaweza kuongeza uelewa wa jamii kuhusu changamoto kama uchafuzi wa plastiki, ukataji miti na uharibifu wa vyanzo vya maji. Tafiti zote pia zinaonyesha umuhimu wa mahojiano, simulizi, picha, video na ushuhuda wa wahusika halisi katika kurahisisha ujumbe wa mazingira na kuufanya ueleweke kwa jamii. Hata hivyo, zinatofautiana katika aina ya vyombo vya habari na upeo wa maudhui yanayochunguzwa. Ong'ong'a (2023) alijikita katika redio za kijamii na vyombo vya habari vya kidijitali, wakati utafiti huu unachunguza televisheni kupitia *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Aidha, utafiti huu unajikita mahsusi katika masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto za kimazingira na mikakati ya mawasiliano inayojitokeza katika vipindi hivyo. Kwa hivyo, tafiti zote zinafikia hitimisho kwamba vyombo vya habari vinaweza kuwa nyenzo muhimu ya elimu ya mazingira, lakini utafiti huu unaangalia kwa kina namna televisheni inavyotekeleza jukumu hilo kupitia vipindi maalumu vya mazingira.

Matokeo ya mchango wa Ong'ong'a (2023), bado kuna pengo kuhusu namna Runinga ya Citizen inavyowasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira kupitia *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Utafiti huo haujachunguza vipindi hivi wala kubainisha kwa kina aina za masuala ya uhifadhi yanayowasilishwa na changamoto za kimazingira zinazojitokeza katika maudhui yake. Pia, haujachanganua kwa kina mchanganyiko wa mikakati ya mawasiliano inayotumika katika televisheni, kama mahojiano, simulizi, picha, lugha, maandishi na maonyesho ya vitendo. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kuchanganua maudhui ya vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa kuzingatia masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto zinazowasilishwa na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe huo. Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya kwa kuonyesha si tu nini kinachowasilishwa kuhusu uhifadhi, bali pia changamoto zipi zinaibuliwa na jinsi ujumbe wa kukabiliana nazo unavyowasilishwa.

Cohn et al. (2023), katika utafiti "*Carrier Bag Storytelling with Coastal Kenyan Families: Sharing Food, Illustrations, and Knowledge for Tangible Environmental Justice Impacts,"* wanaonyesha kuwa simulizi, vielelezo na uzoefu wa maisha ya kila siku vinaweza kurahisisha uelewa wa ujumbe wa mazingira. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi teule vya Runinga ya Citizen nchini Kenya, kwa kuonyesha kuwa ujumbe unaohusishwa na maisha halisi ya jamii huwa rahisi kueleweka na unaweza kuhamasisha uelewa kuhusu uhifadhi wa mazingira. Mtazamo huu unaonekana pia katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, ambako changamoto za mazingira zinaweza kuwasilishwa kupitia

simulizi, picha, ushuhuda na mifano ya vitendo. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika chombo na eneo la mawasiliano. Cohn et al. (2023) walijikita katika simulizi na vielelezo katika jamii za pwani ya Kenya, wakati utafiti huu unachunguza mawasiliano ya mazingira kupitia vipindi vya televisheni vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Aidha, utafiti huu unakwenda zaidi ya kuchunguza simulizi pekee kwa kuangalia masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto za kimazingira na mikakati mbalimbali ya mawasiliano inayotumika katika vipindi hivyo. Kwa hivyo, tafiti zote zinaonyesha kuwa ujumbe unaounganishwa na uzoefu halisi unaweza kuongeza uelewa wa mazingira, lakini utafiti huu unachunguza namna kanuni hiyo inavyotekelezwa kupitia televisheni.

Pamoja na mchango wa Cohn et al. (2023), bado kuna pengo kuhusu namna vipindi vya Runinga ya Citizen vinavyotumia mikakati ya mawasiliano kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya**.** Utafiti wao haukuchunguza *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala haukubainisha kwa kina masuala ya uhifadhi na changamoto za kimazingira zinazowasilishwa katika vipindi vya televisheni. Pia, haukuchanganua mchanganyiko wa mikakati kama mahojiano, simulizi, picha, lugha, maandishi na maonyesho ya vitendo katika mawasiliano ya mazingira. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kuchanganua maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa kuzingatia masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto zinazojitokeza na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe huo. Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira ya Runinga ya Citizen kwa kuonyesha nini kinachowasilishwa kuhusu uhifadhi, changamoto zipi zinaibuliwa na ni kwa namna gani ujumbe wa kukabiliana na changamoto hizo unawasilishwa kwa watazamaji.

Mutoro et al. (2026), katika utafiti "*Effectiveness of Using Different Presentation Methods on Cheetah Conservation Awareness and Education in Kenya,"* wanaonyesha kuwa video, picha, mahojiano, simulizi na vielelezo vya kuona vinaweza kuongeza uelewa wa jamii kuhusu uhifadhi. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* ya Runinga ya Citizen nchini Kenya kwa kuonyesha kuwa matumizi ya mikakati mseto ya mawasiliano hurahisisha uelewa wa ujumbe wa mazingira. Mfanano huu unaonekana katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, ambavyo hutumia picha halisi, mahojiano, simulizi na maonyesho ya vitendo kuwasilisha masuala ya kilimo endelevu na uhifadhi wa mazingira. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika eneo la maudhui na upeo wa uchunguzi**.** Mutoro et al. (2026) walijikita katika uhamasishaji kuhusu uhifadhi wa duma, wakati utafiti huu unachunguza kwa upana masuala ya uhifadhi wa mazingira

yanayowasilishwa katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, changamoto zinazojitokeza na mikakati ya mawasiliano inayotumika kuwasilisha ujumbe huo. Kwa hiyo, tafiti zote zinafikia hitimisho kwamba mbinu mseto za mawasiliano zinaweza kuongeza uelewa wa ujumbe wa uhifadhi, lakini utafiti huu unaangalia matumizi ya mikakati hiyo katika maudhui mapana ya mazingira.

Aidha, mchango wa Mutoro et al. (2026), bado kuna pengo kuhusu namna vipindi vya televisheni nchini Kenya vinavyotumia mikakati mseto kuwasilisha masuala mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira. Utafiti huo haukuchunguza *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala haukubainisha kwa kina changamoto za mazingira kama vile mmomonyoko wa udongo, ukame na uhaba wa maji, kupungua kwa rutuba ya udongo, ukataji wa miti, upotevu wa bioanuai na mabadiliko ya tabianchi zinazoweza kuwasilishwa katika vipindi hivyo. Pia, haukuchanganua kwa kina jinsi mahojiano, picha, simulizi, lugha na maonyesho ya vitendo vinavyounganishwa katika kuwasilisha ujumbe wa mazingira. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kuchanganua maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa kuzingatia masuala ya uhifadhi, changamoto za kimazingira na mikakati ya mawasiliano inayotumika. Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira kwa kuonyesha masuala yanayowasilishwa, changamoto zinazoibuliwa na namna ujumbe wa uhifadhi unavyowasilishwa kwa watazamaji nchini Kenya.

Monyenye et al (2023), katika utafiti "*Analysis of Citizen Television's Framing of GMO-Related Stories for Public Awareness in Kenya,"* wanaonyesha kuwa Runinga ya Citizen hutumia mahojiano, picha, video, simulizi na maelezo ya wataalamu katika kuwasilisha taarifa zinazohusu GMO. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira kwa kuonyesha kuwa namna ujumbe unavyowasilishwa huathiri uelewa wa watazamaji kuhusu masuala ya kilimo na mazingira. Mikakati hiyo ya mawasiliano pia inajitokeza katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, ambavyo hutumia maudhui ya kuona, mahojiano, simulizi na maonyesho ya vitendo katika kufikisha ujumbe wa mazingira. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana katika aina ya maudhui yanayochunguzwa**.** Monyenye et al. (2023) walijikita katika uwasilishaji wa habari za GMO, wakati utafiti huu unachunguza masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto za kimazingira na mikakati ya mawasiliano katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Kwa hiyo, tafiti zote zinafikia hitimisho kwamba namna ujumbe wa televisheni unavyowasilishwa ni muhimu katika kuongeza uelewa wa jamii, lakini utafiti huu unapanua mjadala kutoka habari za GMO hadi maudhui mapana ya uhifadhi wa mazingira.

Pamoja na mchango wa Monyenye et al. (2023), bado kuna pengo la utafiti kuhusu maudhui ya vipindi vya mazingira vya Runinga ya Citizen**.** Utafiti wao haukuchunguza *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala haukubainisha kwa kina masuala ya uhifadhi yanayowasilishwa na changamoto za mazingira zinazoibuliwa katika vipindi hivyo**.** Pia, haukuchanganua kwa kina matumizi ya mikakati ya mawasiliano katika vipindi vya elimu na burudani vinavyolenga mazingira. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kuchanganua masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet***,** changamoto zinazojitokeza na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe huo. Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kwa kuonyesha namna mahojiano, picha, video, simulizi, lugha na maonyesho ya vitendo vinavyotumika katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira kupitia Runinga ya Citizen nchini Kenya.

Kitula na Ubaga (2026), katika utafiti "*Social Media as a Mechanism for Communicating Climate Change and Sustainability to the Youth in Kenya,"* wanaonyesha kuwa vyombo vya habari vinaweza kuongeza uelewa wa jamii kuhusu mabadiliko ya tabianchi na maendeleo endelevu. Utafiti huu unakubaliana na utafiti wa uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya kwa kubainisha umuhimu wa video, picha, simulizi, mahojiano, muziki na ujumbe mfupi katika kurahisisha mawasiliano ya mazingira. Mikakati hii ina uhusiano na namna *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* zinavyoweza kutumia maudhui ya kuona na mifano halisi kuwasilisha masuala ya uhifadhi wa udongo na maji, upandaji miti, mabadiliko ya tabianchi na matumizi endelevu ya rasilimali**.** Tafiti zote zinafikia hitimisho kwamba mawasiliano yanapotumia mbinu zinazovutia na zinazoeleweka kwa hadhira huongeza uelewa wa masuala ya mazingira. Hata hivyo, zinatofautiana katika chombo cha habari na eneo la uchunguzi. Kitula na Ubaga (2026) walijikita katika mitandao ya kijamii na vijana, wakati utafiti huu unachunguza vipindi vya televisheni vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa kuzingatia masuala ya uhifadhi, changamoto za kimazingira na mikakati ya mawasiliano inayotumika katika vipindi hivyo.

Kwa kuzingatia mchango wa Kitula na Ubaga (2026), bado kuna pengo kuhusu namna vipindi vya televisheni vya Citizen vinavyowasilisha kwa kina ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Utafiti wao haukuchunguza *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, wala haukubainisha kwa kina masuala ya uhifadhi na changamoto za kimazingira zinazowasilishwa katika vipindi hivyo. Pia, ulijikita katika mawasiliano ya kidijitali kwa vijana, hivyo haukuchanganua kwa kina mikakati ya mawasiliano inayotumika katika vipindi vya televisheni vinavyolenga hadhira pana. Utafiti huu

unajaza pengo hilo kwa kuchanganua maudhui ya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa kuzingatia masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto zinazojitokeza na mikakati ya mawasiliano inayotumika kufikisha ujumbe huo. Hivyo, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira kwa kuonyesha jinsi mahojiano, simulizi, picha, lugha, muziki, maandishi na maonyesho ya vitendo vinavyoweza kutumika katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya.

Utafiti wa Wefwafwa (2025), *TV Portrayal and People's Perceptions on Indigenous Environmental Conservation in Kenya*, unachunguza namna televisheni inavyowasilisha uhifadhi wa mazingira ya asili na maarifa ya kienyeji nchini Kenya. Utafiti huo unaonesha kuwa televisheni hutumia video, picha, mahojiano na simulizi katika kuwasilisha ujumbe wa mazingira, na kwamba uwasilishaji wa mila, desturi na mbinu za jadi za uhifadhi unaweza kuongeza uelewa na kuthaminiwa kwa maarifa ya asili. Matokeo haya yanaendana na utafiti huu kwa kuthibitisha kuwa televisheni ni chombo muhimu cha mawasiliano katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira. Aidha, tafiti zote zinatambua umuhimu wa kutumia mbinu shirikishi na za kuona, kama vile mahojiano, picha, video, simulizi na maonesho ya vitendo, katika kufanya ujumbe wa mazingira ueleweke kwa urahisi na kuvutia watazamaji. Hata hivyo, utafiti wa Wefwafwa unatofautiana na utafiti huu katika eneo la mkazo**.** Wefwafwa alijikita katika uwasilishaji wa uhifadhi wa mazingira ya asili na maarifa ya kienyeji kupitia televisheni, ilhali utafiti huu unalenga uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya**.**

Kwa kuzingatia mada hiyo, utafiti huu unapanua mjadala kwa kuchanganua si tu masuala ya mazingira yanayowasilishwa, bali pia namna ujumbe wa uhifadhi unavyoundwa na kuwasilishwa kwa watazamaji**.** Utafiti unazingatia maudhui kama vile uhifadhi wa udongo na maji, upandaji na uhifadhi wa miti, kilimo endelevu, mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa bioanuai na uchafuzi wa mazingira, pamoja na changamoto zinazohusiana na masuala hayo. Aidha, unachunguza mikakati ya mawasiliano inayotumiwa katika vipindi hivyo, ikiwamo mahojiano, maonesho ya vitendo, picha na video, simulizi, matumizi ya mifano halisi na elimu-burudani**,** katika kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Hivyo, pengo linalojitokeza katika utafiti wa Wefwafwa ni kutokuchanganua kwa kina namna vipindi maalumu vya televisheni vinavyotumia mikakati hiyo katika kuwasilisha mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira. Utafiti huu unalenga kuziba pengo hilo kwa kuchanganua maudhui ya uhifadhi wa mazingira, changamoto za kimazingira na mikakati ya mawasiliano inayojitokeza katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, na hivyo kuongeza

maarifa kuhusu nafasi ya runinga katika kuwasilisha elimu na ujumbe wa uhifadhi wa mazingira nchini Kenya.

2.5 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhakiki Ikolojia**,** ambayo ilianza kujengeka katika miaka ya 1970 na kuhusishwa na William Rueckert, aliyelitumia neno "*ecocriticism"* mwaka 1978 katika kazi yake kuhusu fasihi na ikolojia. Baadaye, nadharia hii iliendelezwa na wataalamu mbalimbali, wakiwamo Cheryll Glotfelty na Harold Fromm, ambao walichangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha na kueneza mkabala huo kupitia kitabu *The Ecocriticism Reader: Landmarks in Literary Ecology* (Glotfelty & Fromm, 1996). Kimsingi, nadharia hii hujikita katika kuchunguza uhusiano na utegemeano uliopo kati ya binadamu, mazingira na mifumo ya mawasiliano katika jamii. Katika utafiti huu, Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia ilitumika kuchambua mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya. Nadharia hii ilichaguliwa kwa sababu ina mihimili inayowezesha uchambuzi wa masuala ya uharibifu wa mazingira, athari zake kwa jamii, pamoja na juhudi za utetezi na uhifadhi wa mazingira kupitia vyombo vya habari. Aidha, nadharia hii ilimsaidia mtafiti kuchunguza jinsi vipindi hivyo vinavyotoa elimu, kuhamasisha jamii kuhusu matumizi bora ya rasilimali za mazingira, na kuchochea mabadiliko ya tabia zinazolenga kulinda mazingira kwa maendeleo endelevu.

2.5.1 Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia

Hatua muhimu zaidi katika kuimarika kwa Uhakiki-Ikolojia ilitokea mwaka 1996, wakati Cheryll Glotfelty na Harold Fromm walipochapisha kitabu *The Ecocriticism Reader*: *Landmarks in Literary Ecology*. Kitabu hicho kilitoa msingi muhimu wa kinadharia na kimetodolojia kwa tafiti za Uhakiki-Ikolojia na kusaidia kueneza mkabala huo katika taaluma mbalimbali. Baada ya hapo, nadharia hiyo iliendelea kupanuka kutoka katika uchambuzi wa fasihi na kujumuisha mawasiliano, vyombo vya habari, utamaduni, siasa, elimu na masuala ya mazingira**.** Wasomi kama Lawrence Buell, William Howarth, Joseph Meeker, Christopher Manes, Neil Evernden, Scott Slovic, Simon Estok na Ursula Heise walitoa mchango mkubwa katika kuendeleza mitazamo mbalimbali ya Uhakiki-Ikolojia. Kwa ujumla, historia ya nadharia hii inaonesha mabadiliko kutoka katika kuchunguza uwakilishi wa mazingira katika fasihi hadi kuchanganua kwa upana namna mawasiliano na vyombo vya habari vinavyounda mitazamo, uelewa na mahusiano ya jamii na mazingira**.** Mtazamo huu unaifanya nadharia hiyo kuwa mwafaka kwa utafiti huu

unaochanganua mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya.

Kimsingi, Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia huchunguza uhusiano uliopo kati ya binadamu, mazingira na mifumo ya mawasiliano katika jamii. Nadharia hii huangalia namna mazingira yanavyowasilishwa, kuthaminiwa au kuharibiwa kupitia vyombo mbalimbali vya mawasiliano pamoja na namna jamii inavyoathiriwa kuhusu masuala ya mazingira. Ingawa hapo awali nadharia hii ilitumika zaidi katika uchambuzi wa kazi za kifasihi, katika utafiti huu, ilitumika kuchunguza mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya, Kupitia vipindi hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira, matumizi bora ya rasilimali za asili, kilimo endelevu, uhifadhi wa maji, upandaji miti na njia za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, nadharia hii inasisitiza kuwa utamaduni wa binadamu na mazingira huhusiana na kuathiriana. Kwa msingi huo, vyombo vya habari vina mchango muhimu katika kujenga mitazamo na tabia za jamii kuhusu mazingira. Kupitia maudhui yanayopeperushwa katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet,* jamii hupata maarifa yanayoweza kubadili tabia zinazochangia uharibifu wa mazingira na kuhamasishwa kushiriki katika shughuli za uhifadhi wa mazingira. Vilevile, nadharia hii husaidia kuchunguza jinsi vyombo vya habari vinavyoweza kuibua mjadala wa kimazingira, kuhamasisha uwajibikaji wa pamoja, na kuendeleza utamaduni wa kulinda mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Hivyo, Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia ni mwafaka katika utafiti huu kwa sababu iliwezesha uchambuzi wa mchango wa vyombo vya habari katika kuelimisha, kuhamasisha na kuleta mabadiliko ya kijamii kuhusu uhifadhi wa mazingira.

2.5.2 Mihimili ya Nadharia

Mihimili ya Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia ni misingi inayotumika kuchunguza uhusiano kati ya fasihi, binadamu na mazingira. Nadharia hii huangalia jinsi mazingira yanavyowasilishwa katika kazi za kifasihi na namna shughuli za binadamu zinavyoathiri mazingira. Mihimili yake mikuu ni pamoja na:

1. **Uhusiano kati ya binadamu na mazingira:** Huhimiza kuelewa kuwa binadamu ni sehemu ya mazingira, si mtawala wake. Fasihi huonyesha jinsi maisha ya watu yanavyotegemea mazingira.

2. **Uhifadhi wa mazingira:** Nadharia hii inasisitiza umuhimu wa kulinda mazingira dhidi ya uharibifu kama vile ukataji miti, uchafuzi wa mazingira na matumizi mabaya ya rasilimali.

3. **Ukosoaji wa uharibifu wa mazingira:** Huikosoa jamii au mifumo inayochangia uharibifu wa mazingira kupitia maendeleo yasiyo endelevu, viwanda au tamaa ya kiuchumi.

4. **Uwakilishi wa mazingira katika fasihi:** Huchunguza jinsi mazingira kama mito, misitu, wanyama, na hali ya hewa yanavyoelezwa katika kazi za fasihi na umuhimu wake katika kuendeleza maudhui.

5. **Maadili ya kimazingira:** Hukuza maadili ya kuheshimu viumbe vyote na kutumia rasilimali kwa njia endelevu ili vizazi vijavyo vinufaike.

6. **Athari za shughuli za binadamu kwa ikolojia:** Huchunguza matokeo ya shughuli za kibinadamu kama ukulima kupita kiasi, uchimbaji madini na mchakato wa kuongezeka kwa miji kwa mfumo wa ikolojia.

7. **Uendelevu:** Huhimiza matumizi ya rasilimali kwa namna inayokidhi mahitaji ya sasa bila kuharibu uwezo wa vizazi vijavyo kukidhi mahitaji yao.

2.5.3 Uhusiano wa Nadharia ya Uhakiki-ikolojia na Utafiti Huu

1. Uhusiano na utegemeano kati ya binadamu na mazingira: Mhimili huu unaangalia namna maisha na shughuli za binadamu zinavyohusiana na kutegemea mazingira, pamoja na namna mabadiliko katika mazingira yanavyoathiri maisha ya jamii. Katika utafiti huu, mhimili ulisaidia kuchanganua jinsi *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* zinavyowasilisha utegemeano wa jamii na ardhi, maji, misitu, bioanuwai na rasilimali nyingine za asili. Mhimili huu unahusiana moja kwa moja na lengo la kwanza, linalohusu kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika vipindi hivyo, kwa sababu uliwezesha kutambua na kufafanua namna vipindi vinavyowasilisha matumizi na uhifadhi wa rasilimali za mazingira kwa ajili ya ustawi wa jamii.

2. Uharibifu wa mazingira, sababu na athari zake: Mhimili huu unachunguza namna shughuli za binadamu na sababu nyingine zinavyochangia mabadiliko na uharibifu wa mazingira, pamoja

na athari zake kwa binadamu na mifumo ikolojia. Katika utafiti huu, mhimili ulisaidia kuchanganua namna vipindi vinavyowasilisha changamoto kama ukataji miti, uchafuzi wa mazingira, mmomonyoko wa udongo, ukame, kupungua kwa rutuba ya udongo, upotevu wa bioanuwai na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo, mhimili huu unahusiana moja kwa moja na lengo la pili la utafiti, ambalo ni kuchanganua changamoto za kimazingira zinazoibuliwa katika vipindi. Pia uliwezesha kutathmini uhusiano kati ya vitendo vya binadamu, athari za kimazingira na madhara yanayoyapata jamii.

3. Uhifadhi, uendelevu na wajibu wa binadamu kwa mazingira: Mhimili huu unasisitiza umuhimu wa kuchunguza namna matini au mawasiliano yanavyohamasisha ulinzi wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za asili. Katika utafiti huu, mhimili ulisaidia kuchanganua suluhisho na hatua za uhifadhi zinazowasilishwa katika vipindi, kama vile upandaji miti, uhifadhi wa maji na udongo, kilimo hifadhi, agroforestry, uhifadhi wa bioanuwai, usimamizi wa taka na matumizi ya nishati endelevu. Mhimili huu unahusiana na lengo la kwanza kwa kubainisha masuala ya uhifadhi yanayowasilishwa na pia unachangia katika lengo la tatu, kwa kuwa mikakati ya kuwasilisha na kuhamasisha hatua za uhifadhi ni sehemu ya mawasiliano yanayochunguzwa katika utafiti.

4. Uwakilishi na ujenzi wa ujumbe wa kimazingira: Mhimili huu unachunguza namna mazingira, matatizo ya mazingira, binadamu na suluhisho za uhifadhi zinavyowakilishwa na kujengwa kupitia mawasiliano. Katika utafiti huu, mhimili ulisaidia kuchanganua namna vipindi vinavyotumia lugha, maelezo, picha, vielelezo, simulizi, mahojiano, ushuhuda wa jamii na maonesho ya vitendo kujenga na kufikisha ujumbe kuhusu mazingira. Mhimili huu unahusiana kwa karibu na lengo la tatu, linalohusu kuchunguza mikakati ya kimawasiliano inayotumiwa katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Kwa msingi huo, uliwezesha utafiti kwenda zaidi ya kubainisha *kile kinachosemwa* na kuchunguza pia *namna* ujumbe huo unavyowasilishwa.

5. Uhusiano kati ya utamaduni, jamii na mazingira: Mhimili huu unatambua kwamba uhusiano wa binadamu na mazingira huathiriwa pia na maarifa, mila, desturi, uzoefu na shughuli za kijamii na kiuchumi. Katika utafiti huu, mhimili ulisaidia kuchanganua namna vipindi vinavyohusisha uzoefu wa jamii na maarifa ya kimazingira katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi. Kwa mfano, matumizi ya ushuhuda wa wanajamii na maonesho ya vitendo huunganisha maarifa ya kitaalamu na uzoefu wa kila siku wa jamii. Mhimili huu unachangia zaidi lengo la tatu, kwa kuwa unaonesha

namna ushiriki wa jamii na uzoefu wao unavyotumiwa kama sehemu ya mkakati wa mawasiliano ya mazingira.

Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia inafaa katika utafiti huu kwa kuwa inatoa msingi wa kuchanganua namna mawasiliano ya televisheni yanavyowasilisha uhusiano kati ya binadamu na mazingira. Kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu, nadharia hii inasaidia kuchanganua masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*. Pia, inasaidia kuchunguza changamoto za kimazingira zinazoibuliwa katika vipindi hivyo na namna zinavyohusishwa na shughuli za binadamu na matumizi ya rasilimali za asili. Aidha, nadharia hii inatoa msingi wa kuchanganua mikakati ya mawasiliano inayotumiwa na vipindi hivyo katika kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Hivyo, Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia inauwezesha utafiti huu kutathmini namna *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* zinavyotumia mawasiliano ya televisheni kuelimisha, kujenga uelewa na kuhamasisha mitazamo inayounga mkono uhifadhi na matumizi endelevu ya mazingira nchini Kenya**.**

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Kothari (2004) anatoa wazo la ufafanuzi wa mbinu za utafiti kuwa ni njia zote zinazotumiwa na watafiti katika kufanya utafiti wao. Kitabu hiki cha mbinu za utafiti, kina mbinu za utafiti nilizotumia ili kufikia malengo ya utafiti huu. Sura hii iliangazia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli na usampulishaji. Pia, iliangazia mbinu nilizotumia kukusanya data, vipengele vya uchanganuzi wa data na maadili ya utafiti.

3.2 Muundo wa Utafiti

Muundo uliotumika kufanya utafiti huu ni wa kithamano wenye mwelekeo wa uchambuzi wa maudhui. Kothari (2004) anaeleza kuwa muundo wa utafiti ni mfumo wa jumla unaoelekeza jinsi utafiti unavyopaswa kufanywa ili kupata majibu ya maswali ya utafiti. Utafiti wa kimaelezo katika mkabala wa kitaamuli hulenga kueleza, kufasiri na kuwasilisha maana ya matukio, maandiko au uzoefu wa kijamii kwa kutumia maelezo badala ya vipimo vya nambari. Muundo huu hunuia kufafanua maana ya jambo linalochunguzwa kwa kutoa maelezo ya kina na jinsi hali ilivyo. Muundo huu unaendana na tafsiri ya Ary et al. (2010) kuwa utafiti wa kitaamuli unasisitiza ufahamu wa maana zilizojificha na muktadha wa maudhui.

3.3 Eneo la Utafiti

Kwa mujibu wa Creswell (2009), Azorín na Cameron (2010) pamoja na McBride et al. (2019), eneo la utafiti ni muktadha au uwanda ambao mtafiti huuteua kwa ajili ya kukusanya na kuchanganua data kulingana na madhumuni ya utafiti. Kwa kuwa utafiti huu ni utafiti wa nyaraka unaotumia uchambuzi wa maudhui na haukuhusisha utafiti wa nyanjani, bali ulifanyika katika Runinga ya Citizen nchini Kenya na vipindi maalumu vilivyoteuliwa kuwa vyanzo vya data. Utafiti ulijikita katika uchambuzi wa maudhui ya vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vinavyohusiana na uhifadhi wa mazingira. Data ilipatikana kutoka katika vipindi vilivyorekodiwa na kuhifadhiwa katika kumbukumbu za Runinga ya Citizen, majukwaa yake ya kidijitali na vyanzo vingine rasmi vinavyohifadhi au kusambaza vipindi hivyo.

3.4 Kundi Lengwa

Kundi lengwa la utafiti huu lilijumuisha maudhui ya vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vilivyorushwa na Runinga ya Citizen, pamoja na nyaraka na machapisho yaliyohusiana na mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Kwa *Shamba Shape-Up*, utafiti uliteua kipindi cha miaka miwili, kuanzia Machi 2024 hadi Machi 2026**,** kwa sababu kipindi hicho kinatoa muda mpana wa kuchanganua mwendelezo wa mawasiliano ya mazingira katika misimu mbalimbali na kupunguza uwezekano wa matokeo kuakisi msimu mmoja pekee. Aidha, kipindi hicho kinajumuisha Series 14 ya mwaka 2024, Series 15 ya mwaka 2025 na Series 16 ya mwaka 2026, ambazo zina maudhui yanayohusiana na udongo, maji, miti, kilimo endelevu na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Series 14, kwa mfano, ilirushwa kuanzia Machi hadi Septemba 2024, huku kumbukumbu za Mediae zikithibitisha kuwa *Series* 15 ilikuwa msimu wa mwaka 2025 na Series 16 mwaka wa 2026. Kwa kuwa *Shamba Shape-Up* hurushwa mara mbili kwa wiki, Jumamosi na Jumapili, kwa lugha mbili, matangazo yanakuwa takribani 208 katika miaka miwili ikiwa kila wiki ilitumika kikamilifu (52 × 2 × 2); hata hivyo, matangazo ya Jumamosi na Jumapili yanawakilisha kipindi kimoja katika kila wiki, hivyo idadi ya vipindi tofauti ni ndogo kuliko idadi ya matangazo.

Kundi lengwa la utafiti huu lilijumuisha maudhui ya vipindi vya Runinga ya Citizen, hususan vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, pamoja na nyaraka, ripoti, na tafiti mbalimbali zinazohusiana na mawasiliano ya mazingira na uhifadhi wa mazingira nchini Kenya.

3.5 Uteuzi wa Sampuli na Usampulishaji

Utafiti huu ulitumia usampulishaji wa kimakusudi kwa sababu ulilenga kuchagua maudhui, ripoti na vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vinavyohusiana moja kwa moja na mada ya uhifadhi wa mazingira. Patton (2002) anaeleza kuwa usampulishaji wa kimakusudi unafaa katika tafiti za ubora ambazo hazihitaji uwakilishi wa idadi kubwa bali kina cha taarifa. Katika utafiti huu, vipindi 12 vya *Shamba Shape-Up* viliteuliwa kutoka katika miaka hiyo miwili kwa kutumia usampulishaji lengwa**.** Vipindi hivyo vilichaguliwa kwa sababu vilikuwa na maudhui yanayohusiana moja kwa moja na malengo ya utafiti, hususan uhifadhi wa udongo na maji, upandaji na uhifadhi wa miti, kilimo endelevu, mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa bioanuai na changamoto za kimazingira**,** pamoja na matumizi ya mikakati mbalimbali ya mawasiliano. Kwa upande wa *Citizen Planet*, utafiti ulijikita katika kipindi cha mwaka mmoja, kuanzia Machi 2025 hadi Februari 2026**,** kwa sababu uliwezesha kuchanganua maudhui ya hivi karibuni ya mazingira katika kipindi hicho na kulinganisha namna ujumbe wa uhifadhi ulivyowasilishwa katika kipindi tofauti na *Shamba Shape-Up*. Ndani ya mwaka huo, vipindi 12 vya *Citizen Planet* viliteuliwa kwa usampulishaji lengwa kwa kuzingatia vipindi vilivyokuwa na maudhui ya moja kwa moja kuhusu uhifadhi wa mazingira, changamoto za kimazingira na mikakati ya mawasiliano. Kwa hivyo, jumla ya vipindi 24 viliteuliwa vikiwa 12 vya *Shamba Shape-Up* na 12 vya *Citizen Planet*. Vipindi hivi vilitumika kama sampuli ya msingi ya uchambuzi**,** kwa kuwa idadi hiyo iliwezesha uchambuzi wa kina bila kulazimisha mtafiti kuchanganua kila kipindi kilichorushwa katika kipindi chote cha utafiti.

3.6 Mbinu za Kukusanya Data

Kwa kuwa utafiti huu ni wa kimaelezo unaotumia uchambuzi wa maudhui ya nyaraka na haukuhusisha ukusanyaji wa data moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa nyanjani, data zilikusanywa kutoka katika vyanzo vya maandishi, sauti na picha vinavyohusiana na vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen. Kwa mujibu wa Bowen (2009), uchambuzi wa nyaraka ni mbinu inayofaa katika utafiti unaotegemea data zilizopo kwa kuwa humwezesha mtafiti kuchunguza kwa utaratibu taarifa zilizohifadhiwa katika nyaraka mbalimbali.

3.7 Uchanganuzi wa Data

Kwa mujibu wa Braun na Clarke (2006), uchanganuzi wa kimaudhui huhusisha kutambua, kupanga, kuchanganua na kutafsiri mada na mifumo inayojitokeza katika data. Data za utafiti huu zilichanganuliwa kwa kutumia uchanganuzi wa kimaudhui**,** ambapo vipindi vilivyoteuliwa kwa

kimaksudi vilichanganuliwa kwa kuzingatia uhusiano wake na malengo ya utafiti. Uteuzi huu ulihusisha kuchagua vipindi 12 vya *Shamba Shape-Up* kutoka Machi 2024 hadi Februari 2026 na vipindi 12 vya *Citizen Planet* kutoka Machi 2025 hadi Juni 2026 vilivyokuwa na maudhui yanayohusiana moja kwa moja na uhifadhi wa mazingira. Katika utafiti huu, kila kipindi kilichoteuliwa kilitazamwa na kuchanganuliwa kwa kuzingatia mada na vipengele vilivyowekwa kulingana na malengo ya utafiti**.** Uchanganuzi ulilenga kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet,* kama vile uhifadhi wa udongo na maji, upandaji na uhifadhi wa miti, kilimo endelevu, uhifadhi wa bioanuai na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, data zilichanganuliwa ili kubainisha changamoto za kimazingira zinazoibuliwa katika vipindi hivyo, pamoja na sababu na madhara yanayohusishwa nazo. Vilevile, utafiti ulichanganua mikakati ya mawasiliano inayotumiwa kufikisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira, ikiwemo mahojiano, maonesho ya vitendo, picha na video, simulizi, matumizi ya mifano halisi, lugha na elimu-burudani. Baada ya uchanganuzi, taarifa ziliwekwa katika makundi na mada zinazolingana na malengo matatu ya utafiti**,** kisha kufasiriwa ili kubainisha namna Runinga ya Citizen inavyotumia vipindi hivi kuwasilisha mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Ili kuwezesha utambuzi, upangaji na ufuatiliaji wa data wakati wa uchanganuzi, mtafiti alitumia mfumo wa usimbaji wa data. Msimbo M-01-V-SSU umetumika kumaanisha Mtaalamu wa kwanza (M-01), Video (V), kutoka katika kipindi cha *Shamba Shape-Up* **(**SSU)**.** Namba inayofuata baada ya herufi M ilitumika kutofautisha wataalamu au vipengele vya data vilivyotambuliwa katika uchanganuzi. Mfumo huu uliwezesha mtafiti kutenganisha data kwa mujibu wa chanzo chake na kurahisisha ufuatiliaji wa ushahidi kutoka katika video hadi kwenye kategoria, maudhui na tafsiri ya data.

3.8 Vifaa vya Utafiti

Utafiti huu ulitumia vifaa mbalimbali vilivyowezesha ukusanyaji, uhifadhi na uchanganuzi wa data kutoka katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen. Kifaa kikuu kilikuwa ni kompyuta ambayo ilitumika kutazama na kuhifadhi kumbukumbu za vipindi, kutayarisha na kuhifadhi data, pamoja na kuandika na kuhariri taarifa za utafiti. Intaneti ilitumika kufikia kumbukumbu za vipindi, tovuti na majukwaa rasmi ya kidijitali ya Runinga ya Citizen, pamoja na machapisho ya kitaaluma, ripoti na nyaraka zinazohusiana na mawasiliano na uhifadhi wa mazingira. Kifaa cha kuhifadhia data, kama vile diski ya kuhifadhia taarifa au hifadhi ya kidijitali, kilitumika kutunza nakala za vipindi, madondoo na data zilizokusanywa. Vifaa hivi vilitumika kwa pamoja ili kuhakikisha kuwa data kutoka katika vipindi vilivyoteuliwa

zinakusanywa, zinahifadhiwa na kuchanganuliwa kwa utaratibu unaoendana na malengo ya utafiti.

3.9 Maadili ya Utafiti

Hata katika utafiti usiohusisha kazi ya nyanjani, masuala ya kimaadili ni muhimu katika kuhakikisha mchakato mzima wa utafiti unazingatia uadilifu, uwazi, uaminifu na uwajibikaji wa kitaaluma. Orb et al. (2001) wanasisitiza umuhimu wa kuzingatia maadili katika matumizi, uchambuzi na uwasilishaji wa taarifa kutoka vyanzo mbalimbali. Katika utafiti huu, mtafiti alihakikisha kuwa vipindi vya televisheni, nyaraka, machapisho ya kitaaluma na vyanzo vingine vilivyotumika vinatambuliwa na kunukuliwa ipasavyo kwa kuzingatia kanuni za uandishi wa kitaaluma na haki miliki. Aidha, mtafiti aliepuka wizi wa kazi za wengine, ughushi, upotoshaji na uchaguaji wa taarifa kwa upendeleo**,** na aliwasilisha matokeo kulingana na data zilizopatikana bila kuzibadilisha ili kuendana na matarajio ya utafiti. Kuzingatia misingi hii kunaendana na kaida na viwango vya uadilifu wa kitaaluma vya Chuo kikuu Kikatoliki cha Afrika Mashariki**,** vinavyohimiza uaminifu, uwajibikaji, heshima kwa haki miliki na uadilifu katika shughuli za kitaaluma na utafiti. Kwa hivyo, utekelezaji wa maadili haya uliwezesha utafiti kufanyika kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma, kulinda uaminifu wa data na matokeo, na kuheshimu haki za wamiliki wa nyaraka na maudhui yaliyotumika.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

4.0 Utangulizi

Sura hii iliwasilisha na kujadili matokeo ya utafiti kuhusu mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya. Uchambuzi umezingatia malengo ya utafiti yaliyolenga kubainisha masuala na changamoto za uhifadhi wa mazingira pamoja na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa kuwasilisha ujumbe huo. Data zilitokana na vipindi vilivyoteuliwa kwa uteuzi wa kimaksudi, pamoja na nyaraka na machapisho husika. Uwasilishaji na uchambuzi wa matokeo uliongozwa na Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia (Glotfelty & Fromm, 1996) na ulifanywa kwa kutumia misimbo, kategoria na mada zilizojitokeza katika uchanganuzi wa kimaudhui.

4.1 Masuala ya Uhifadhi wa Mazingira

Katika sehemu hii, mtafiti anawasilisha na kuchanganua data zilizopatikana kutoka katika vipindi teule vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa kuzingatia lengo la kwanza la utafiti, ambalo lililenga kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira yanayowasilishwa katika vipindi hivyo. Uchanganuzi ulifanywa kwa kutumia uchanganuzi wa kimaudhui, ambapo taarifa zilizopatikana katika vipindi ziliainishwa katika mada na kategoria zinazohusiana na uhifadhi wa mazingira. Miongoni mwa masuala yaliyobainika ni uhifadhi wa udongo, uhifadhi na matumizi endelevu ya maji, upandaji na uhifadhi wa miti, kilimo endelevu, uhifadhi wa bioanuai, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira. Katika kuendeleza uchanganuzi, mtafiti alizingatia namna vipindi hivi vinavyowasilisha uhusiano kati ya shughuli za binadamu na mazingira, pamoja na hatua zinazopendekezwa ili kupunguza uharibifu wa mazingira na kuimarisha matumizi endelevu ya rasilimali za asili. Uchanganuzi huu uliongozwa na Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia, inayosisitiza umuhimu wa kuchunguza uhusiano kati ya

binadamu na mazingira na kupinga mitazamo na matendo yanayochangia uharibifu wa mazingira.

UNESCO (2021) inaonesha kuwa vyombo vya habari, hususan televisheni, vina nafasi muhimu katika kuwasilisha taarifa, kutoa elimu na kuongeza uelewa wa jamii kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya mazingira**.** Mtazamo huu unaakisiwa katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*, ambavyo huwasilisha masuala mbalimbali ya mazingira kwa kutumia mifano halisi, maelezo ya wataalamu, mahojiano na maonesho ya vitendo. Katika utafiti huu, vipindi hivyo vilibainika kuwasilisha masuala kama uhifadhi wa maji na udongo, upandaji na uhifadhi wa miti, kilimo endelevu, matumizi endelevu ya rasilimali za asili, uhifadhi wa bioanuai na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa hivyo, maudhui ya vipindi hivi yanaonesha namna televisheni inavyoweza kutumika kama njia ya mawasiliano ya mazingira kwa kuunganisha maarifa na vitendo vinavyolenga kupunguza uharibifu wa mazingira na kuimarisha uhifadhi wake. Aidha, matokeo haya yaliweza kufasiriwa kwa kutumia Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia**,** ambayo inasisitiza uchunguzi wa uhusiano kati ya binadamu na mazingira pamoja na umuhimu wa kuendeleza mahusiano yanayozingatia uendelevu wa mifumo ya ikolojia (Glotfelty & Fromm, 1996). Kwa mtazamo huu, *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* hazikuwasilishi mazingira kama chanzo cha rasilimali pekee, bali pia zilionesha changamoto zinazotokana na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali na hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kulinda mazingira**.** Hivyo, maudhui yanayowasilishwa katika vipindi hivyo yanaendana na msingi wa Uhakiki-Ikolojia kwa kuhamasisha uelewa kuhusu utegemeano wa binadamu na mazingira. Kwa upande wa utafiti huu, matokeo yalionesha kuwa mawasiliano ya televisheni yanaweza kuwa nyenzo muhimu katika kujenga uelewa wa mazingira na kuhamasisha jamii kuhusu hatua za uhifadhi**,** jambo linaloendana moja kwa moja na lengo la kuchanganua mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*.

4.1.1 Uhifadhi wa Udongo

Uhifadhi wa Udongo ni mbinu na hatua zinazochukuliwa kulinda udongo dhidi ya mmomonyoko, upotevu wa rutuba, na uharibifu mwingine ili uweze kuendelea kutumika kwa kilimo na shughuli nyingine kwa muda mrefu.

M-01-V-SSU

Kwa mfano *Shamba Shape-Up*, Series 14, Episode 1 (2024), “Fertiliser, Soil Test, Certified Seed and Compost,” inasisitiza umuhimu wa kufanya upimaji wa udongo kabla ya kutumia mbolea ili kubaini mahitaji ya virutubisho na aina ya mbolea inayofaa. Kipindi hiki kilichapishwa kwenye YouTube tarehe 19 Machi 2024, huku muda rasmi wa kurushwa kwenye Runinga ya Citizen ukiwa Jumamosi saa 1:30 jioni kwa toleo la Kiingereza na Jumapili saa 1:30 jioni kwa toleo la Kiswahili. Tarehe na saa ya kurekodiwa hazijaainishwa katika chanzo rasmi.

Mtaalamu wa mbolea katika shamba la Anastasia anasema kwamba:

> *“Ni muhimu kufanya upimaji wa udongo kwanza kabla ya kutumia mbolea, kwa sababu matokeo ya upimaji ndiyo yanaonyesha virutubisho vinavyyokosekana na aina sahihi ya mbolea inayohitajika shambani.”*

Nukuu hii inaonesha umuhimu wa upimaji wa udongo kama msingi wa kufanya maamuzi sahihi kuhusu matumizi ya mbolea na usimamizi wa rutuba ya ardhi. Kupitia upimaji wa udongo, mkulima hupata taarifa za kisayansi kuhusu hali ya udongo wake na hivyo kuwezeshwa kutumia mbolea kulingana na mahitaji halisi ya mazao na udongo husika. Hali hii husaidia kupunguza matumizi ya mbolea kupita kiasi, kupunguza gharama za uzalishaji na kuzuia madhara ya kimazingira yanayoweza kusababishwa na matumizi yasiyo sahihi ya pembejeo za kilimo. Kwa mantiki hiyo, upimaji wa udongo ni sehemu muhimu ya mikakati ya uhifadhi wa udongo kwa kuwa unachangia matumizi endelevu ya rasilimali za ardhi.

Kauli hii inaonesha kuwa uhifadhi wa udongo hauhusishi tu kuzuia mmomonyoko wa ardhi, bali pia matumizi ya maarifa ya kisayansi katika usimamizi wa rutuba ya udongo. Upimaji wa udongo huwapa wakulima uwezo wa kufanya maamuzi yanayotegemea ushahidi badala ya mazoea ya kawaida, jambo linalochangia kuongeza uzalishaji wa kilimo huku likilinda ubora wa udongo kwa muda mrefu. Aidha, matumizi ya mboji na samadi kama mbinu mbadala za kuongeza rutuba yanaonesha umuhimu wa mbinu endelevu zinazolenga kulinda mazingira na kupunguza utegemezi wa pembejeo za viwandani.

Nadharia ya uhakiki ikolojia inasisitiza kuwa udongo ni sehemu muhimu ya mfumo wa ikolojia unaopaswa kulindwa na kutumiwa kwa njia endelevu. Kwa mujibu wa nadharia hii, matumizi sahihi ya rasilimali za mazingira yanapaswa kuzingatia usawa kati ya mahitaji ya binadamu na uhifadhi wa mazingira. Hivyo, upimaji wa udongo unaonekana kama mbinu inayochangia matumizi endelevu ya ardhi na kuhifadhi afya ya mfumo wa ikolojia.

Matokeo haya yanaafikiana na utafiti wa *United Nations Environment Programme* (2022) katika *Global Environment Outlook 6: Youth, Media and Environmental Awareness*, ambao unaonesha kuwa vyombo vya habari vina nafasi muhimu katika kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala ya mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za asili. Utafiti huo unaeleza kuwa maudhui ya elimu ya mazingira yanayowasilishwa kupitia vyombo vya habari huwasaidia wananchi kuelewa changamoto za mazingira na kuchukua hatua sahihi za kuzitatua. Kwa kuzingatia hoja ya upimaji wa udongo, elimu inayotolewa kuhusu umuhimu wa kuchunguza hali ya udongo kabla ya matumizi ya mbolea huwajengea wakulima maarifa ya kisayansi yanayowasaidia kuhifadhi rutuba ya udongo na kuongeza tija ya kilimo. Hivyo, matokeo haya yanathibitisha kuwa mawasiliano ya mazingira yana mchango mkubwa katika kuhamasisha matumizi endelevu ya ardhi na uhifadhi wa udongo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Kwa kuhitimisha, uchambuzi unaonesha kuwa upimaji wa udongo ni mbinu muhimu ya uhifadhi wa udongo inayowezesha matumizi sahihi ya mbolea, kuimarisha rutuba ya ardhi na kulinda mazingira. Aidha, elimu inayotolewa kuhusu suala hili ina mchango mkubwa katika kujenga uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa usimamizi endelevu wa rasilimali za udongo.

> *Video yake inapatikana katika Kipindi cha Shamba Shape-Up Series 14 – Episode 1 https://shambashapeup.com/kenya-series/series-14/ep-1-fertilizer-soil-test-certified-seed-and-compost/*

4.1.2 Upandaji wa Miti na Uhifadhi wa Misitu

Upandaji wa miti na uhifadhi wa misitu ni muhimu sana kwa kulinda mazingira na kuboresha maisha ya viumbe hai. Miti husaidia kusafisha hewa kwa kufyonza gesi ya kaboni na kutoa oksijeni, huku pia ikizuia mmomonyoko wa udongo na mafuriko kwa kushikilia udongo kwa mizizi yake. Aidha, misitu ni makazi ya wanyama na ndege mbalimbali, hivyo uhifadhi wake husaidia kulinda viumbe hawa na kudumisha uwiano wa mazingira. Kwa sababu hizi, ni wajibu wa kila mtu kushiriki katika upandaji wa miti na kulinda misitu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

M-01-V-CP

Kwa mfano: *Citizen Planet*, “Saving Chepalungu Forest: KFS engages communities to restore Chepalungu Forest,” 14 Juni 2026, 10:43 pm, muda 8:58, KenyaMOJA/ Runinga ya Citizen

> *“Msitu wa Chepalungu unarejeshwa kupitia ushirikiano kati ya Kenya Forest Service na jamii, huku urejeshaji wa asili wa misitu ukitumika kuimarisha uhifadhi wa mazingira.”*

Nukuu hii inaonesha kuwa uhifadhi wa misitu hauwezi kufanikiwa kwa juhudi za serikali pekee, bali unahitaji ushirikiano wa karibu kati ya taasisi za uhifadhi na jamii zinazozunguka misitu. Katika video ya *Citizen Planet*, urejeshaji wa Msitu wa Chepalungu unaelezwa kuwa umechochewa na urejeshaji wa asili wa misitu pamoja na juhudi za pamoja za Kenya Forest Service na jamii. Ushirikishwaji wa jamii ni mkakati muhimu wa mawasiliano na uhifadhi**,** kwa sababu jamii inapopewa nafasi ya kushiriki katika kulinda na kurejesha misitu, hujenga uwajibikaji na umiliki wa rasilimali hizo. Hivyo, maudhui haya yanaonesha mchango wa *Citizen Planet* katika kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa ushirikiano, urejeshaji wa misitu na matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira.

Hoja hii inaonesha kuwa mafanikio ya uhifadhi na urejeshaji wa misitu yanategemea kwa kiasi kikubwa ushiriki wa jamii pamoja na ushirikiano wa taasisi za uhifadhi**.** Jamii zinaposhirikishwa katika upandaji miti, urejeshaji wa misitu na usimamizi wa rasilimali za misitu, hujenga uelewa, uwajibikaji na umiliki wa rasilimali zao za asili. Aidha, ushirikiano kati ya jamii na taasisi kama Kenya Forest Service husaidia kuzuia uharibifu wa misitu unaosababishwa na ukataji miti ovyo na matumizi yasiyo endelevu ya ardhi. Kwa hivyo, uhifadhi wa misitu hauhusiani na kulinda miti pekee, bali ni mkakati wa kurejesha mifumo ya ikolojia, kuhifadhi bioanuwai, kulinda vyanzo vya maji na kuhakikisha ustawi endelevu wa jamii na mazingira kwa ujumla.

Nadharia ya Uhakiki wa Ikolojia ina uhusiano mkubwa na nukuu ya Msitu wa Chepalungu, kwa sababu inachunguza uhusiano kati ya binadamu na mazingira pamoja na namna shughuli za binadamu zinavyoathiri mifumo ya ikolojia. Katika nukuu hiyo, urejeshaji wa Msitu wa Chepalungu kupitia ushirikiano kati ya Kenya Forest Service na jamii unaonesha mtazamo wa kuhifadhi mazingira kwa kutambua umuhimu wa misitu katika kudumisha uwiano wa kiikolojia. Aidha, ushiriki wa jamii katika urejeshaji wa misitu unaendana na Nadharia ya Uhakiki wa Ikolojia kwa kusisitiza uwajibikaji wa binadamu katika kulinda na kurejesha mazingira yaliyoharibiwa. Kwa hiyo, nukuu hii inaonesha kuwa uhifadhi wa Msitu wa Chepalungu si suala la kulinda miti pekee, bali ni juhudi za pamoja za binadamu za kurejesha mfumo wa ikolojia,

kuhifadhi bioanuwai na kuhakikisha uendelevu wa rasilimali za asili kwa vizazi vya sasa na vijavyo**.**

Hoja hii inaendana na mtazamo wa UNESCO (2021) kuhusu *Media and Information Literacy for the Public Good*, unaosisitiza umuhimu wa upatikanaji wa taarifa sahihi, uelewa wa maudhui ya vyombo vya habari na uwezo wa wananchi kutumia taarifa hizo kushiriki katika masuala ya manufaa ya umma na maendeleo endelevu. Uhusiano huu unaonekana katika kipindi cha *Citizen Planet* kuhusu urejeshaji wa Msitu wa Chepalungu, ambapo televisheni inaonesha ushirikiano kati ya Kenya Forest Service na jamii katika kurejesha msitu kupitia urejeshaji wa asili. Kwa namna hii, maudhui ya kipindi yanaunganisha taarifa za kimazingira na vitendo halisi vya uhifadhi, kwa kuwa watazamaji hawaonyeshwi tu changamoto ya uharibifu wa misitu, bali pia wanaoneshwa namna wadau mbalimbali wanavyoshirikiana katika kuitatua. Maudhui haya yanaonesha kuwa *Citizen Planet* inatekeleza dhima ya mawasiliano ya mazingira kwa kutumia televisheni kama chombo cha elimu, uhamasishaji na ujenzi wa uwajibikaji wa kijamii. Kwa kuonesha uzoefu wa Chepalungu, kipindi kinawapa wananchi mfano unaoeleweka wa namna jamii inaweza kuwa mshirika muhimu katika urejeshaji na usimamizi wa misitu. Aidha, uwasilishaji wa juhudi za Kenya Forest Service na jamii unaonesha kuwa uhifadhi wa mazingira si jukumu la serikali pekee, bali ni jukumu la pamoja linalohitaji maarifa, ushirikiano na ushiriki wa wananchi**.** Hivyo, maudhui ya *Citizen Planet* yanaweza kuchangia kubadili mtazamo wa watu kutoka kuona uharibifu wa misitu kama tatizo lisilo na suluhisho hadi kutambua kwamba ushiriki wa jamii, taarifa sahihi na mikakati ya urejeshaji vinaweza kusaidia kurejesha mifumo ya ikolojia na kuhakikisha uendelevu wa rasilimali za misitu**.**

> *Kipindi hiki kinaweza kupatikana katika: https://www.kenyamoja.com/video/saving-chepalungu-forest-kfs-engages-communities-restore-chepalungu-forest-citizen-tv-364705?*

4.1.3 Uhifadhi wa Bioanuai

Uhifadhi wa bioanuai ni mchakato wa kulinda, kusimamia na kutumia kwa njia endelevu aina zote za viumbe hai, yaani wanyama, mimea na viumbe vidogo pamoja na makazi yao ya asili ili kuhakikisha kuwa hazitoweki na zinaendelea kuwepo kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo. Hoja hii inahusisha hatua kama kulinda misitu, kupanda miti, kuzuia uharibifu wa makazi ya viumbe hai, kudhibiti uchafuzi wa mazingira na kusimamia matumizi ya rasilimali za asili kwa uwiano. Hivyo basi, uhifadhi wa bioanuai unamaanisha kuhakikisha kuwa mifumo ya maisha ya

asili inabaki imara na yenye uwiano, ili kudumisha afya ya mazingira na ustawi wa binadamu kwa ujumla.

M-02-V-SSU

Kwa mfano: *Shamba Shape-Up* series 15 episode 13 Agro-biodiversity, agroforestry, kilimo mseto na ufugaji na mkulima Beatrice Ojwang, North Alego, Siaya. Kiswahili siku ya Jumapili, saa 1:30 mchana na Kiingereza Jumamosi, saa 1:30 mchana.

> "*Kilimo mseto na upandaji wa miti shambani husaidia kuboresha udongo, kulinda ardhi na kuongeza bioanuai, huku mseto wa mazao na ufugaji ukiimarisha ustahimilivu wa shamba."*

Nukuu hii inaeleza kuwa kilimo mseto inaonesha kuwa uhifadhi wa bioanuai na urejeshaji wa mifumo ya ikolojia unaweza kuunganishwa na shughuli za uzalishaji wa kilimo. Katika shamba ya Beatrice Ojwang, mkulima kutoka North Alego, Siaya, anaoneshwa akitumia mbinu za kilimo mseto kwa lengo la kuboresha udongo, kulinda ardhi na kuongeza ustahimilivu wa shamba. Kwa hivyo, maudhui haya yanaonesha kuwa mkulima anaweza kuwa mzalishaji wa chakula na wakati huohuo mhifadhi wa mazingira, kwa kutumia miti, mazao na mifugo kwa namna inayosaidia kulinda udongo na kudumisha bioanuai. Aidha, kuwasilisha mbinu hizi kupitia uzoefu halisi wa mkulima kunafanya ujumbe wa uhifadhi kuwa wa vitendo na unaoweza kueleweka na kutekelezwa na watazamaji. Hivyo, kipindi kinaonesha umuhimu wa kuunganisha uzalishaji wa kilimo, matumizi endelevu ya rasilimali na uhifadhi wa mazingira ili kukidhi mahitaji ya sasa bila kuhatarisha uwezo wa vizazi vijavyo kutumia rasilimali hizo.

Hoja hii inasisitiza jinsi kilimo mseto kinaifanya jamii kuwa seh4emu ya moja kwa moja ya suluhisho la changamoto za mazingira, kwa sababu mkulima mwenyewe anashiriki katika kutekeleza mbinu zinazounganisha uzalishaji na uhifadhi. Upandaji wa miti pamoja na mazao na ufugaji hauishii katika kuongeza uzalishaji au kipato, bali pia unaweza kusaidia kulinda ardhi, kuboresha afya ya udongo, kuhifadhi bioanuai na kuongeza ustahimilivu wa mfumo wa kilimo. Hivyo, tofauti na mtazamo unaomchukulia mwanajamii kama mpokeaji wa elimu ya mazingira pekee, *Shamba Shape-Up* inamwasilisha mkulima kama mshiriki na mtekelezaji wa uhifadhi. Kwa namna hiyo, maudhui ya kipindi yanaunga mkono hoja kwamba elimu na uhamasishaji wa mazingira huwa na ufanisi zaidi pale unapounganishwa na vitendo vinavyotekelezwa katika mazingira halisi ya jamii.

Dondoo hii ina uhusiano mkubwa na nadharia ya uhakiki ikolojia kwa kuwa, maudhui haya yanaonesha uhusiano wa karibu kati ya shughuli za binadamu na uhifadhi wa mazingira. Kilimo mseto kinapowezesha mkulima kuunganisha miti, mazao na mifugo katika mfumo mmoja wa uzalishaji, uzalishaji wa chakula hauonekani tena kuwa kinyume na uhifadhi wa mazingira, badala yake, shughuli za kilimo zinaweza kufanyika kwa namna inayolinda ardhi na kuboresha afya ya udongo. Kwa hivyo, nukuu hii inadhihirisha msingi muhimu wa Uhakiki wa Ikolojia kwamba binadamu ni sehemu ya mfumo wa ikolojia na anapaswa kutumia mazingira kwa namna inayodumisha uwiano wake. Katika mfano wa Beatrice, mkulima anakuwa si mtumiaji wa rasilimali za mazingira pekee, bali pia mshiriki katika uhifadhi wake**.** Hivyo, kilimo mseto kinaweza kuchukuliwa kama mkakati unaounganisha mahitaji ya kiuchumi ya mkulima na wajibu wa kulinda mazingira. Mtazamo huu unaifanya *Shamba Shape-Up* kuwasilisha uhifadhi wa mazingira kama sehemu ya maisha na shughuli za kila siku za jamii, badala ya kuuona kama jukumu la taasisi za mazingira pekee.

Matokeo haya yanaendana kwa kiasi kikubwa na Chemarum (2023)**,** *Coverage of environmental issues by the Kenyan media: A case study of Citizen Televisio*n**,** hasa katika msisitizo wake kuhusu umuhimu wa mawasiliano, ushiriki wa jamii na matumizi endelevu ya rasilimali katika kukabiliana na changamoto za mazingira. Uhusiano huu unaonekana katika nukuu ya kilimo mseto kutoka *Shamba Shape-Up* Series 15, Episode 13, ambapo kilimo mseto cha mazao na mifugo kinaoneshwa kama mbinu zinazoweza kuboresha udongo, kulinda ardhi na kuongeza ustahimilivu wa shamba. Kwa hivyo, Chemarum anaangazia umuhimu wa kuwawezesha jamii kupitia mawasiliano na elimu ya mazingira**,** wakati *Shamba Shape-Up* inaonesha jinsi maarifa hayo yanavyoweza kubadilishwa kuwa vitendo katika ngazi ya mkulima**.** Hivyo, kilimo mseto kinakuwa mfano wa matumizi endelevu ya rasilimali unaounganisha uzalishaji wa chakula na uhifadhi wa mazingira, kwa kuwa upandaji wa miti pamoja na mazao na ufugaji unaweza kusaidia kulinda udongo, kuongeza bioanuai na kuimarisha ustahimilivu wa mfumo wa kilimo. Aidha, kipindi kinatumia uzoefu halisi wa mkulima kuwasilisha ujumbe huu, jambo linaloendana na msisitizo wa Chemarum kwamba mawasiliano bora yanaweza kuongeza uelewa na kuchochea hatua za pamoja dhidi ya changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Kwa hivyo**,** tofauti kuu ni kwamba Chemarum (2023) anatoa mwongozo wa kimkakati wa mawasiliano ya mabadiliko ya tabianchi katika ngazi ya kikanda, wakati *Shamba Shape-Up* inatoa mfano wa vitendo wa namna maarifa ya uhifadhi yanavyoweza kutekelezwa na mkulima katika shamba

lake**.** Hoja hizi mbili zinaunganishwa na dhana ya ushiriki wa jamii, matumizi endelevu ya rasilimali na uendelevu wa mazingira.

> *Video inayolingana na hoja hii inapatikana kwa Shamba Shape-Up Series 15 Episode 13: Agro-biodiversity & Agroforestry*
> *https://shambashapeup.com/kenya-series/series-15/ep-13-agro-biodiversity-agroforestry-and-tiller-and-shamba-ni-biz-drama/*

4.1.4 Matumizi ya Nishati Safi

Matumizi ya nishati safi ni matumizi ya vyanzo vya nishati visivyozalisha au vinavyozalisha kwa kiwango kidogo sana gesi chafu na uchafuzi wa mazingira, hivyo kuchangia katika uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Nishati safi inajumuisha vyanzo kama nishati ya jua, upepo, maji, gesi asilia inayozalishwa kwa njia endelevu na gesi ya bayolojia**,** ambavyo ni salama zaidi kwa mazingira kuliko matumizi ya kuni, mkaa na mafuta ya kisukuku. Matumizi ya nishati hizi husaidia kupunguza ukataji miti, kuboresha ubora wa hewa, kulinda afya za binadamu na kupunguza athari za ongezeko la joto duniani. Hivyo, matumizi ya nishati safi ni hatua muhimu katika kuendeleza maendeleo endelevu kwa kuhakikisha kuwa mahitaji ya nishati yanatimizwa bila kuhatarisha mazingira na ustawi wa vizazi vya sasa na vijavyo.

M-O2-V-CP

Kwa mfano: Runinga ya Citizen / KenyaMOJA Mageta Island shines as a model for renewable energy Tarehe 3 Aprili 2026 Saa ya kuchapishwa/kurushwa kwenye KenyaMOJA: 9:51 usiku Urefu wa video: dakika 4:33**.**

> *“Matumizi ya nishati safi na mbadala katika Kisiwa cha Mageta yamepunguza utegemezi wa nishati zinazochafua mazingira, huku nishati ya jua ikiwezesha shule, hospitali na biashara kupata huduma ya umeme.*

Nukuu hii inaeleza kuwa, hoja hii inaendana kwa kiasi kikubwa na maudhui ya video ya Mageta Island shines as a model for renewable energy, kwa sababu video inaonesha matumizi ya Mageta Solar Mini Grid kama mfano wa mpito kuelekea nishati safi na mbadala. Chanzo kinaeleza kuwa shule, hospitali na biashara katika Kisiwa cha Mageta zinatumia nishati ya jua, huku mradi huo ukihudumia takribani watu 25,000. Kwa mfano, Mageta unaonesha kwamba matumizi ya nishati safi yanaweza kuhusisha uhifadhi wa mazingira pamoja na maendeleo ya kijamii na kiuchumi**,**

kwa kuwa nishati ya jua inawezesha upatikanaji wa huduma muhimu, kuimarisha shughuli za biashara na kuboresha maisha ya jamii. Hivyo, maudhui ya Runinga ya Citizen yanaonesha kwa vitendo kwamba mpito kutoka vyanzo vya nishati vinavyotegemea mafuta ya kisukuku kwenda kwenye nishati mbadala si hatua ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pekee, bali pia ni mkakati wa kuongeza upatikanaji wa nishati, kuimarisha ustawi wa jamii na kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira**.**

Kauli hii inasisitiza umuhimu wa kubadili mifumo ya uzalishaji na matumizi ya nishati ili kuendana na mahitaji ya uhifadhi wa mazingira. Kuendelea kutegemea mafuta ya kisukuku kunaongeza uharibifu wa mazingira na kuhatarisha maisha ya viumbe hai, hivyo matumizi ya nishati safi yanapaswa kupewa kipaumbele katika sera na mipango ya maendeleo. Kuna haja ya jamii, serikali na taasisi mbalimbali kuwekeza katika teknolojia za nishati safi pamoja na kutoa elimu kwa umma ili kuongeza matumizi yake na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hoja hii ina uhusiano na nadharia ya uhakiki ikolojia kwa sababu nadharia hiyo huchunguza namna shughuli za binadamu zinavyoathiri mazingira na kusisitiza haja ya kuwepo kwa uwiano kati ya binadamu na asili Uhakiki ikolojia hukosoa matumizi ya rasilimali kwa njia inayosababisha uharibifu wa mazingira na kuhimiza mitazamo endelevu inayolinda mifumo ya ikolojia. Kwa hiyo, matumizi ya nishati safi yanaonekana kama hatua ya kurekebisha uhusiano kati ya binadamu na mazingira kwa kupunguza uchafuzi, kulinda bioanuai na kuhakikisha maendeleo yanayozingatia uendelevu wa sayari.

Utafiti wa Chemarum, S. C. (2023). *Coverage of environmental issues by the Kenyan media: A case study of Citizen Television* una uhusiano na nukuu hii. Utafiti wa Nkabala unaonesha kuwa televisheni ina nafasi muhimu katika kuongeza uelewa wa umma kuhusu masuala ya mazingira kwa kutoa taarifa, elimu na kuhamasisha jamii kuchukua hatua za kulinda mazingira. Vilevile, nukuu inaeleza umuhimu wa kuchukua hatua za kimazingira kupitia matumizi ya nishati safi ili kupunguza uchafuzi na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hivyo, tafiti hizi mbili zinaungana katika kuonyesha kuwa uelewa wa jamii ni msingi wa mabadiliko ya tabia; ambapo televisheni inaweza kusaidia kufikisha elimu kuhusu faida za nishati safi na kuhamasisha matumizi ya teknolojia endelevu. Kwa ujumla, Chemarum anaangazia nafasi ya mawasiliano katika kujenga uelewa wa mazingira, wakati nukuu inaeleza hatua ya vitendo inayoweza kuchukuliwa ili kufikia uendelevu wa mazingira.

Kipindi hiki kinapatikana katika: Runinga ya Citizen – Mageta Island shines as a model for renewable energy Mageta Island shines as a model for renewable energy

4.1.5 Uhifadhi wa Maji

Uhifadhi wa maji ni mchakato wa kulinda, kukusanya na kutumia maji kwa njia endelevu ili kuhakikisha yanapatikana kwa matumizi ya sasa na ya baadaye. Uhifadhi huu unahusisha mbinu mbalimbali kama vile kuvuna maji ya mvua, kuzuia uchafuzi wa vyanzo vya maji, kupanda miti ili kuhifadhi mazingira, na kutumia maji kwa uangalifu bila kuyapoteza. Uhifadhi wa maji ni muhimu kwa sababu husaidia kukidhi mahitaji ya binadamu, kilimo, mifugo na viumbe wengine hai, hasa wakati wa ukame au mabadiliko ya tabianchi. Kwa hivyo, kila mtu anapaswa kushiriki katika juhudi za kuhifadhi maji ili kuhakikisha rasilimali hii muhimu inaendelea kupatikana kwa vizazi vijavyo.

M-03-V-SSU

Kwa mfano: *Shamba Shape-Up* – Series 15, Episode 9: Water Storage, Drip Irrigation, Compost and Conservation Agriculture tarehe 19 Mei 2025 *Shamba Shape-Up* / Mediae

> "*Uvunaji na uhifadhi wa maji pamoja na matumizi ya umwagiliaji wa matone husaidia kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa mazao na matumizi bora ya rasilimali ya maji katika shamba."*

Nukuu hii inaonesha kuwa usimamizi endelevu wa maji ni sehemu muhimu ya uhifadhi wa mazingira na uendelevu wa kilimo**.** Katika *Shamba Shape-Up* Series 15, Episode 9, kipindi kinawasilisha uvunaji na uhifadhi wa maji pamoja na umuhimu wa umwagiliaji wa matone kama mbinu za kuhakikisha maji yanapatikana kwa mazao na yanatumika kwa ufanisi. Ujumbe huu una umuhimu kwa mazingira kwa sababu matumizi bora ya maji hupunguza upotevu wa rasilimali hiyo na kumwezesha mkulima kukabiliana na vipindi vya ukame na mabadiliko ya upatikanaji wa mvua. Aidha, kuwasilisha mbinu hizi kupitia televisheni kunafanya maarifa ya uhifadhi wa maji kuwa ya vitendo na yanayoweza kueleweka na jamii ya wakulima. Hivyo, maudhui ya kipindi yanaonesha kuwa kilimo chenye tija na uhifadhi wa mazingira vinaweza kuunganishwa kupitia matumizi yenye ufanisi ya maji, jambo linalochangia uendelevu wa uzalishaji wa kilimo na uhifadhi wa rasilimali za asili.

Hoja hii ya usimamizi mzuri wa mifumo ya umwagiliaji na uvunaji wa maji ni hatua muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula na uhifadhi wa mazingira. Ukaguzi wa mara kwa mara wa mifumo hii husaidia kuzuia upotevu wa maji, kuongeza uzalishaji wa mazao na kupunguza utegemezi wa mvua ambazo zimekuwa hazitabiriki kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, kutoa elimu kwa wakulima kuhusu teknolojia za kuhifadhi maji na matumizi endelevu ya rasilimali ni muhimu katika kujenga kilimo kinacholinda mazingira na kusaidia maisha ya jamii.

Dondoo hii ina uhusiano mkubwa na nadharia ya uhakiki ikolojia kwa sababu nadharia hiyo huchunguza uhusiano kati ya binadamu na mazingira pamoja na namna shughuli za binadamu zinavyoweza kuathiri mifumo ya asili. Uhakiki ikolojia husisitiza matumizi ya rasilimali kwa uwajibikaji na kupinga matumizi yanayosababisha uharibifu wa mazingira. Kwa hiyo, matumizi ya umwagiliaji wa matone na uvunaji wa maji yanaonyesha mtazamo wa kiikolojia unaolenga kuhifadhi rasilimali za maji, kupunguza shinikizo kwa mazingira na kuendeleza mahusiano endelevu kati ya binadamu na asili.

Hoja hii inaungwa mkono na tafiti za *United Nations Environment Programme (UNEP)* **(**2022) pamoja na utafiti wa International Food Policy Research Institute (IFPRI) na Wageningen University & Research (2022). Tafiti hizi zinaonesha umuhimu wa matumizi endelevu ya rasilimali za asili, hasa maji, katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha uzalishaji wa kilimo. UNEP (2022) inasisitiza umuhimu wa uhifadhi wa mazingira, matumizi bora ya rasilimali na kuhamasisha jamii kutumia mbinu zinazopunguza athari za mazingira. Vilevile, IFPRI na Wageningen University (2022) wanaeleza umuhimu wa teknolojia na mikakati ya kilimo endelevu, ikiwemo usimamizi bora wa maji, ili kuongeza uzalishaji wa chakula huku ikipunguza shinikizo kwa mifumo ya ikolojia. Hivyo, tafiti hizi zinaunga mkono nukuu kwa kuonyesha kuwa ukaguzi na matumizi sahihi ya mifumo ya umwagiliaji na uvunaji wa maji ni njia muhimu ya kuhifadhi maji, kukabiliana na ukame na kuhakikisha kilimo endelevu katika mazingira yanayobadilika.

> *Video ya kipindi hiki inapatikana kwa Shamba Shape-Up – Series 15 Episode 9: Water Storage, Drip Irrigation, Compost and Conservation Agriculture*

4.1.6 Kilimo Hai na Matumizi ya Mbolea Asilia

Kilimo hai na matumizi ya mbolea asilia ni mfumo wa kilimo unaolenga uzalishaji wa mazao bila kutumia kemikali za viwandani, bali unategemea mbinu za asili kama vile mboji, samadi ya

mifugo, mabaki ya mazao na mimea ya kijani ili kuboresha rutuba ya udongo. Mfumo huu husaidia kuongeza ubora wa udongo, kuimarisha uwezo wake wa kuhifadhi maji na kuboresha afya ya mimea kwa njia endelevu. Aidha, kilimo hai hupunguza uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na mbolea na viuatilifu vya kemikali, hivyo kulinda udongo na vyanzo vya maji. Pia hupunguza gharama za uzalishaji kwa mkulima na kuhakikisha mazao yanayozalishwa ni salama kwa afya ya binadamu kwa kuwa hayana mabaki ya kemikali hatarishi. Kwa ujumla, kilimo hai ni mbinu ya kilimo endelevu inayosaidia kuongeza uzalishaji, kulinda mazingira na kuhakikisha usalama wa chakula kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

M-04-V-SSU

Kwa mfano: video ya Shape Up Series 15 – Episode 6: Improved Kienyeji, Feeds, Vermi Compost & Spraying Tarehe ya kuchapishwa: 22 Aprili 2025 Mahali**:** Ugenya, Siaya County, Kenya.

> "*Jinsi ya kuboresha afya ya udongo kwa kutumia mbolea inayotokana na mboji na minyoo."*

Mtafiti anabaini kuwa matumizi ya Vermi Compost yanatoa mchango muhimu katika kukuza kilimo hai na uhifadhi wa mazingira kwa kuonesha namna wakulima wanavyoweza kutumia rasilimali za kikaboni kuboresha afya na rutuba ya udongo. Kauli "Jinsi ya kuboresha afya ya udongo kwa kutumia Vermi Compost" inaonesha kuwa *Shamba Shape-Up* haitoi elimu ya kilimo pekee, bali pia inahamasisha matumizi ya mbolea asilia kama njia ya kupunguza utegemezi wa pembejeo za kemikali, kurejesha rutuba ya udongo na kuchakata mabaki ya kikaboni kuwa rasilimali yenye manufaa. Kwa mtazamo wa mtafiti, uwasilishaji wa maarifa haya kupitia televisheni unaongeza uelewa wa wakulima kuhusu mbinu rafiki kwa mazingira na kuwawezesha kuona kuwa uhifadhi wa udongo unaweza kuunganishwa na uzalishaji endelevu wa mazao. Hivyo, kipindi kinatimiza nafasi ya elimu na uhamasishaji wa jamii kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira**.**

Kauli hii inaonesha kuwa uhamasishaji wa matumizi ya Vermi Compost unachangia kukuza kilimo hai kwa kuboresha afya na rutuba ya udongo**,** huku ukihimiza matumizi ya mabaki ya kikaboni kama rasilimali ya kilimo. Kwa hivyo, matumizi ya Vermi Compost yanaweza kupunguza utegemezi wa pembejeo za kemikali na hivyo kuunga mkono mbinu za kilimo

zinazozingatia uhifadhi wa mazingira. Aidha, uhamasishaji wa teknolojia hii kupitia *Shamba Shape-Up* unawawezesha wakulima kutambua thamani ya taka za kikaboni na kuzitumia katika uzalishaji wa mbolea asilia. Hivyo, ujumbe huu unaunganisha uboreshaji wa rutuba ya udongo, uzalishaji endelevu wa chakula na uhifadhi wa mazingira**,** na kuonesha nafasi ya televisheni katika kuelimisha jamii kuhusu mbinu rafiki kwa mazingira

Nukuu hii ina uhusiano mkubwa na nadharia ya uhakiki ikolojia kwa sababu nadharia hiyo inasisitiza umuhimu wa kuwepo kwa uwiano kati ya binadamu na mazingira pamoja na matumizi ya rasilimali kwa njia endelevu. Uhakiki ikolojia hukosoa mifumo ya uzalishaji inayosababisha uharibifu wa asili na kuhimiza mbinu zinazolinda mifumo ya ikolojia. Kwa hiyo, matumizi ya minyoo katika kutengeneza mboji yanaakisi mtazamo wa kiikolojia kwa kuwa yanarudisha virutubisho ardhini, yanapunguza uchafuzi wa mazingira na yanaunga mkono kilimo kinachoheshimu uwezo wa asili kujirekebisha.

Utafiti wa Chemarum (2023) Coverage *of Environmental Issues by the Kenyan Media: A Case Study of Citizen Television* una uhusiano na hoja hii. Utafiti wa Chemarum unaonesha umuhimu wa mawasiliano ya mabadiliko ya tabianchi katika kuongeza uelewa wa jamii, kuhamasisha matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira na kujenga uwezo wa wananchi kukabiliana na changamoto za kimazingira. Mkakati huo unasisitiza kuimarisha elimu ya mazingira, usambazaji wa taarifa na ushirikishwaji wa wadau ili kuwezesha jamii kuchukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa upande mwingine, matumizi ya minyoo kutengeneza mboji inaeleza njia ya vitendo ya kuhifadhi mazingira kupitia kilimo endelevu, kwa kubadilisha taka za kikaboni kuwa mbolea yenye manufaa kwa udongo na mazao. Hivyo, tafiti hizi mbili zinaungana kwa kuonyesha kuwa uendelevu wa mazingira unahitaji siyo tu teknolojia na mbinu bora kama utengenezaji wa mboji, bali pia elimu na mawasiliano bora yanayowafanya wakulima na jamii kuelewa na kutumia mbinu hizo. Kwa ujumla, utafiti huu unaangazia nafasi ya taarifa na uhamasishaji katika kuchochea hatua za mazingira, wakati nukuu inaonyesha utekelezaji wa hatua hizo kupitia matumizi ya teknolojia ya asili inayolinda afya ya udongo na kuongeza uzalishaji endelevu.

https://www.youtube.com/watch?v=oj5IAkzAD5w&utm

4.1.7 Usimamizi Endelevu wa Taka Ngumu kupitia Urejelezaji

Mfano mwingine wa video ya masuala ya uhifadhi wa mazingira inapatikana *Citizen Planet* kuhusu How Mombasa youth are turning waste papers into waste bins Tarehe ya kuchapishwa: 22 Juni 2025 Chanzo: Runinga ya Citizen Kenya Eneo la Mikindani, Jomvu Constituency,

M-03-V-CP

> "*Ubadilishaji wa taka za karatasi kuwa mapipa ya taka unaonesha namna ubunifu wa vijana unavyoweza kusaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira na kuhimiza usimamizi endelevu wa taka katika jamii."*

Nukuu hii inaonesha kuwa *Citizen Planet* inawasilisha taka kama rasilimali inayoweza kurejelewa na kutumika tena**,** badala ya kuonekana kama uchafu usio na thamani. Mpango wa vijana wa Mikindani unaonesha kuwa usimamizi wa taka unaweza kuhusisha ubunifu, ushiriki wa jamii na matumizi ya teknolojia rahisi katika kutatua changamoto za kimazingira. Ubadilishaji wa taka za karatasi kuwa mapipa ya taka unasaidia kupunguza kiasi cha taka kinachoishia katika mazingira, huku ukiibua fursa ya kutumia taka kama malighafi yenye thamani. Kwa mtazamo huu, *Citizen Planet* haijishughulishi tu na kuonesha tatizo la uchafuzi wa mazingira, bali pia inaonesha suluhisho linalotekelezwa na jamii yenyewe**,** jambo linaloweza kuhamasisha hadhira kuiga vitendo vya urejeleaji na matumizi endelevu ya rasilimali. Aidha, ujumbe huu unaonesha umuhimu wa kuwashirikisha vijana katika uhifadhi wa mazingira, kwa kuwa wanakuwa sehemu ya utatuzi wa changamoto badala ya kuwa watazamaji wa matatizo ya mazingira. Hivyo, video hii inahusiana moja kwa moja na usimamizi endelevu wa taka ngumu, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira na uhamasishaji wa jamii kuhusu uchumi unaozingatia urejeleaji na matumizi tena ya rasilimali**.**

Kwa mtazamo wa Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia, ujumbe huu unaonesha uhusiano wa karibu na utegemeano kati ya binadamu, taka na mazingira**,** kwa kusisitiza kwamba namna binadamu anavyotumia na kutupa rasilimali ina athari katika afya ya mazingira. Nukuu hii inaonesha mabadiliko ya mtazamo kutoka kuiona taka kama kitu kisichokuwa na thamani kwenda kuichukulia kama rasilimali inayoweza kurejelewa, kutumika tena na kupewa thamani mpya**.** Kitendo cha vijana wa Mikindani kubadilisha taka za karatasi kuwa mapipa ya taka kinaonesha kwamba jamii inaweza kushiriki moja kwa moja katika kupunguza uchafuzi wa mazingira kupitia ubunifu na matumizi endelevu ya rasilimali. Kwa mujibu wa mtazamo wa Uhakiki-Ikolojia, suala la mazingira haliwezi kutenganishwa na shughuli na maamuzi ya binadamu; hivyo, tabia za uzalishaji, matumizi, utupaji na urejeleaji wa taka zina nafasi katika kuamua hali

ya mazingira. Katika muktadha huu, *Citizen Planet* haioneshi tu athari za taka katika mazingira, bali pia inawasilisha uwezekano wa kupata suluhisho kupitia hatua za jamii**,** hususan vijana. Aidha, ujumbe huu unaashiria umuhimu wa kujenga utamaduni wa kupunguza taka, kurejeleza na kutumia tena rasilimali**,** jambo linaloweza kupunguza shinikizo kwa mazingira na kusaidia matumizi endelevu ya maliasili. Hivyo, kwa kuzingatia nukuu hii, mtafiti anaona kuwa *Citizen Planet* inatekeleza dhima ya kimazingira kwa kuhamasisha hadhira kutambua kuwa uhifadhi wa mazingira hauishii katika sera au taasisi pekee, bali huanzia katika mabadiliko ya mitazamo na vitendo vya kila siku vya mtu na jamii katika namna wanavyoshughulikia taka na kutumia rasilimali za mazingira

Matokeo ya utafiti huu yanaunga mkono hoja ya *United Nations Environment Programme* (UNEP, 2021) katika GEO-6 for Youth, ambayo inasisitiza kuwa vijana wana nafasi muhimu katika kuchochea mabadiliko ya kimazingira kupitia maarifa, ubunifu, vitendo vya kila siku na ushiriki wa jamii katika shughuli endelevu. Ufanano huu unaonekana katika video ya *Citizen Planet*, How Mombasa Youth Are Turning Waste Papers into Waste Bins, ambapo vijana wanaoneshwa wakibadilisha taka za karatasi kuwa mapipa ya taka, hatua inayochangia urejeleaji wa rasilimali na kupunguza uchafuzi wa mazingira. Kwa hivyo, video hii inadhihirisha kwa vitendo msisitizo wa UNEP kwamba vijana wanaweza kuwa mawakala wa mabadiliko ya mazingira kupitia hatua zinazotekelezwa katika jamii zao. Hata hivyo, tofauti ni kwamba UNEP inatoa mtazamo mpana wa kimataifa kuhusu nafasi ya vijana katika kukabiliana na changamoto mbalimbali za mazingira, wakati utafiti huu unaangazia namna *Citizen Planet* inavyowasilisha mfano mahususi wa vijana wa Mombasa na shughuli zao za usimamizi wa taka. Kwa msingi huo, utafiti huu unaongeza maarifa kwa kuonesha kuwa televisheni inaweza kuwa chombo muhimu cha kuibua, kuonesha na kuhamasisha vitendo vya vijana katika uhifadhi wa mazingira**,** kwa kugeuza shughuli za kawaida za jamii kuwa mifano inayoweza kueleweka na kuigwa na hadhira.

*Mombasahttps://www.youtube.com/watch?v=wP4U04g69b4&utm_*

4.2 Changamoto Zinazoibuka Kutokana na Kutohifadhi Mazingira

Katika sehemu hii, mtafiti alichambua data iliyokusanywa kutoka katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa lengo la kubainisha changamoto zinazotokana na kutohifadhi mazingira. Katika uchambuzi huo, mtafiti alibainisha mada ndogondogo zinazoakisi namna baadhi ya shughuli za binadamu na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za mazingira

vinavyochangia kudhoofisha mifumo ya ikolojia, hususan katika maeneo ya kilimo, maji na udongo. Uchanganuzi huu uliongozwa na mhimili wa nadharia ya uhakiki-ikolojia unaoangazia athari za mtazamo wa binadamu unaotanguliza matumizi ya mazingira bila kuzingatia uendelevu wake. Aidha, mtafiti alitumia nukuu na mifano kutoka katika vipindi teule kuonesha namna changamoto hizo zinavyojitokeza katika maudhui ya vyombo vya habari, hivyo kuwezesha kuelewa kwa kina athari za kutohifadhi mazingira na umuhimu wa kuimarisha mbinu endelevu za matumizi ya rasilimali za asili.

4.2.1 Changamoto za Mmomonyoko wa Udongo

Mmomonyoko wa udongo ni mchakato wa kuondolewa au kusombwa kwa tabaka la juu la udongo lenye rutuba kutoka sehemu moja kwenda nyingine kutokana na nguvu za asili kama vile maji ya mvua, upepo au shughuli za binadamu. Tabaka hili la juu la udongo ndilo lenye virutubisho muhimu kwa ukuaji wa mimea, hivyo kupotea kwake husababisha kupungua kwa rutuba ya ardhi na kushuka kwa uzalishaji wa kilimo. Mmomonyoko wa udongo unaweza kusababishwa na ukataji miti ovyo, kilimo kisichozingatia hifadhi ya udongo, malisho ya kupita kiasi na matumizi mabaya ya ardhi. Ili kudhibiti tatizo hili, hatua kama upandaji wa miti, kilimo cha matuta, kufunika udongo kwa mabaki ya mimea na matumizi ya mbinu za kilimo hifadhi hutumika ili kulinda udongo na kuhakikisha uendelevu wa uzalishaji wa kilimo.

M-05-V-SSU

Kwa mfano: *Shamba Shape-Up* – Series 15, Episode 8: “Soil Health”

> *“Utunzaji wa afya ya udongo ni muhimu katika kudumisha rutuba ya ardhi na kuhakikisha uzalishaji endelevu wa mazao.”*

Kauli hii inaonesha kuwa utunzaji wa afya ya udongo ni msingi wa kudumisha rutuba ya ardhi na kuhakikisha uzalishaji endelevu wa mazao. Matumizi ya mbinu za uhifadhi wa udongo, kama ujenzi wa matuta na upandaji wa nyasi kwenye kingo, husaidia kupunguza kasi ya maji yanayotiririka, kuzuia mmomonyoko na kupunguza upotevu wa udongo wenye rutuba na virutubisho muhimu kwa mimea. Aidha, nyasi zinazopandwa kwenye kingo husaidia kushikilia udongo kwa mizizi yake na kupunguza athari za maji ya mvua, hivyo kulinda muundo na ubora wa udongo. Kwa hivyo, uhifadhi wa udongo haupaswi kuonekana kama njia ya kukabiliana na mmomonyoko pekee, bali kama mkakati wa muda mrefu wa kuhifadhi rutuba ya ardhi, kuongeza

tija ya kilimo na kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Hoja hii ya matumizi ya matuta na nyasi kingo ni njia muhimu ya kuunganisha uzalishaji wa kilimo na uhifadhi wa mazingira. Kwa kuwa mmomonyoko wa udongo ni tishio kubwa linalopunguza rutuba ya ardhi na kuathiri usalama wa chakula, wakulima wanapaswa kupewa elimu kuhusu mbinu hizi za uhifadhi. Aidha, usimamizi mzuri wa ardhi kupitia teknolojia rahisi kama matuta na uoto kinga unaweza kusaidia kupunguza uharibifu wa mazingira, kuongeza uzalishaji wa mazao na kuhifadhi rasilimali za ardhi kwa vizazi vijavyo.

Nukuu hii ina uhusiano mkubwa na nadharia ya uhakiki ikolojia kwa sababu nadharia hiyo inasisitiza uhusiano wa karibu kati ya binadamu na mazingira pamoja na matumizi ya rasilimali kwa njia endelevu. Uhakiki ikolojia hukosoa shughuli za kibinadamu zinazosababisha uharibifu wa mifumo ya asili na kuhimiza mbinu zinazolinda uwiano wa kiikolojia. Hivyo, ujenzi wa matuta na upandaji wa nyasi kingo vinaakisi mtazamo wa uhakiki ikolojia kwa kuwa vinasaidia kurejesha na kulinda mazingira, kuhifadhi udongo na kuendeleza kilimo kinachozingatia uwezo wa asili wa kujirekebisha.

Tafiti za Alago et al. (2024) katika *Nature-Based Solutions to Land Degradation in East African Savannahs na ripoti ya Farm Radio International (2024)* kuhusu *Shamba Shape-Up* Series 14 KAP Report (Kenya**)** zina uhusiano mkubwa na hoja hii. Utafiti wa Alago et al. (2024) unaeleza umuhimu wa suluhisho zinazotokana na asili katika kukabiliana na uharibifu wa ardhi katika maeneo ya savanna za Afrika Mashariki. Utafiti huo unaonesha kuwa mbinu kama urejeshaji wa uoto, uhifadhi wa udongo na usimamizi endelevu wa ardhi zinaweza kusaidia kupunguza mmomonyoko wa udongo na kurejesha afya ya mifumo ya ikolojia. Hivyo, unalingana na nukuu kwa sababu matuta na nyasi kingo ni mifano ya suluhisho za asili zinazolenga kulinda udongo, kuhifadhi virutubisho na kuboresha uzalishaji wa kilimo. Kwa upande mwingine, ripoti ya Farm Radio International (2024) kuhusu *Shamba Shape-Up* Series 14 KAP Report (Kenya) inaonesha nafasi ya vyombo vya habari katika kutoa elimu ya kilimo na kuhamasisha wakulima kutumia mbinu bora za uzalishaji. Kupitia programu kama *Shamba Shape-Up,* wakulima hupata taarifa kuhusu uhifadhi wa udongo, kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi na matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira. Ripoti hiyo inaonyesha kuwa mawasiliano ya kilimo yanaweza kuchochea wakulima kubadili tabia na kutumia mbinu endelevu katika mashamba yao. Kwa hivyo, tafiti hizi mbili zinaunga mkono nukuu kwa kuonyesha kuwa udhibiti wa mmomonyoko

wa udongo hauhitaji tu mbinu za kitaalamu kama matuta na upandaji wa nyasi kingo, bali pia elimu na ushiriki wa jamii. Alago et al. wanaangazia upande wa uhifadhi wa mazingira na urejeshaji wa mifumo ya ikolojia, wakati Farm Radio International inaonyesha kuwa vyombo vya habari vinaweza kusaidia kusambaza maarifa hayo kwa wakulima ili wayatumie kwa vitendo.

https://shambashapeup.com/kenya-series/series-15/?

4.2.2 Changamoto za Ukame na Uhaba wa Maji

Ukame na uhaba wa maji ni hali inayotokea pale ambapo eneo linapokea mvua kidogo sana kwa muda mrefu au mvua kukosekana kabisa, hali inayosababisha upungufu mkubwa wa maji katika mito, mabwawa, visima na udongo. Ukame unaweza kusababishwa na mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira kama ukataji miti, na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za maji. Matokeo yake ni kukauka kwa vyanzo vya maji, kupungua kwa uzalishaji wa kilimo na mifugo, na kuongezeka kwa uhaba wa chakula. Aidha, uhaba wa maji huathiri afya ya binadamu kwa kuongeza hatari ya magonjwa yanayotokana na maji machafu na pia huongeza migogoro kati ya jamii zinazoshindania rasilimali chache za maji. Hivyo, ukame na uhaba wa maji ni changamoto kubwa za kimazingira na kijamii zinazohitaji mikakati ya uhifadhi wa maji, upandaji

M-06-V-SSU

Mfano mwafaka wa mada hii ni *Shamba Shape-Up* Series 16, Episode 10: Tiller, Tomatoes and Dairy Parasite Control Tiller, kwa mkulima Philip Mwaura Kimana, Kajiado County.

> *"Ukame na uhaba wa maji ni changamoto kubwa kwa wakulima, hivyo matumizi bora ya maji ni muhimu katika kuhakikisha uzalishaji wa mazao unaendelea."*

Ujumbe huu unaibua uhusiano wa karibu kati ya uhaba wa maji na uzalishaji wa kilimo. Katika Series 16 Episode 10, changamoto ya uhaba wa maji inaonekana katika mazingira halisi ya mkulima anayezalisha nyanya na capsicum huko Kimana, Kajiado County. Hali hii inaonyesha kuwa mabadiliko katika upatikanaji wa rasilimali za maji yanaweza kuwa na athari katika shughuli za uzalishaji wa chakula. Kwa hivyo, kuwasilishwa kwa changamoto hii kupitia kipindi cha *Shamba Shape-Up* kunaongeza uelewa wa hadhira kuhusu umuhimu wa rasilimali za maji katika kilimo na haja ya kuzingatia matumizi endelevu ya rasilimali hizo.

Kwa mtazamo wa Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia**,** hoja ya ukame na uhaba wa maji inaonesha utegemeano mkubwa kati ya binadamu na mazingira, hususan katika shughuli za kilimo zinazotegemea upatikanaji wa maji. Uwasilishaji wa changamoto hii katika *Shamba Shape-Up* unaonesha kwamba mabadiliko katika upatikanaji wa rasilimali za maji hayaathiri mazingira pekee, bali pia uzalishaji wa chakula, kipato na ustawi wa jamii za wakulima. Kwa mujibu wa Glotfelty (1996), Uhakiki-Ikolojia huchunguza uhusiano kati ya binadamu na ulimwengu wa kimaumbile, hivyo hoja hii inadhihirisha namna maisha ya binadamu yanavyofungamana na afya na upatikanaji wa rasilimali za asili. Aidha, msisitizo wa matumizi bora na endelevu ya maji unaibua umuhimu wa kuwa na mtazamo wa uwajibikaji katika matumizi ya mazingira, kwa kuwa matumizi yasiyozingatia uendelevu yanaweza kuongeza shinikizo kwa rasilimali chache za maji. Hivyo, *Shamba Shape-Up* haitoi tu taarifa kuhusu changamoto ya ukame, bali pia inajenga uelewa wa hadhira kuhusu umuhimu wa kulinda rasilimali za maji kama msingi wa uhifadhi wa mazingira, usalama wa chakula na uzalishaji endelevu wa kilimo**.**

Matokeo haya yanaungwa mkono na Bryan et al ambao wanaonesha kuwa mabadiliko ya tabianchi na kutotabirika kwa hali ya hewa huathiri uzalishaji na maisha ya wakulima, hivyo kuhitaji mikakati ya kukabiliana nayo, ikiwemo umwagiliaji pamoja na uhifadhi wa udongo na maji. Aidha, utafiti wa Bryan et al. (2024) unaonesha kuwa ukame huathiri matumizi na usimamizi wa maji ya umwagiliaji, jambo linaloonesha umuhimu wa kufanya maamuzi bora kuhusu matumizi ya maji katika mazingira yenye uhaba wa rasilimali hiyo. Matokeo haya yanafanana na ujumbe unaowasilishwa katika *Shamba Shape-Up*, unaosisitiza kuwa ukame na uhaba wa maji ni changamoto kwa wakulima na kwamba matumizi bora ya maji ni muhimu katika kuendeleza uzalishaji wa mazao. Hata hivyo, tofauti kuu ni kwamba tafiti zilizotangulia zinachunguza zaidi athari za ukame na mikakati ya kukabiliana nao katika mifumo ya kilimo, wakati utafiti huu unachunguza namna runinga inavyowasilisha changamoto hiyo na kuelimisha wakulima kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za maji**.** Hivyo, utafiti huu unaongeza uelewa kuhusu nafasi ya vyombo vya habari katika kuwasilisha maarifa ya kukabiliana na changamoto za kimazingira katika jamii.

> *https://shambashapeup.com/kenya-series/ssu-16/ep-10-tiller-tomatoes-and-dairy-parasite-control/?*

4.2.3 Changamoto za Kupungua kwa Rutuba ya Udongo

Kupungua kwa rutuba ya udongo ni hali inayotokea pale ambapo udongo unapoteza uwezo wake wa kusaidia ukuaji bora wa mimea kutokana na kupungua kwa virutubisho muhimu, pamoja na kupungua kwa viumbe hai vya udongo vinavyosaidia katika mzunguko wa virutubisho. Hali hii husababishwa na mambo mbalimbali ikiwemo mmomonyoko wa udongo unaoondoa tabaka la juu lenye rutuba, kilimo cha muda mrefu bila kuongeza mbolea au virutubisho, ukataji miti unaosababisha upotevu wa mboji, na mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri muundo wa udongo. Matokeo yake ni kushuka kwa uzalishaji wa mazao, mimea kudumaa, na kuongezeka kwa utegemezi wa mbolea za viwandani ili kufidia upungufu huo. Aidha, rutuba inapopungua, uwezo wa udongo kuhifadhi maji na kusaidia mfumo wa ikolojia hupungua pia, jambo linaloongeza hatari ya kuharibika kwa ardhi na kupungua kwa usalama wa chakula. Hivyo basi, kupungua kwa rutuba ya udongo ni changamoto kubwa ya kiikolojia inayohitaji mikakati endelevu kama kilimo hifadhi, matumizi ya mboji, mzunguko wa mazao na upandaji miti ili kurejesha afya ya udongo.

M-07-V-SSU

Kwa mfano: *Shamba Shape-Up* series 16-episode 3 conservation agriculture 23 mechi 2026 kutoka kwa youtube.

> "*Kilimo hifadhi ni njia ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuongeza uzalishaji wa mazao kupitia mbinu kama kulima kwa kiwango kidogo, kilimo mseto, mzunguko wa mazao na kilimo cha mistari.*"

D**o**ndoo hii inaonesha kuwa matumizi ya mbolea za asili ni mkakati muhimu wa kurejesha na kudumisha afya ya udongo**,** kwa sababu samadi, mboji na mabaki ya mimea huongeza virutubisho na mabaki ya kikaboni yanayosaidia kuboresha muundo wa udongo, uwezo wa kuhifadhi maji na shughuli za viumbe hai. Ushahidi wa utafiti wa Kenya unaonesha pia kwamba matumizi ya samadi na uhifadhi wa mabaki ya mazao yanaweza kuboresha viashiria vya afya ya udongo na rutuba yake. Kwa hiyo, mbolea za asili hazipaswi kuchukuliwa kama pembejeo za kuongeza mavuno pekee, bali kama mkakati wa muda mrefu wa kurejesha virutubisho vinavyopotea, kupunguza uharibifu wa udongo na kuimarisha uzalishaji endelevu wa kilimo**.** Hata hivyo, matumizi yake yanahitaji usimamizi sahihi kwa sababu kiasi na ubora wa samadi au

mboji vinatofautiana, na katika baadhi ya mazingira yanaweza yasitosheleze mahitaji yote ya virutubisho vya mazao.

Hoja hii inaonyesha umuhimu wa mbinu endelevu za kilimo katika kulinda mazingira na kuimarisha uzalishaji wa chakula. Matumizi ya mbolea ya asili ni njia bora ya kupunguza utegemezi wa mbolea za kemikali ambazo zinaweza kusababisha uchafuzi wa mazingira na kudhoofisha ubora wa udongo endapo zitatumika kupita kiasi. Aidha, mbolea za asili huchangia katika kuhifadhi rutuba ya udongo kwa muda mrefu, kupunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima, na kuimarisha usalama wa chakula kwa kuongeza mavuno kwa njia rafiki kwa mazingira.

Nukuu hii ina uhusiano mkubwa na nadharia ya uhakiki ikolojia kwa kuwa inasisitiza matumizi ya rasilimali za mazingira kwa namna inayodumisha uwiano wa mfumo wa ikolojia. Nadharia ya uhakiki ikolojia huangazia umuhimu wa binadamu kuishi kwa maelewano na mazingira badala ya kuyatumia kwa njia zinazoweza kuyaharibu. Matumizi ya mbolea ya asili yanaonyesha mtazamo wa kuhifadhi afya ya udongo na viumbe hai wanaouzunguka, huku yakikuza uzalishaji wa mazao kwa njia endelevu. Hivyo, nukuu hii inaunga mkono hoja ya uhakiki ikolojia kwamba maendeleo ya binadamu yanapaswa kuzingatia ulinzi wa mazingira na matumizi bora ya rasilimali za asili ili kuhakikisha manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo.

Utafiti wa Bryan et al (2024) unaafikiana na nukuu hii kwa kusisitiza kuwa matumizi ya mbinu endelevu za usimamizi wa udongo, ikiwemo mbolea za asili, ni muhimu katika kuongeza uzalishaji wa mazao na kuhifadhi rutuba ya udongo kwa muda mrefu. Watafiti hawa wanaonyesha kwamba wakulima wanaotumia mbolea za asili hupata manufaa si tu katika ongezeko la mavuno bali pia katika kuboresha muundo wa udongo, kuhifadhi unyevunyevu na kuongeza ustahimilivu wa kilimo dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi. Hoja hii inalingana na nukuu inayobainisha kuwa mbolea za asili hurejesha rutuba ya udongo na kuimarisha uzalishaji wa mazao. Tofauti ndogo ni kwamba nukuu inalenga zaidi faida za moja kwa moja za mbolea za asili katika uzalishaji wa mazao, ilhali Bryan et al wanaipanua hoja hiyo kwa kuonyesha mchango wake katika uendelevu wa mazingira na usalama wa chakula kwa muda mrefu. Hivyo, utafiti huu unathibitisha kuwa matumizi ya mbolea za asili si tu mbinu ya kuongeza mavuno bali pia ni mkakati muhimu wa kuhifadhi mfumo wa ikolojia wa udongo, jambo linaloendana na nadharia ya uhakiki ikolojia inayosisitiza matumizi ya rasilimali za mazingira kwa njia inayodumisha uwiano kati ya binadamu na mazingira.

Video ya kipindi hiki inapatikana kwa Shamba Shape-Up Series
https://www.youtube.com/watch?v=7uUSVOylT-U

M-5-V-CP

Vile vile kuna mfano wa: Smart Farm: Farmers adopt climate-smart practices to tackle drought and crop losses na mwandishi ni Denis Otieno tarehe 01 Aprili 10:24pm Machakos County, Kenya kwenye YouTube ya Runinga ya Citizen 2026.

> "*Wakulima wanazidi kugeukia kilimo kinachozingatia hali ya hewa ili kukabiliana na hali ya hewa isiyotabirika na kupungua kwa rutuba ya udongo."*

Nukuu hii inaeleza kuwa kutokana na kuongezeka kwa changamoto za mabadiliko ya tabianchi, kama vile ukame wa mara kwa mara, mvua zisizotabirika, mafuriko na kupungua kwa rutuba ya udongo, wakulima wengi wanatumia mbinu za kilimo kinachozingatia hali ya hewa ili kuendelea kuzalisha mazao kwa ufanisi. Mbinu hizi zinajumuisha matumizi ya mbegu zinazostahimili ukame, uhifadhi wa maji, upandaji miti mashambani, matumizi ya mbolea za asili, mzunguko wa mazao na mbinu nyingine zinazosaidia kuongeza uzalishaji huku zikihifadhi mazingira. Hivyo, kilimo kinachozingatia hali ya hewa ni mkakati wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha usalama wa chakula.

Kauli hii inaonyesha uwezo wa wakulima kubadilika kulingana na changamoto za mazingira zinazozidi kujitokeza duniani. Kilimo kinachozingatia hali ya hewa ni suluhisho muhimu kwa sababu kinaongeza ustahimilivu wa sekta ya kilimo dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi huku kikihifadhi rasilimali za asili. Aidha, mbinu hizi husaidia kupunguza uharibifu wa mazingira, kuboresha afya ya udongo na kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao kwa muda mrefu. Kwa hiyo, kuhamasisha matumizi ya mbinu hizi ni hatua muhimu katika kufanikisha maendeleo endelevu na usalama wa chakula.

Nukuu hii ina uhusiano mkubwa na nadharia ya uhakiki ikolojia kwa kuwa inasisitiza umuhimu wa kuoanisha shughuli za binadamu na mahitaji ya mazingira. Nadharia ya uhakiki ikolojia huangalia namna binadamu wanavyohusiana na mazingira yao na umuhimu wa kuyatumia kwa njia endelevu. Kilimo kinachozingatia hali ya hewa kinaonyesha juhudi za binadamu za kuendana na mabadiliko ya mazingira badala ya kuyapuuza au kuyaharibu. Kupitia mbinu zinazohifadhi rutuba ya udongo, maji na bioanuwai, wakulima wanachangia kudumisha uwiano wa ikolojia huku wakihakikisha uzalishaji wa chakula unaendelea. Hivyo, nukuu hii inaakisi

msingi wa nadharia ya uhakiki ikolojia unaosisitiza kuwa maendeleo ya binadamu yanapaswa kwenda sambamba na uhifadhi wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za asili.

Utafiti wa Bryan et al (2024) unaunga mkono nukuu inayosema kuwa kwa kuonyesha kuwa mabadiliko ya tabianchi yameleta changamoto kubwa katika mifumo ya kilimo, hivyo kuhitaji wakulima kutumia mbinu zinazoongeza ustahimilivu wa uzalishaji. Watafiti hawa wanaeleza kuwa matumizi ya teknolojia na mbinu za kilimo kinachozingatia hali ya hewa, kama uhifadhi wa maji, matumizi ya mbolea za asili, kilimo mseto na usimamizi bora wa udongo, husaidia kurejesha afya ya udongo, kuongeza mavuno na kupunguza utegemezi wa rasilimali zinazoweza kuharibu mazingira. Hivyo, nukuu na utafiti huu vinafanana kwa kutambua kuwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kunahitaji mabadiliko ya mbinu za kilimo kutoka kwenye uzalishaji usio endelevu kwenda kwenye mifumo inayolinda mazingira. Tofauti ni kwamba nukuu inaeleza hali ya wakulima kwa ujumla, wakati Bryan, Ringler na Okoba wanaweka hoja hiyo katika msingi wa utafiti unaoonyesha umuhimu wa kilimo kinachozingatia hali ya hewa katika kujenga ustahimilivu wa jamii na kuhakikisha usalama wa chakula.

> *Video inayolingana ni Citizen Planet – Smart Farm / Climate-Smart Agriculture (2026) https://www.kenyamoja.com/video/smart-farm-farmers-adopt-climate-smart-practices-tackle-drought-and-crop-losses-citizen-tv?utm*

4.2.4 Changamoto za Mabadiliko ya Tabianchi

Mabadiliko ya tabianchi ni mabadiliko ya muda mrefu katika hali ya hewa ya dunia yanayosababishwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za binadamu kama vile ukataji miti, matumizi ya mafuta ya kisukuku, na uzalishaji wa gesi chafuzi. Mabadiliko haya husababisha ongezeko la joto duniani, ukame wa mara kwa mara, mafuriko, kuyeyuka kwa barafu, na mabadiliko ya mifumo ya mvua. Athari zake huathiri kilimo, afya ya binadamu, upatikanaji wa maji, na mazingira kwa ujumla. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuchukua hatua za kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti, kutumia nishati safi, na kupunguza uchafuzi wa hewa ili kukabiliana na changamoto hii.

M-06-V-CP

Kwa mfano: Kipindi *Citizen Planet*, Samburu's rotational grazing revolution, defying climate chaos 26 oktoba 2026 saa 9:56 usiku dakika 8.04 Samburu County, Kenya Youtube

"Malisho ya mzunguko huipa ardhi muda wa kurejea katika hali yake, huwezesha nyasi kuchipua upya na kusaidia kulinda udongo dhidi ya mmomonyoko."

Nukuu hii inaeleza kuwa malisho ya mzunguko huipa ardhi muda wa kurejea, huwezesha nyasi kuchipua upya na kulinda udongo dhidi ya mmomonyoko. Mfano wa jamii za Samburu unaonesha kuwa mabadiliko katika usimamizi wa malisho yanaweza kuwa mkakati muhimu wa kukabiliana na ukame na athari za mabadiliko ya tabianchi, kwa kuwa kubadilisha maeneo ya kuchungia kwa vipindi maalumu hupunguza shinikizo la mifugo kwenye ardhi na kuruhusu uoto wa asili kujirejesha. Kwa hivyo, hatua hii haifaidi mifugo pekee, bali pia inalinda afya ya udongo, inapunguza uharibifu wa ardhi na kuhifadhi bioanuai ya maeneo ya malisho**.** Aidha, matumizi ya maarifa ya jadi pamoja na mbinu za kisasa yanaonesha umuhimu wa kuhusisha jamii katika usimamizi wa rasilimali za mazingira kwa sababu jamii ndiyo yenye uhusiano wa moja kwa moja na ardhi na mifugo. Hivyo, *Citizen Planet* kupitia maudhui haya inaonesha uhifadhi wa mazingira kama mchakato unaounganisha ustawi wa jamii, uzalishaji wa mifugo na uendelevu wa mifumo ya ikolojia, badala ya kuutazama uhifadhi kama jukumu la taasisi pekee.

Kauli hii inaonyesha kuwa mabadiliko ya tabianchi yamelazimisha jamii zinazotegemea ufugaji kutafuta njia mpya za kuendeleza maisha yao. Usimamizi bora wa malisho ni muhimu kwa sababu ukame unapoongezeka, utegemezi wa mifugo bila mipango madhubuti unaweza kusababisha kupungua kwa mimea, mmomonyoko wa udongo na migogoro ya rasilimali. Hivyo, matumizi ya mbinu bunifu za kuhifadhi malisho na maji yanaweza kuongeza uwezo wa jamii kustahimili ukame, kulinda mazingira na kuimarisha uchumi wa wafugaji. Aidha, ushirikishwaji wa jamii katika maamuzi kuhusu matumizi ya ardhi ni muhimu ili kuhakikisha mikakati hiyo inakuwa endelevu.

Nukuu hii ina uhusiano mkubwa na nadharia ya uhakiki ikolojia kwa kuwa inaangazia mwingiliano kati ya binadamu, mifugo na mazingira. Nadharia ya uhakiki ikolojia husisitiza kuwa shughuli za binadamu zinapaswa kuzingatia uwezo wa mazingira kujirekebisha ili kuepuka uharibifu wa mfumo wa ikolojia. Katika muktadha huu, usimamizi wa malisho unaonyesha juhudi za jamii kutumia rasilimali za asili kwa uangalifu badala ya kuzimaliza. Jamii za Samburu zinapoimarisha uhifadhi wa malisho, maji na ardhi, zinaonyesha namna binadamu anavyoweza kuishi kwa uwiano na mazingira huku akiendelea kukidhi mahitaji yake ya kijamii na kiuchumi. Hivyo, nukuu inaunga mkono msingi wa uhakiki ikolojia kwamba suluhisho la changamoto za mazingira linahitaji uwajibikaji wa binadamu katika matumizi ya rasilimali za asili.

Kauli hii inaungwa mkono na Utafiti wa Potts et al. (2024) kuhusu *"Global Biodiversity Threats & Protected Areas Expansion (30x30 Agenda)"* Utafiti wa Potts na wenzake unaonyesha umuhimu wa kulinda bioanuwai na kupanua maeneo yanayohifadhiwa ili kupunguza vitisho vinavyosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa makazi ya viumbe na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za asili. Hoja hii inafanana na nukuu kwa kuwa zote zinasisitiza umuhimu wa usimamizi bora wa mazingira kama njia ya kukabiliana na changamoto za ikolojia. Nukuu inalenga zaidi usimamizi wa malisho katika jamii za wafugaji ili kuhifadhi ardhi, maji na mimea inayotegemewa na mifugo, wakati utafiti wa Potts et al. unaangazia kwa upana zaidi uhifadhi wa mifumo ya ikolojia na ulinzi wa viumbe hai kupitia upanuzi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Hivyo, tafiti zote zinaonyesha kuwa matumizi endelevu ya ardhi na ushirikishwaji wa jamii ni muhimu katika kujenga ustahimilivu wa mazingira na kuhakikisha rasilimali za asili zinadumu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

> *Video ya kipindi hiki inapatikana kwenye Citizen Planet | Samburu's rotational grazing revolution, defying climate chaos*

4.2.5 Changamoto za Kupotea kwa Bioanuwai

Kupotea kwa bioanuwai ni hali ya kupungua au kutoweka kwa aina mbalimbali za viumbe hai kama mimea, wanyama na viumbe vidogo katika mazingira fulani au duniani kwa ujumla. Hali hii husababishwa na shughuli za binadamu kama ukataji miti ovyo, uchafuzi wa mazingira, mabadiliko ya tabianchi, matumizi mabaya ya ardhi na ujangili. Bioanuwai inapopotea, mifumo ya ikolojia hudhoofika kwa sababu kila kiumbe kina nafasi yake katika kulinda uwiano wa mazingira, kama vile uchavushaji wa mimea, udhibiti wa wadudu na uimarishaji wa rutuba ya udongo. Matokeo yake ni kupungua kwa uzalishaji wa chakula, kuongezeka kwa majanga ya mazingira na kuvurugika kwa mzunguko wa asili wa maisha. Hivyo, kulinda bioanuwai ni muhimu kwa ustawi wa mazingira na maisha ya binadamu kwa ujumla.

M-08-V-SSU

Mfano mwingine ni *Shamba Shape-Up* – Series 15, Episode 22: "Polyculture, Crab Shack Maeneo ya pwani ya Kenya tarehe 6 Septemba 2025

> *"Ufugaji wa nyuki na uchavushaji husaidia wakulima kuongeza mavuno ya mazao na kulinda mazingira kupitia mbinu za kilimo endelevu."*

Nukuu hii inaeleza kuwa ufugaji wa nyuki na mchakato wa uchavushaji una mchango mkubwa katika kuboresha uzalishaji wa kilimo na kuhifadhi mazingira. Nyuki husaidia kuhamisha chavua kutoka ua moja hadi jingine, jambo linalowezesha mimea kutengeneza matunda na mbegu kwa ufanisi zaidi. Kupitia uchavushaji mzuri, wakulima wanaweza kupata mavuno mengi na yenye ubora zaidi. Aidha, ufugaji wa nyuki huchochea uhifadhi wa mimea na maua kwa sababu nyuki huhitaji mazingira yenye mimea hai ili kuishi. Hivyo, ufugaji wa nyuki unakuwa njia ya kuongeza kipato cha wakulima huku ukichangia uhifadhi wa bioanuwai na matumizi endelevu ya mazingira.

Kauli hii inaonyesha kuwa shughuli za kilimo zinaweza kuunganishwa na uhifadhi wa mazingira ili kupata manufaa ya kiuchumi na kiikolojia kwa wakati mmoja. Ufugaji wa nyuki ni mbinu endelevu kwa sababu hauhitaji uharibifu mkubwa wa mazingira bali unategemea uwepo wa mifumo hai ya asili kama misitu, mimea na maua. Pia, ufugaji wa nyuki unaweza kusaidia wakulima kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi kwa kuongeza vyanzo vya kipato na kuhamasisha uhifadhi wa maeneo yenye mimea. Kwa hiyo, kuendeleza ufugaji wa nyuki ni mkakati unaoweza kuimarisha uzalishaji wa chakula na kulinda rasilimali za asili.

Nukuu hii ina uhusiano mkubwa na nadharia ya uhakiki ikolojia kwa kuwa inaonyesha utegemeano kati ya binadamu na viumbe wengine katika mfumo wa mazingira. Nadharia ya uhakiki ikolojia husisitiza kwamba binadamu hawezi kutenganishwa na asili kwa sababu maisha yake yanategemea mahusiano ya kiikolojia. Katika muktadha huu, nyuki wanaonekana kuwa sehemu muhimu ya mfumo wa ikolojia unaosaidia uzalishaji wa chakula na kudumisha bioanuwai. Ufugaji wa nyuki unaonyesha namna jamii inaweza kutumia rasilimali za asili kwa njia inayolinda mazingira badala ya kuyaharibu. Hivyo, nukuu inaunga mkono mtazamo wa uhakiki ikolojia kwamba maendeleo ya kilimo yanapaswa kuzingatia uhifadhi wa viumbe hai na uwiano wa mazingira.

Hoja hii inalingana na utafiti wa ***"****Environmental Conservation Strategies in Secondary Schools: UNEP Alignment Study"*. Utafiti huu unaonyesha umuhimu wa kuimarisha elimu na mikakati ya uhifadhi wa mazingira katika shule ili kujenga uelewa wa jamii kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za asili. Hoja hii inaendana na nukuu kwa kuwa zote zinasisitiza umuhimu wa kulinda mazingira kupitia vitendo vinavyosaidia kudumisha mifumo ya ikolojia. Nukuu inalenga zaidi mchango wa nyuki katika uzalishaji wa kilimo, uchavushaji na uhifadhi wa bioanuwai, wakati utafiti wa UNEP unaangazia nafasi ya elimu ya mazingira na mikakati ya uhifadhi katika

kuwajengea wanafunzi na jamii uwezo wa kushiriki katika kulinda mazingira. Hivyo, tafiti zote zinaonyesha kuwa uhifadhi wa mazingira unahitaji maarifa, ushiriki wa jamii na matumizi ya mbinu endelevu zinazolinda viumbe hai na rasilimali za asili. Kwa ujumla, ufugaji wa nyuki unaweza kuchukuliwa kama mfano wa vitendo wa elimu ya uhifadhi inayolenga kuunganisha uzalishaji wa chakula na ulinzi wa mazingira.

> *Video ya kipindi hiki inapatikana kwa Shamba Shape-Up – https://shambashapeup.com/kenya-series/series-15/?*

M-07-V-CP

Mfano mwingine ni: *Citizen Planet* Drones deployed to curb Kajiado elephant menace 31 Agosti 2025 Kajiado County, Kenya Runinga ya Citizen Kenya – YouTube.

> *"Katika maeneo ya Kajiado, migongano kati ya binadamu na tembo imeongezeka kutokana na mabadiliko ya tabianchi, hivyo droni zinatumika kama njia salama ya kuwaondoa tembo mashambani na kulinda mazao pamoja na wanyamapori."*

Nukuu hii inaeleza kuwa mabadiliko ya tabianchi yamechangia kuongezeka kwa migongano kati ya binadamu na wanyamapori, hasa tembo katika maeneo ya Kajiado. Ukame na kupungua kwa vyanzo vya maji na malisho huwafanya tembo kusogea karibu na makazi ya watu na mashamba wakitafuta chakula na maji, hali inayosababisha uharibifu wa mazao na tishio kwa usalama wa jamii. Matumizi ya droni yanaonekana kuwa mbinu ya kisasa ya kudhibiti migongano hiyo kwa kuwafuatilia tembo na kuwaelekeza mbali na maeneo ya kilimo bila kuwadhuru. Kwa njia hii, teknolojia inatumika kusaidia kulinda maisha ya watu, uzalishaji wa chakula na uhifadhi wa wanyamapori.

Kauli hii inaonyesha umuhimu wa kutumia ubunifu wa kiteknolojia katika kutatua changamoto zinazotokana na mabadiliko ya mazingira. Matumizi ya droni yanaweza kuwa suluhisho lenye manufaa kwa sababu yanapunguza matumizi ya mbinu hatarishi kama kuwadhuru au kuwaua wanyama wanaovamia mashamba. Hata hivyo, teknolojia pekee haitoshi; ni muhimu pia kushughulikia sababu kuu za migongano hiyo, kama uharibifu wa makazi ya wanyamapori, upungufu wa maji na mabadiliko ya matumizi ya ardhi. Ushirikiano kati ya jamii, wataalamu wa uhifadhi na taasisi za mazingira ni muhimu ili kupata suluhisho la kudumu.

Nukuu hii ina uhusiano mkubwa na nadharia ya uhakiki ikolojia kwa kuwa inachunguza uhusiano kati ya binadamu, wanyamapori na mazingira yanayowazunguka. Nadharia ya uhakiki ikolojia husisitiza kuwa migogoro ya mazingira mara nyingi hutokana na kuvurugika kwa uwiano kati ya shughuli za binadamu na mifumo ya asili. Katika hali hii, ongezeko la migongano kati ya tembo na binadamu linaonyesha namna mabadiliko ya tabianchi yanavyoathiri mahusiano ya viumbe ndani ya mfumo wa ikolojia. Matumizi ya droni yanaonyesha jitihada za kutafuta njia ya kuishi kwa pamoja kati ya binadamu na wanyamapori bila kuharibu mazingira. Hivyo, nukuu inaunga mkono wazo la uhakiki ikolojia kwamba suluhisho la changamoto za mazingira linahitaji kuheshimu mahusiano ya viumbe vyote na kudumisha uwiano wa mfumo wa ikolojia.

Hoja hii inaungwa mkono na utafiti wa Olago et al. (2024) kuhusu "*Nature-Based Solutions to Land Degradation in East African Savannahs*". Utafiti wa Olago na wenzake unaonyesha kuwa suluhisho zinazotegemea mazingira ni muhimu katika kukabiliana na uharibifu wa ardhi, mabadiliko ya tabianchi na changamoto zinazotokea katika mifumo ya savanna za Afrika Mashariki. Watafiti wanaeleza kuwa mbinu kama urejeshaji wa ardhi, usimamizi endelevu wa malisho, uhifadhi wa mimea na ushirikishwaji wa jamii zinaweza kusaidia kurejesha afya ya mazingira na kupunguza migogoro inayotokana na ushindani wa rasilimali. Nukuu na utafiti huu vinafanana kwa kusisitiza umuhimu wa kutumia mbinu bunifu na rafiki kwa mazingira katika kutatua changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Nukuu inalenga zaidi matumizi ya teknolojia ya droni kudhibiti migogoro kati ya binadamu na tembo kwa kulinda mazao na wanyamapori bila kuleta madhara kwa viumbe hai, wakati utafiti wa Olago et al. unaangazia zaidi matumizi ya suluhisho za asili katika kurejesha ardhi iliyoharibika na kuboresha uhusiano kati ya jamii na mazingira. Hivyo, tafiti zote zinaonyesha kuwa changamoto za mazingira zinahitaji mikakati inayounganisha maendeleo ya binadamu, matumizi ya teknolojia na uhifadhi wa mifumo ya ikolojia ili kuhakikisha maisha ya jamii na wanyamapori yanaendelea kuwepo kwa uwiano.

> *Video ya kipindi hiki inapatikana kwa Citizen Planet: Drones deployed to curb Kajiado elephant menace*

4.2.6 Changamoto za Kuongezeka kwa Uchafuzi wa Mazingira

Kuongezeka kwa uchafuzi wa mazingira ni hali ya ongezeko la vitu hatarishi kama taka ngumu, moshi wa viwandani, gesi za magari, kemikali na plastiki zinazoingia kwenye hewa, maji na

ardhi kwa kiwango kinachodhuru viumbe hai na mifumo ya ikolojia. Hali hii husababishwa na shughuli za binadamu kama ukuaji wa viwanda, ongezeko la idadi ya watu, matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali, na utupaji holela wa taka. Athari zake ni pamoja na magonjwa ya mfumo wa hewa kama pumu, uchafuzi wa vyanzo vya maji, vifo vya viumbe wa majini, uharibifu wa udongo, na kuchochea mabadiliko ya tabianchi kupitia gesi chafuzi. Hivyo, kuongezeka kwa uchafuzi wa mazingira ni changamoto kubwa inayohitaji hatua za haraka kama udhibiti wa taka, matumizi ya nishati safi na elimu ya mazingira ili kulinda afya ya binadamu na uendelevu wa mazingira.

M-08-V-CP

Citizen Planet Lake Nkunga pollution a ticking time bomb for Meru 14 septemba 2025 Nkunga, Meru County Runinga ya Citizen Kenya – YouTube

> *"Kwa miaka mingi, wakazi wa Nkunga wamekuwa wakikumbwa na athari za utupaji holela wa taka unaosababisha harufu kali, uchafuzi wa hewa na maji, huku taka zinazooza zikitoa gesi ya methane ambayo huchangia ongezeko la mabadiliko ya tabianchi na kuhatarisha afya ya jamii."*

Nukuu hii inaeleza athari za utupaji holela wa taka katika eneo la Nkunga na namna hali hiyo inavyoathiri mazingira pamoja na afya ya jamii. Taka zinapotupwa bila mpangilio, hasa zile zinazooza kama mabaki ya chakula na mimea, huanza kuoza na kutoa harufu mbaya, kuchafua hewa na kuathiri ubora wa vyanzo vya maji. Wakati wa kuoza, taka hizi hutoa gesi ya methane ambayo ni gesi chafu inayochangia ongezeko la joto duniani na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo, tatizo la taka si suala la usafi pekee bali ni changamoto ya kimazingira, kiafya na kijamii inayohitaji usimamizi bora wa taka.

Kauli hii inaonyesha umuhimu wa kuwa na mifumo madhubuti ya usimamizi wa taka ili kulinda afya ya jamii na mazingira. Utupaji holela wa taka unatokana na ukosefu wa elimu ya mazingira, miundombinu duni ya ukusanyaji taka na kutokuwepo kwa mikakati endelevu ya urejeleaji wa taka. Kwa hiyo, jamii inapaswa kuhamasishwa kuhusu upangaji wa taka, urejeleaji na matumizi ya teknolojia kama uzalishaji wa mbolea kutoka taka zinazooza ili kupunguza uchafuzi na

uzalishaji wa gesi chafu. Hatua hizi zinaweza kusaidia kuboresha mazingira, kupunguza magonjwa na kuchangia katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Nukuu hii ina uhusiano mkubwa na nadharia ya uhakiki ikolojia kwa kuwa inaonyesha athari za matendo ya binadamu kwa mazingira na namna uharibifu wa mazingira unavyorudi kuathiri maisha ya binadamu. Nadharia ya uhakiki ikolojia husisitiza kuwa binadamu ni sehemu ya mfumo wa ikolojia na kwamba matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali yanaweza kuvuruga uwiano wa mazingira. Katika hali hii, utupaji holela wa taka unaonyesha jinsi shughuli za binadamu zinavyoweza kuharibu hewa, maji na afya ya viumbe hai. Kwa hiyo, nadharia hii inasisitiza umuhimu wa kubadili mitazamo na tabia za jamii ili kuweka uwiano kati ya mahitaji ya binadamu na uhifadhi wa mazingira kwa maendeleo endelevu.

Hoja hii inakaribiana sana utafiti wa Rasowo et al (2024) kuhusu "*Decarbonization and Blue Economy Sustainability in Kenya"* Utafiti wa Rasowo et al unaonyesha umuhimu wa kupunguza uzalishaji wa gesi chafu na kutumia rasilimali za mazingira kwa njia endelevu kupitia mikakati ya kupunguza kaboni na maendeleo endelevu ya rasilimali za majini. Tafiti hizi zinafanana kwa kuwa zote zinahusu athari za shughuli za binadamu kwa mazingira na hitaji la kubadili mifumo ya matumizi ya rasilimali ili kupunguza madhara ya mabadiliko ya tabianchi. Utafiti wa uchumi endelevu wa bahari unaeleza kuwa uhifadhi wa mifumo ya ikolojia kama mikoko, matumizi ya nishati safi na miradi ya kupunguza kaboni husaidia kulinda mazingira huku ikiimarisha maisha ya jamii. Kwa upande mwingine, nukuu inalenga zaidi tatizo la usimamizi wa taka katika jamii na athari zake kwa afya ya binadamu, hewa na maji, wakati utafiti wa Rasowo et al unaangazia suluhisho pana zaidi za kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia matumizi endelevu ya rasilimali na teknolojia rafiki kwa mazingira. Hata hivyo, zote zinaonyesha kuwa uchafuzi wa mazingira na uzalishaji wa gesi chafu hauwezi kutatuliwa bila kuwepo kwa mifumo bora ya usimamizi wa mazingira. Kwa hiyo, usimamizi sahihi wa taka, urejeleaji na matumizi ya teknolojia safi vinaweza kuchukuliwa kama sehemu ya mikakati ya kupunguza kaboni na kujenga jamii yenye mazingira salama na endelevu.

Video ya Citizen Planet inapatikana katika kipindi cha "Lake Nkunga pollution a ticking time bomb for Meru"

M-09-V-SSU

Kwa mfano: *Citizen Planet* Scientists alarmed as pollution rises in Lake Victoria tarehe 11 Januari 2026 chanzo ni Runinga ya Citizen Kenya – YouTube

> "*Kuongezeka kwa uchafuzi katika Ziwa Victoria kunatishia afya ya mfumo wa ikolojia wa ziwa na viumbe wanaotegemea maji yake."*

Nukuu hii inaeleza kuwa uchafuzi wa Ziwa Victoria ni changamoto ya kiikolojia inayohitaji hatua za pamoja za kulinda mfumo mzima wa mazingira ya ziwa. Kuongezeka kwa uchafuzi kunaweza kuathiri ubora wa maji, viumbe wa majini na shughuli za jamii zinazotegemea ziwa. Maudhui ya *Citizen Planet* yanaonesha umuhimu wa kuchukua hatua dhidi ya uchafuzi huo, hasa kwa kuwa utafiti ulioripotiwa na kipindi ulionyesha uwepo wa tabaka za mafuta pamoja na viwango vya juu vya ammonium na nitrite, hali iliyohusishwa na vifo vya samaki. Kwa hivyo, mtafiti anaona kuwa uhifadhi wa Ziwa Victoria haupaswi kuishia katika kudhibiti uchafuzi wa maji pekee, bali unapaswa kuhusisha ulinzi wa bioanuai, udhibiti wa taka na majitaka, pamoja na ushirikiano kati ya serikali, wataalamu, jamii na taasisi za mazingira**.**

Dondoo hii inaonyesha umuhimu wa kuwa na usimamizi madhubuti wa taka na matumizi endelevu ya rasilimali za maji. Uchafuzi wa mito mara nyingi husababishwa na ongezeko la shughuli za kibinadamu, ukuaji wa miji, ukosefu wa mifumo bora ya kutibu taka na kutowajibika kwa baadhi ya watumiaji wa mazingira. Hivyo, ni muhimu kuweka mikakati kama usafishaji na urejeshaji wa mito, udhibiti wa taka za viwandani na hospitalini, elimu ya mazingira kwa jamii na utekelezaji wa sheria za uhifadhi wa maji. Hatua hizi zinaweza kusaidia kurejesha afya ya mito na kuhakikisha maji yanabaki salama kwa matumizi ya binadamu, mifugo na viumbe wengine.

Hoja hii ina uhusiano mkubwa na nadharia ya uhakiki ikolojia kwa sababu ya shughuli za binadamu zinavyoweza kuvuruga uwiano wa mifumo ya ikolojia na hatimaye kuathiri maisha ya jamii. Katika muktadha wa Ziwa Victoria, kuongezeka kwa uchafuzi wa maji, ikiwemo taka na vichafuzi vinavyoingia katika ziwa, kunaweza kuathiri viumbe wa majini, ubora wa maji na shughuli za jamii zinazotegemea ziwa. Kwa mtazamo wa Nadharia ya Uhakiki wa Ikolojia**,** hali hii inaonesha kuwa binadamu hawezi kujitenga na mazingira, kwa sababu uharibifu wa mfumo wa ikolojia wa ziwa huleta madhara kwa viumbe hai na pia kwa ustawi wa binadamu. Kwa hivyo, uhifadhi wa Ziwa Victoria unahitaji mabadiliko ya tabia za jamii, udhibiti wa uchafuzi na matumizi endelevu ya rasilimali za maji**.** Maudhui ya *Citizen Planet* kuhusu uchafuzi wa Ziwa Victoria yanaonesha umuhimu wa vyombo vya habari katika kufichua changamoto za

kimazingira na kuhamasisha jamii na taasisi husika kuchukua hatua za kulinda bioanuai na kudumisha uwiano wa ikolojia.

Hoja hii ina uhusiano wa karibu sana na utafiti wa Potts et al. (2024) kuhusu *"Global Biodiversity Threats & Protected Areas Expansion (30x30 Agenda)"*, unaosisitiza umuhimu wa kuimarisha maeneo ya uhifadhi ili kukabiliana na vitisho vinavyoathiri bioanuwai na mifumo ya ikolojia duniani. Agenda ya 30x30 inalenga kuongeza uhifadhi wa maeneo ya nchi kavu na baharini ifikapo mwaka 2030 ili kulinda viumbe hai, makazi yao na huduma za mifumo ya ikolojia. Nukuu kuhusu Ziwa Victoria inaendana na utafiti huu kwa kuonesha namna uchafuzi wa mazingira unavyoweza kuhatarisha mfumo wa ikolojia wa ziwa na viumbe wanaotegemea maji yake. Wakati nukuu inalenga zaidi ongezeko la uchafuzi katika Ziwa Victoria na athari zake kwa ubora wa maji, samaki na viumbe wengine wa majini**,** Potts et al. (2024) wanaangazia kwa mtazamo mpana zaidi vitisho vinavyosababisha kupungua kwa bioanuwai, uharibifu wa makazi na umuhimu wa kuimarisha hatua za uhifadhi. Kwa mtazamo huu, uchafuzi wa Ziwa Victoria unaweza kuchukuliwa kama mfano wa tishio la moja kwa moja kwa bioanuwai linalohitaji mikakati ya uhifadhi inayozingatia si tu kuweka maeneo chini ya ulinzi, bali pia kudhibiti uchafuzi, kurejesha mifumo ya ikolojia ya maji, kuimarisha usimamizi wa rasilimali na kuwashirikisha jamii zinazotegemea ziwa**.** Hivyo, nukuu na utafiti wa Potts et al. (2024) vinaunga mkono kwa pamoja hoja kwamba uhifadhi wa bioanuwai unahitaji hatua madhubuti za kupunguza shughuli za kibinadamu zinazoharibu mazingira na kulinda mifumo ya ikolojia kwa manufaa ya viumbe hai na ustawi wa jamii kwa muda mrefu.

Video inayolingana na hoja hii inapatikana
*https://www.youtube.com/watch?v=bgZL_QoVKR4&utm_*

4.3 Mikakati ya Kimawasiliano Inayotumika katika Vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*

Katika sehemu hii, mtafiti alichambua data iliyokusanywa kutoka katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa lengo la kubainisha mikakati ya kimawasiliano iliyotumika kuwasilisha ujumbe kuhusu uhifadhi wa mazingira. Kupitia uchambuzi huo, mtafiti alitambua mada ndogondogo zinazoonesha matumizi ya mikakati mbalimbali ya kimawasiliano kama vile maelezo, mahojiano, usimulizi, matumizi ya picha na vielelezo, pamoja na mifano halisi ya

shughuli za mazingira. Uchambuzi huu uliongozwa na mhimili wa nadharia ya uhakiki-ikolojia unaosisitiza uhusiano kati ya binadamu na mazingira na namna maudhui ya vyombo vya habari yanavyoweza kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za asili. Aidha, mtafiti alitumia nukuu na mifano kutoka katika vipindi teule kuonesha jinsi mikakati ya kimawasiliano inayotumiwa kufafanua masuala ya mazingira, kuvutia hadhira na kuhamasisha jamii kushiriki katika shughuli za uhifadhi wa mazingira. Hivyo, uchambuzi huu uliwezesha kuelewa mchango wa mikakati ya kimawasiliano katika kufanikisha mawasiliano ya mazingira kupitia vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*.

4.3.1 Mikakati ya Matumizi ya Maonesho ya Vitendo

Matumizi ya maonesho ya vitendo ni mojawapo ya mikakati ya kimawasiliano inayotumika katika vipindi teule ili kuwasilisha ujumbe kwa njia ya wazi, halisi na inayoeleweka kwa urahisi. Mkakati huu hujitokeza pale ambapo wataalamu, wakulima na wahifadhi wa mazingira huonyesha hatua kwa hatua namna ya kutekeleza shughuli mbalimbali zinazohusiana na kilimo na uhifadhi wa mazingira badala ya kutoa maelezo ya kinadharia pekee. Katika kipindi cha *Shamba Shape-Up*, wataalamu huonyesha kwa vitendo mikakati kama vile utengenezaji wa mboji, upimaji wa udongo na matumizi sahihi ya mbegu bora ili kuboresha uzalishaji wa kilimo. Vivyo hivyo, katika kipindi cha *Citizen Planet*, wataalamu na wanajamii huonyesha kwa vitendo shughuli za uhifadhi wa mazingira kama vile upandaji miti, usimamizi wa taka, uhifadhi wa vyanzo vya maji na matumizi endelevu ya rasilimali za asili. Kupitia maonesho hayo, watazamaji hupata fursa ya kuona utekelezaji wa shughuli husika katika mazingira halisi, jambo linaloongeza uelewa, kuvutia hadhira na kuwahamasisha kuiga mbinu zinazofundishwa. Hivyo, maonesho ya vitendo huchangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha lengo la vipindi hivi la kuelimisha jamii kuhusu kilimo bora na uhifadhi wa mazingira kwa njia rahisi, shirikishi na yenye ushawishi.

M-09-V-SSU

Mfano mwingine ni: *Shamba Shape-Up Shamba Shape-Up* – Series 16, Episode 1:10 Machi 2026**.**Farm Plan, Soil Testing, Compost and Seed Selection Huonyeshwa Jumapili saa 1:30 pm na jumamosi saa 1:30 kiswahili.

> *“Hebu tuone jinsi ya kuboresha ubora wa udongo wetu kwa kutengeneza mboji bora na kuitumia kwa usahihi shambani.”*

Nukuu hii, “Hebu tuone jinsi ya kuboresha ubora wa udongo wetu kwa kutengeneza mboji bora na kuitumia kwa usahihi shambani,” inaonyesha dhamira ya mhusika au mwandishi ya kuhimiza utunzaji wa mazingira kupitia kilimo endelevu. Matumizi ya maneno “kuboresha ubora wa udongo” yanaonesha kuwa udongo unatambuliwa kama rasilimali muhimu inayohitaji kulindwa na kuendelezwa. Aidha, kauli “kutengeneza mboji bora” inasisitiza matumizi ya mbinu za asili katika kuongeza rutuba ya udongo badala ya kutegemea kemikali pekee. Hivyo, nukuu hii inajenga ujumbe wa uwajibikaji wa binadamu katika kuhifadhi mazingira na kuhakikisha uzalishaji endelevu wa mazao.

Matumizi ya mboji bora ni njia muhimu ya kuboresha mazingira ya udongo na kuongeza tija ya kilimo. Mboji huongeza virutubisho muhimu, huboresha uwezo wa udongo kuhifadhi maji, na kusaidia kuimarisha viumbe hai wadogo wanaoishi ardhini ambao ni muhimu katika mzunguko wa virutubisho. Aidha, matumizi ya mboji hupunguza utegemezi wa mbolea za viwandani ambazo zinaweza kuathiri mazingira kwa muda mrefu. Hivyo, wakulima wanapaswa kuelimishwa kuhusu utengenezaji wa mboji bora na matumizi yake sahihi ili kufikia kilimo endelevu.

Kwa kuzingatia nadharia ya uhakiki ikolojia, nukuu hii inaonyesha uhusiano wa karibu kati ya binadamu na mazingira yake. Nadharia hii huchunguza namna binadamu anavyotumia, kuhifadhi au kuharibu mazingira kupitia matendo yake. Katika nukuu hii, matumizi ya mboji yanaonekana kama tendo la kuheshimu mfumo wa asili kwa kurejesha nguvu ya udongo badala ya kuutumia kupita kiasi. Hivyo, ujumbe wa nukuu unaunga mkono wazo la uhakiki ikolojia kwamba binadamu anapaswa kuishi kwa uwiano na mazingira na kuchukua jukumu la kulinda rasilimali za asili kwa vizazi vijavyo. Kwa ujumla, nukuu hii ni mwito wa kuhamasisha kilimo kinachozingatia uhifadhi wa mazingira. Inaonyesha kuwa kuboresha udongo si suala la kuongeza uzalishaji pekee, bali pia ni njia ya kudumisha uhusiano mzuri kati ya binadamu, ardhi na viumbe hai wengine. Kupitia mtazamo wa uhakiki ikolojia, matumizi ya mboji yanaweza kuchukuliwa kama mfano wa uwajibikaji wa binadamu katika kutunza dunia.

Hoja hii ina uhusiano wa karibu sana na utafiti wa Langat (2021) kuhusu *“Communicating Agricultural Information Using Electronic Media: The Case of ‘Shamba Shape-Up’ Programme on Citizen Television in Kenya,”* unaochunguza namna taarifa za kilimo zinavyowasilishwa kwa wakulima kupitia vyombo vya kielektroniki, hususan televisheni. Nukuu inayosema, “Hebu tuone jinsi ya kuboresha ubora wa udongo wetu kwa kutengeneza mboji bora na kuitumia kwa

usahihi shambani," inaendana na utafiti huu kwa kuonesha namna *Shamba Shape-Up* inavyotumia mawasiliano ya televisheni kutoa elimu ya kilimo kwa njia rahisi, shirikishi na inayolenga vitendo. Wakati nukuu inalenga zaidi elimu kuhusu uboreshaji wa rutuba ya udongo kupitia utengenezaji na matumizi sahihi ya mboji**,** Langat (2021) anaangazia kwa mtazamo mpana zaidi namna taarifa za kilimo zinavyowasilishwa kupitia televisheni na mchango wake katika kuwafikishia wakulima maarifa ya kilimo**.** Kwa mtazamo huu, matumizi ya maonyesho ya vitendo kuhusu utengenezaji wa mboji yanaweza kuchukuliwa kama mkakati wa mawasiliano ya kilimo unaorahisisha uelewa na matumizi ya maarifa hayo katika shughuli za kilimo. Hivyo, nukuu na utafiti wa Langat (2021) vinaunga mkono kwa pamoja hoja kwamba televisheni inaweza kuwa nyenzo muhimu ya kuwasilisha maarifa ya kilimo na mazingira kwa kutumia maelezo na maonyesho ya vitendo yanayowezesha wakulima kuelewa na kutumia mbinu endelevu za kuboresha udongo na uzalishaji wa kilimo.

https://www.youtube.com/watch?v=-oaaDHCShsA&utm

M-10-V-CP

Kwa mfano: *Citizen Planet* Lake Victoria farmers adopt durable, eco-friendly plastic fish cages, tarehe1 Machi 2026, 10:27 usiku, Dakika 8:56 Runinga ya Citizen**,** chanzo ni KenyaMOJA

> *"Vizimba hivyo, ambavyo huhifadhi zaidi samaki aina ya sato huelea ndani ya Ziwa Victoria kwa kutumia miundo imara inayoelea ambayo huwawezesha wafugaji kuwapatia chakula samaki, kuwafuatilia na kuwavuna moja kwa moja kutoka majini huku wakidumisha mifumo ya uzalishaji iliyo chini ya udhibiti."*

Nukuu hii, inadhihirisha matumizi ya mkakati wa maonyesho ya vitendo kwa kuwa mwandishi anaonesha kwa hatua na matendo halisi namna ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba unavyofanyika. Badala ya kueleza kwa ujumla kuwa samaki wanafugwa ndani ya ziwa, mwandishi anafafanua jinsi vizimba vinavyoelea majini, namna wafugaji wanavyowapatia samaki chakula, wanavyowafuatilia ukuaji wao na hatimaye kuwavuna. Maelezo haya yanampa msomaji taswira ya moja kwa moja ya mchakato wa ufugaji wa samaki na hivyo kuifanya

mkakati wa maonyesho ya vitendo kuwa bayana katika kuwasilisha ujumbe wa matumizi endelevu ya rasilimali za maji.

Kauli hii ya matumizi ya mkakati wa maonyesho ya vitendo katika nukuu hii inaongeza uhalisia na uelewekaji wa ujumbe kuhusu ufugaji wa kisasa wa samaki. Kupitia maelezo ya hatua zinazofuatwa katika matumizi ya vizimba, mwandishi anadhihirisha namna teknolojia inavyoweza kutumika kuongeza uzalishaji wa samaki bila kutegemea uvuvi wa kupita kiasi kutoka kwenye mazingira ya asili. Aidha, mkakati huu humsaidia msomaji kuelewa kuwa ufugaji wa samaki si shughuli ya kubahatisha bali ni mfumo unaohitaji usimamizi, ufuatiliaji na udhibiti wa karibu ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali za maji. Hivyo, maonyesho ya vitendo yamefanikiwa kuwasilisha maarifa ya kimazingira kwa namna inayoelimisha na kushawishi.

Kwa mujibu wa nadharia ya uhakiki ikolojia, nukuu hii inaonesha uhusiano kati ya binadamu na mazingira ya majini katika matumizi ya rasilimali kwa njia endelevu. Mkakati wa maonyesho ya vitendo unaotumiwa na mwandishi unaonesha jinsi binadamu anavyotumia mazingira ya Ziwa Victoria kwa utaratibu unaodhibitiwa ili kukidhi mahitaji yake bila kuharibu mfumo wa ikolojia wa ziwa. Maelezo ya kuwafuatilia samaki, kuwapatia chakula na kudhibiti uzalishaji yanaashiria juhudi za kuhakikisha kuwa matumizi ya rasilimali za maji yanafanyika kwa uwiano unaolinda mazingira na viumbe wanaoishi ndani yake. Hivyo, nukuu hii inaafikiana na msingi wa uhakiki ikolojia unaosisitiza matumizi yenye uwajibikaji wa mazingira na umuhimu wa kudumisha usawa kati ya mahitaji ya binadamu na uhifadhi wa mifumo ya asili.

Hoja hii ina uhusiano na utafiti wa Ong'ong'a (2024) kuhusu *"Caring for Water, Plastics, and Trees: Community Radio and Digital Media in Kenya's Environmental Movements,"* unaochunguza nafasi ya vyombo vya habari, hususan redio za jamii na vyombo vya kidijitali, katika kuwasilisha taarifa na kuhamasisha jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira. Nukuu kuhusu vizimba vya samaki katika Ziwa Victoria inaendana na utafiti huu kwa kuonesha namna mawasiliano ya vyombo vya habari yanavyoweza kuwasilisha maarifa kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za maji na shughuli za kiuchumi zinazotegemea mazingira. Wakati nukuu inalenga zaidi ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba vinavyoelea na namna shughuli hiyo inavyodhibitiwa ili kuongeza uzalishaji wa samaki, Ong'ong'a (2024) anaangazia kwa mtazamo mpana zaidi jinsi redio za jamii na vyombo vya kidijitali vinavyowezesha uhamasishaji na ushiriki wa jamii katika masuala ya maji, plastiki, miti na uhifadhi wa mazingira**.** Kwa mtazamo huu, taarifa kuhusu ufugaji wa samaki katika vizimba inaweza kuchukuliwa kama mfano wa

mawasiliano ya matumizi endelevu ya rasilimali za maji, hasa pale ujumbe unapowahusisha jamii wanaotegemea Ziwa Victoria kwa maisha na shughuli za kiuchumi. Hivyo, nukuu na utafiti wa Ong'ong'a (2024) vinaunga mkono kwa pamoja hoja kwamba vyombo vya habari vinaweza kuwa nyenzo muhimu katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira na ushiriki wao katika uhifadhi wa mifumo ya ikolojia ya maji.

> *Video inayowasilisha hoja hii inapatikana kwa Citizen Planet – Lake Victoria eco-friendly fish cages*

M-11-V-CP

Mfano mwingine ni: *Citizen Planet*, Rural communities help preserve Nairobi's watersheds, tarehe 5 Aprili 2026, Runinga ya Citizen Kenya – YouTube mwandishi ni Agnes Oloo

> *"Jamii zinashiriki kikamilifu katika kurejesha maeneo ya vyanzo vya maji yaliyoharibika kupitia upandaji miti, kuweka uzio katika kingo za mito, na kudhibiti matumizi ya ardhi ili kulinda vyanzo vya maji na kuboresha upatikanaji wa maji katika maeneo ya chini ya mito."*

Nukuu hii, inadhihirisha matumizi ya mkakati wa maonyesho ya vitendo kwa kuwa mwandishi haishii kueleza umuhimu wa kuhifadhi vyanzo vya maji, bali anaonesha hatua mahsusi zinazochukuliwa na jamii katika utekelezaji wa shughuli hizo. Kupitia maelezo ya upandaji miti, uwekaji wa uzio kandokando ya mito na udhibiti wa matumizi ya ardhi, msomaji anaoneshwa kwa vitendo namna juhudi za uhifadhi wa mazingira zinavyotekelezwa. Hivyo, matumizi ya mkakati wa maonyesho ya vitendo yanajitokeza wazi kwa kuwa mwandishi anawasilisha matendo halisi yanayofanywa na jamii ili kurejesha na kulinda vyanzo vya maji badala ya kutoa maelezo ya kinadharia pekee.

Kauli ya matumizi ya mkakati wa maonyesho ya vitendo katika nukuu hii inaimarisha uelewa wa msomaji kuhusu wajibu wa jamii katika uhifadhi wa mazingira. Kwa kuonesha vitendo vinavyotekelezwa kama vile kupanda miti, kuweka uzio na kusimamia matumizi ya ardhi, mwandishi anabainisha kuwa utunzaji wa vyanzo vya maji unahitaji ushiriki wa moja kwa moja wa wananchi. Mkakati huu unasaidia kuonesha kuwa matatizo ya kimazingira yanaweza kutatuliwa kupitia hatua za pamoja na mipango endelevu ya uhifadhi. Aidha, maonyesho ya

vitendo yanatoa ushahidi wa namna shughuli za kibinadamu zinavyoweza kubadilishwa na kuelekezwa katika kulinda mazingira badala ya kuyaharibu.

Kwa mujibu wa nadharia ya uhakiki wa ikolojia, nukuu hii inasisitiza uhusiano wa karibu kati ya binadamu na mazingira pamoja na wajibu wa binadamu katika kuyahifadhi. Mkakati wa maonyesho ya vitendo unaotumika unaonesha jinsi jamii zinavyoshiriki moja kwa moja katika kurejesha usawa wa ikolojia kupitia hatua za kulinda vyanzo vya maji. Upandaji miti husaidia kuhifadhi unyevunyevu wa udongo na kuimarisha mzunguko wa maji, uwekaji wa uzio hulinda kingo za mito dhidi ya uharibifu, na udhibiti wa matumizi ya ardhi hupunguza shughuli zinazoweza kuhatarisha mazingira. Kwa hiyo, nukuu hii inaafikiana na misingi ya uhakiki ikolojia kwa kuonesha kwamba ustawi wa binadamu unategemea mazingira salama na kwamba uhifadhi wa mazingira unahitaji vitendo halisi vinavyodumisha uwiano wa mifumo ya asili.

Kauli hii ina uhusiano na utafiti wa Cohn et al. (2023) kuhusu *"Carrier Bag Storytelling with Coastal Kenyan Families: Sharing Food, Illustrations, and Knowledge for Tangible Environmental Justice Impacts,"* unaoangazia namna usimulizi shirikishi wa hadithi, maarifa na ubunifu wa jamii unavyoweza kuchochea uelewa na hatua kuhusu masuala ya mazingira na haki ya kimazingira. Nukuu inayosema, "Jamii zinashiriki kikamilifu katika kurejesha maeneo ya vyanzo vya maji yaliyoharibika kupitia upandaji miti, kuweka uzio katika kingo za mito, na kudhibiti matumizi ya ardhi..." inaendana na utafiti huu kwa kusisitiza ushiriki wa jamii katika kutatua changamoto za mazingira na kutumia maarifa ya jamii katika kuchochea hatua za uhifadhi**.** Wakati nukuu inalenga zaidi ushirikishwaji wa jamii katika kurejesha vyanzo vya maji, kupanda miti, kulinda kingo za mito na kudhibiti matumizi ya ardhi**,** Cohn et al. (2023) wanaangazia zaidi matumizi ya usimulizi wa hadithi, michoro, chakula na maarifa ya jamii kama njia za kuhamasisha uelewa na matokeo yanayolenga haki ya kimazingira**.** Kwa mtazamo huu, shughuli za jamii zilizotajwa katika nukuu zinaweza kuchukuliwa kama mfano wa utekelezaji wa maarifa na uhamasishaji wa kimazingira unaolenga kuleta mabadiliko halisi katika jamii. Hivyo, nukuu na utafiti wa Cohn et al. (2023) vinaunga mkono kwa pamoja hoja kwamba ushirikishwaji wa jamii na matumizi ya mbinu shirikishi za mawasiliano ni muhimu katika kuongeza uelewa, kuchochea hatua za uhifadhi na kuleta mabadiliko endelevu katika usimamizi wa mazingira

> *Video inayorejelea kipindi hiki inapatikana kwa Citizen Planet – Water catchment conservation Watersheds*

4.3.2 Mikakati ya Matumizi ya Elimu-Burudani

Matumizi ya Elimu-Burudani ni mkakati wa kufundisha na kutoa maarifa kwa kuchanganya elimu na burudani ili kufanya ujumbe uwe rahisi kueleweka na kuvutia zaidi kwa hadhira. Mkakati huu hutumia njia mbalimbali kama vile tamthilia, muziki, filamu, michezo, vipindi vya redio na televisheni kufikisha taarifa muhimu kuhusu masuala ya kijamii, afya, mazingira na maendeleo. Kupitia elimu-burudani, watu hujifunza kwa njia ya kufurahisha, jambo linaloongeza uelewa, kumbukumbu na uwezekano wa kubadili mitazamo au tabia zao kwa manufaa ya jamii.

M-10-V-SSU

Vile vile kuna mfano wa *Shamba Shape-Up* series 16-episode 23. Solar Powered Irrigation Systems, Mastitis, Pressure Cleaner and Shamba ni Biz Drama, eneo la Kimana Kajiado County, mhusika mkuu ni Simon Sankale muda Jumapili saa 1:30 mchana (Kiswahili) na Jumamosi saa 1:30 mchana (Kiingereza)**,** runinga Citizen Kenya

> *“Kipindi kinatumia mkakati wa elimu-burudani kwa kuchanganya mafunzo ya vitendo kuhusu kilimo na ufugaji na maigizo ya* Shamba ni Biz Drama, *hali inayorahisisha uwasilishaji wa maarifa na kuongeza mvuto wa ujumbe kwa watazamaji.”*

Nukuu hii inaeleza kuwa kipindi kinaonesha kuwa elimu-burudani ni mkakati muhimu wa mawasiliano ya kilimo, kwa sababu huunganisha maarifa ya kitaalamu na vipengele vya burudani vinavyorahisisha kuelewa na kukumbuka ujumbe unaowasilishwa. Katika *Shamba Shape-Up* Series 16, Episode 23, mafunzo kuhusu umwagiliaji wa kilimo, afya ya mifugo na shughuli za kuongeza kipato yanaunganishwa na kipengele cha Shamba ni Biz Drama, hivyo ujumbe wa kilimo hauwasilishwi kwa namna ya kitaalamu pekee bali pia kwa njia ya kuvutia na shirikishi. Kwa hivyo, mbinu hii huongeza uwezekano wa kujifunza, kuhusisha maarifa na mazingira yao na kuchochewa kuchukua hatua**.** Hivyo, matumizi ya elimu-burudani katika kipindi yanaonesha kuwa televisheni inaweza kuwa chombo cha kutoa elimu ya vitendo huku ikidumisha mvuto, jambo linaloendana na maelezo rasmi ya *Shamba Shape-Up* kwamba programu hiyo imejengwa juu ya kuchanganya elimu na burudani.

Kauli hii inaonyesha jinsi mkakati wa elimu burudani unavyoweza kutumika kwa ufanisi katika kusambaza maarifa ya kilimo na ufugaji kwa jamii. Elimu-burudani ni mkakati wa kuwasilisha maarifa ya kilimo kwa njia inayochanganya elimu na burudani. Katika *Shamba Shape-Up* Series 16, Episode 23, mafunzo ya vitendo kuhusu kilimo na ufugaji yanaambatana na kipengele cha maigizo cha Shamba ni Biz Drama, hivyo ujumbe wa kielimu huwasilishwa kwa namna rahisi, ya kuvutia na inayoweza kushirikisha jamii. Muunganiko huu husaidia kupunguza ugumu wa ujumbe wa kitaalamu na kuufanya uwe rahisi kueleweka na kukumbukwa. Hivyo, nguvu ya elimu-burudani katika kipindi hiki haipo katika kutoa elimu pekee, bali katika kutumia burudani kama nyenzo ya kufanya elimu iwe na mvuto, ushirikishwaji na uelewekaji zaidi.

Kwa mtazamo wa Nadharia ya Uhakiki wa Ikolojia**,** nukuu hii inaonesha kuwa elimu-burudani inaweza kuwa njia muhimu ya kuwasilisha uhusiano kati ya binadamu, kilimo, ufugaji na mazingira. Nadharia hii inasisitiza kuchunguza namna shughuli za binadamu zinavyoathiri mazingira na umuhimu wa kujenga mahusiano endelevu kati ya jamii na ulimwengu wa asili. Katika nukuu hii, mafunzo ya vitendo kuhusu kilimo na ufugaji yanapotolewa kupitia *Shamba Shape-Up* pamoja na maigizo ya Shamba ni Biz Drama, yanaweza kuwasaidia wakulima kuelewa kwamba shughuli za uzalishaji zinapaswa kuzingatia matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira. Kwa mtazamo huu, matumizi ya elimu-burudani yanaifanya dhana ya uhifadhi wa mazingira iwe rahisi kufikishwa kwa jamii kwa kutumia lugha na matukio yanayohusiana na maisha yao ya kila siku. Hivyo**,** uhusiano kati ya nukuu na Nadharia ya Uhakiki wa Ikolojia unaonekana katika matumizi ya mawasiliano ya televisheni kuhamasisha uelewa wa tabia za binadamu zinazoweza kusaidia kulinda mazingira na kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za asili.

Utafiti wa Mutoro et al (2026) kuhusu *Effectiveness of Using Different Presentation Methods on Cheetah Conservation Awareness and Education in Kenya* una uhusiano wa karibu na matumizi ya maigizo ya Shamba ni Biz Drama katika *Shamba Shape-Up*, kwa kuwa tafiti zote zinaonesha umuhimu wa kutumia mbinu za uwasilishaji zinazovutia na kushirikisha hadhira katika kufikisha ujumbe wa kielimu. Mutoro na wenzake walionyesha kuwa matumizi ya mbinu mbalimbali za uwasilishaji, kama video, mabango na vikaragosi, yanaweza kuongeza uelewa wa wanafunzi kuhusu uhifadhi wa duma na mazingira. Vivyo hivyo, Shamba ni Biz Drama hutumia maigizo kama nyenzo ya elimu-burudani**,** ambapo ujumbe kuhusu kilimo, ufugaji na matumizi endelevu ya rasilimali huwasilishwa kupitia matukio yanayohusiana na maisha ya kila siku ya jamii. Kwa hivyo, tofauti kubwa ni kwamba Mutoro na wenzake walijikita katika elimu ya uhifadhi wa

wanyamapori**,** wakati Shamba ni Biz Drama inalenga zaidi elimu ya kilimo, ufugaji na maisha ya kijamii na kiuchumi ya wakulima**.** Hata hivyo, tafiti zote zinaunga mkono hoja kwamba ujumbe unapowasilishwa kwa njia ya kuvutia, ya kisanaa na inayohusisha hadhira, huwa rahisi kueleweka na kukumbukwa**.** Hivyo, matumizi ya maigizo katika Shamba ni Biz Drama yanaonesha namna televisheni inavyoweza kutumia elimu-burudani kuunganisha maarifa na burudani, kuongeza mvuto wa ujumbe na kuhamasisha hadhira kuzingatia mbinu bora na endelevu za kilimo na ufugaji.

> *Video inayolingana na kazi hii ni https://shambashapeup.com/kenya-series/ssu-16/ep-23-solar-powered-irrigation-systems-mastitis-pressure-cleaner-and-shamba-ni-biz-drama/?*

M-12-V-CP

Kwa mfano: *Citizen Planet* Maasai pastoralists in Kajiado adopt innovative grazing, tap carbon credits Tarehe: 14 Desemba 2025 Muda wa kuchapishwa: 10:03 usiku Urefu: dakika 6:55 na Chanzo**:** Runinga ya Citizen kupitia KenyaMOJA.

> *"Wafugaji wa Kajiado wanatumia mbinu bunifu za usimamizi wa malisho zinazosaidia kurejesha ardhi iliyoharibika na kuimarisha uendelevu wa ufugaji katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi."*

Nukuu hii inaonesha mabadiliko kutoka katika usimamizi wa jadi wa malisho kwenda katika mbinu bunifu zinazolenga kurejesha afya ya ardhi na kuimarisha uendelevu wa ufugaji**.** Video inaeleza kuwa wafugaji wa Kajiado wanatumia mbinu za ubunifu za malisho ambazo zinasaidia kurejesha maeneo yaliyoharibika, huku pia zikiunganishwa na fursa za carbon credits katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Jambo muhimu katika nukuu hii ni kwamba uhifadhi wa ardhi hauwasilishwi kama jukumu la mazingira pekee, bali unaunganishwa na maisha na uchumi wa wafugaji**.** Hivyo, matumizi endelevu ya malisho yanaweza kusaidia kulinda uoto wa asili, kupunguza uharibifu wa ardhi na kuwezesha jamii kuendelea kupata riziki kutokana na ufugaji. Nukuu hii pia inaonesha namna *Citizen Planet* inavyotumia simulizi za maisha halisi ya

jamii kuwasilisha ujumbe wa mazingira, jambo linaloweza kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa kurejesha ardhi iliyoharibika na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kauli hii inaonyesha matumizi madhubuti ya mikakati ya elimu burudani katika kuwasilisha maarifa ya ufugaji na uhifadhi wa mazingira. Matumizi ya simulizi za kabla na baada huongeza mvuto wa ujumbe kwa sababu hadhira huweza kuona matokeo halisi ya mabadiliko yanayozungumziwa badala ya kusikia maelezo ya kinadharia pekee. Mkakati huu husaidia kujenga uelewa, kuimarisha kumbukumbu ya ujumbe na kuwahamasisha jamii kubadili mitazamo na tabia zao kwa kuzingatia mifano ya mafanikio inayowasilishwa. Hivyo, elimu inayotolewa huwa na uwezekano mkubwa wa kuleta mabadiliko ya vitendo katika jamii kwa sababu inaunganishwa na uzoefu halisi na ushahidi unaoonekana.

Aidha, katika nadharia ya Uhakiki Ikolojia, nukuu hii inaonyesha uhusiano wa moja kwa moja kati ya shughuli za binadamu, mifugo na mazingira. Usimamizi bora wa malisho unachangia urejeshwaji wa uoto wa asili, kuimarika kwa afya ya mifugo na kuongezeka kwa uzalishaji, jambo linalodhihirisha kuwa matumizi sahihi ya rasilimali za mazingira yanaweza kuleta manufaa kwa binadamu na mfumo ikolojia kwa pamoja. Nadharia hii inasisitiza kuwa mazingira si rasilimali ya kutumiwa tu, bali ni mfumo unaohitaji kulindwa na kusimamiwa kwa uendelevu. Kupitia mkakati wa elimu burudani na matumizi ya simulizi za kabla na baada, hadhira hujengewa ufahamu kuhusu athari za matendo ya binadamu kwa mazingira na umuhimu wa kutumia mbinu zinazorejesha na kuhifadhi usawa wa ikolojia huku zikiboresha ustawi wa jamii.

Hoja hii inaafikiana na utafiti wa Kitula et al kwa kuwa yote yanasisitiza umuhimu wa kutumia mikakati ya mawasiliano inayovutia na kushirikisha hadhira katika kuwasilisha masuala ya mazingira na uendelevu. Ubaga na Kitula walibaini kuwa mitandao ya kijamii kama Instagram, TikTok, WhatsApp na X huongeza uelewa wa vijana kuhusu mabadiliko ya tabianchi kupitia usimulizi wa picha, hadithi za uzoefu, maudhui ya kuvutia na ushirikishwaji wa wahamasishaji wa mtandaoni. Vivyo hivyo, nukuu hii inaonyesha matumizi ya simulizi za kabla na baada katika kueleza mafanikio ya usimamizi wa malisho, ambapo hadhira huoneshwa tofauti ya hali ya mazingira na uzalishaji kabla na baada ya kutumia mbinu mpya. Kwa mtazamo wa elimu burudani, tafiti zote mbili zinaonyesha kuwa hadhira hujifunza kwa urahisi zaidi inapowekewa ushahidi unaoonekana, simulizi zinazogusa hisia na mifano halisi ya mafanikio badala ya maelezo ya kinadharia pekee. Aidha, utafiti wa Ubaga na Kitula unaonyesha kuwa maudhui ya kuvutia huongeza uhamasishaji wa vijana na ushiriki wao katika masuala ya mazingira, huku

nukuu hii ikionyesha kuwa simulizi za mabadiliko chanya katika mifugo na mazingira huwafanya watazamaji kuvutiwa, kuelewa na kuhamasika kuiga mbinu hizo. Hivyo, kazi zote mbili zinathibitisha kuwa mkakati wa elimu burudani ni nyenzo muhimu katika kujenga uelewa, kubadili mitazamo na kuhamasisha jamii kushiriki katika uhifadhi wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za ikolojia.

https://www.kenyamoja.com/video/maasai-pastoralists-kajiado-adopt-innovative-grazing-tap-carbon-credits-amid-climate-change?

4.3.3 Mikakati ya Matumizi ya Mifano Halisi

Matumizi ya mifano halisi ni mkakati wa ufundishaji au mawasiliano inayohusisha kutumia matukio, vitu, uzoefu au hali zinazopatikana katika maisha ya kila siku ili kufafanua na kuimarisha uelewa wa dhana fulani. Mkakati huu huwasaidia walengwa kuhusisha maarifa mapya na mazingira yao halisi, hivyo kufanya ujumbe kuwa rahisi kueleweka, kukumbukwa na kutekelezwa. Kwa mfano, katika kufundisha masuala ya uhifadhi wa mazingira au kilimo endelevu, mwalimu au mwasilishaji anaweza kutumia mifano ya ukame, mmomonyoko wa udongo au mbinu za kilimo zinazotumiwa katika jamii husika. Hivyo, matumizi ya mifano halisi huongeza ushiriki wa walengwa, hujenga uelewa wa kina na huchochea matumizi ya maarifa katika maisha ya kila siku.

M-10-V-SSU

Kwa mfano: Kipindi cha *Shamba Shape-Up* series 15 episode 17. Kilichapishwa tarehe 5 Agosti 2025 na kilirekodiwa Rongai**,** Nakuru County, kikitembelea wakulima Griffin na Edith.

> *"Kipindi kinatumia ushauri wa wataalamu na maonyesho ya vitendo kuwasaidia wakulima kuboresha malezi ya ndama, lishe, usafi wa mabanda na afya ya mifugo."*

Nukuu hii inaeleza kuwa kipindi kinatumia mkakati wa mifano halisi kwa kuwapeleka wataalamu moja kwa moja katika mazingira ya wakulima ili kuonesha na kueleza mkakati bora wa kilimo kwa vitendo. Badala ya kutoa maelezo ya kinadharia pekee, wataalamu huonekana wakitembelea mashamba, kuchunguza changamoto zilizopo na kutoa ushauri unaolingana na hali halisi ya mkulima husika. Mkakati huu huwasaidia wakulima kuona hatua za utekelezaji, kuelewa namna ya kutumia maarifa wanayopata na kuamini zaidi ujumbe unaotolewa kwa

sababu unatokana na uzoefu wa maisha ya kila siku. Hivyo, matumizi ya mifano halisi hufanya elimu ya kilimo kuwa rahisi kufikiwa na yenye uhusiano wa moja kwa moja na mahitaji ya jamii.

Pia, matumizi ya mifano halisi katika kipindi hiki ni mkakati muhimu wa kuongeza ufanisi wa mawasiliano ya elimu kwa wakulima. Kuonesha wataalamu wakifanya kazi kwenye mashamba halisi huongeza uelewa wa watazamaji kwa sababu wanapata nafasi ya kuona tatizo, suluhisho na matokeo yanayoweza kupatikana. Kwa hivyo, mkakati huu hujenga ushiriki wa hadhira, huimarisha kumbukumbu ya ujumbe na kuhamasisha mabadiliko ya tabia kwa kuwa wakulima wanaweza kujifunza kupitia uzoefu wa wakulima wenzao. Aidha, maonyesho ya vitendo hupunguza tofauti kati ya maarifa ya kitaalamu na matumizi yake katika mazingira halisi ya kilimo.

Kwa upande mwingine, Nadharia ya Uhakiki Ikolojia, inaonyesha uhusiano kati ya binadamu, shughuli za kilimo na mazingira yanayowazunguka. Kutembelea mashamba na kutoa ushauri kulingana na hali halisi kunaonesha umuhimu wa kuelewa mazingira kabla ya kupendekeza mkakati wa uzalishaji. Mifano halisi inayotolewa na wataalamu husaidia jamii kutambua athari za matumizi ya rasilimali za asili na umuhimu wa kutumia mikakati endelevu inayolinda udongo, maji na viumbe hai. Kwa njia hii, kipindi kinasaidia kujenga uelewa wa kimazingira kwa kuonesha kuwa maendeleo ya kilimo yanapaswa kuendana na uhifadhi wa mfumo ikolojia na mahitaji ya jamii.

Vile vile, utafiti wa Cohn na wenzake (2023) kuhusu *Carrier Bag Storytelling with Coastal Kenyan Families: Sharing Food, Illustrations, and Knowledge for Tangible Environmental Justice Impacts* una uhusiano na nukuu hii kwa kuwa yote yanatumia mikakati ya kimawasiliano inayolenga kupeleka maarifa ya kitaalamu kwa jamii kupitia mifano inayoeleweka na inayohusiana na maisha ya kila siku. Utafiti wa Cohn na wenzake ulitumia usimulizi wa hadithi, picha na maarifa ya jamii za pwani ya Kenya ili kufikisha ujumbe kuhusu afya, chakula, uendelevu na haki ya mazingira. Utafiti huo ulisisitiza kuwa hadithi na vielelezo vinaweza kuunganisha maarifa ya kisayansi na uzoefu wa jamii, hivyo kufanya ujumbe wa mazingira na maendeleo kueleweka kwa urahisi zaidi. Vivyo hivyo, nukuu kuhusu kipindi kinachohusisha timu ya wataalamu wanaotembelea mashamba mbalimbali inaonyesha matumizi ya mkakati wa mifano halisi, ambapo wakulima hujifunza kupitia maonesho ya vitendo na ushauri unaotolewa katika mazingira yao halisi. Kama ilivyo kwa Cohn na wenzake waliotumia hadithi za familia za pwani kuwasilisha maarifa, kipindi hiki kinatumia mashamba halisi kama jukwaa la

kuonyesha changamoto na suluhisho za kilimo. Njia zote mbili zinaondoa pengo kati ya maarifa ya kitaalamu na uhalisia wa jamii kwa sababu watazamaji hawaishii kusikia maelekezo bali wanaona namna maarifa yanavyotekelezwa katika maisha halisi. Hivyo, tafiti zote mbili zinaonesha kuwa matumizi ya mifano halisi ni mkakati muhimu wa mawasiliano ya maendeleo kwa sababu huongeza ushiriki wa jamii, hujenga uaminifu na kurahisisha mabadiliko ya tabia. Utafiti wa Cohn na wenzake unaonyesha nguvu ya hadithi na vielelezo katika kuhusisha jamii na masuala ya mazingira, huku kipindi cha kilimo kikionyesha nguvu ya maonesho ya vitendo katika kuwafanya wakulima kuona matokeo yanayoweza kupatikana. Hivyo, zote zinaunga mkono wazo kwamba elimu inayotokana na uzoefu halisi huwa na uwezo mkubwa wa kuchochea uelewa na matumizi ya maarifa mapya.

https://shambashapeup.com/kenya-series/series-15/ep-17-calf--heifer-care-and-high-pressure-washer-and-shamba-ni-biz/?

4.3.4 Mikakati ya Matumizi ya Mahojiano ya Jamii

Matumizi ya mahojiano ya jamii ni mkakati wa utafiti na mawasiliano ambapo, mwandishi wa habari au mtayarishaji wa maudhui hukusanya taarifa kwa kuuliza maswali moja kwa moja kwa wanajamii au wahusika husika kuhusu uzoefu wao, maoni yao na changamoto wanazokabiliana nazo katika maisha yao ya kila siku. Mkakati huu humwezesha mtafiti kupata taarifa za moja kwa moja kutoka kwa chanzo halisi, hivyo kuongeza uhalisia, uaminifu na kina cha taarifa zinazokusanywa. Kupitia mahojiano ya jamii, sauti za wananchi husikika na kuakisiwa katika matokeo ya utafiti au mawasiliano ya vyombo vya habari, jambo linalosaidia kuelewa kwa undani hali halisi ya kijamii au kimazingira inayochunguzwa.

M-11-V-SSU

Mfano mwingine: *Citizen Planet*, Tiaty Community Restores Degraded Land Amid Climate Crisis Tarehe ya kuchapishwa: 9 Agosti 2026 Muda 10:51 usiku Urefu: dakika 8:33

Chanzo: Runinga ya Citizen kupitia KenyaMOJA

“Jamii ya Tiaty inashiriki katika kurejesha ardhi iliyoharibika kwa kupanda nyasi za asili, huku wanajamii wakieleza namna hatua hizi zinavyosaidia kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kurejesha mazingira yao.”

Nukuu hii inaonesha umuhimu wa ushirikishwaji wa jamii katika urejeshaji wa mazingira. Wanajamii wa Tiaty hawajaoneshwa kama watazamaji wa changamoto za mabadiliko ya tabianchi, bali kama washiriki wanaochukua hatua za kurejesha ardhi iliyoharibika kwa kutumia nyasi za asili. Chanzo cha video kinaeleza kuwa jamii hiyo inarejesha eneo la ekari 16 lililoharibika, hatua inayolenga kuhuisha ardhi na mifumo ya ikolojia. Jambo hili linaonesha kuwa uhifadhi wa mazingira huwa na ufanisi zaidi pale jamii inapohusishwa moja kwa moja katika kutafuta na kutekeleza suluhisho. Aidha, kupewa nafasi kwa wanajamii kueleza uzoefu wao kupitia *Citizen Planet* kunafanya ujumbe wa mazingira uhusishwe na maisha halisi ya wananchi. Hivyo, kipindi kinaonesha kuwa mawasiliano ya mazingira yanaweza kuunganisha sauti za jamii, maarifa ya eneo husika na hatua za vitendo, na hivyo kuongeza uelewa kuhusu urejeshaji wa mifumo ya ikolojia na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Pia, matumizi ya mahojiano katika kipindi hiki ni njia bora ya kuwashirikisha watazamaji na kuwapa nafasi wakulima kuwa sehemu ya mchakato wa utoaji wa elimu. Mahojiano ya jamii ni kama mkakati wa mawasiliano ya mazingira, kwa sababu inawapa wanajamii nafasi ya kueleza moja kwa moja uzoefu wao katika kurejesha ardhi iliyoharibika. Katika *Citizen Planet* kuhusu Tiaty, jamii inaoneshwa ikiwa mshiriki hai katika kurejesha eneo lililoharibika kwa kutumia nyasi za asili, badala ya kuwasilishwa kama watazamaji wa changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Matumizi ya mahojiano katika mazingira haya huongeza uhalisia na uaminifu wa ujumbe, kwa kuwa jamii hupata fursa ya kusikia uzoefu wa watu wanaohusika moja kwa moja na shughuli za urejeshaji. Pia, mbinu hii hufanya maarifa ya jamii na uzoefu wao wa eneo husika kuwa sehemu ya simulizi la uhifadhi. Hivyo, *Citizen Planet* hutumia sauti za wanajamii kuonesha kwamba uhifadhi na urejeshaji wa mazingira unahitaji ushiriki wa watu wanaoishi katika maeneo hayo**,** huku televisheni ikiwa daraja la kuwasilisha uzoefu huo kwa hadhira pana.

Isitoshe, kwa mujibu wa Nadharia ya Uhakiki Ikolojia, nukuu hii inaonyesha umuhimu wa kuelewa uhusiano kati ya binadamu, shughuli za kilimo na mazingira kupitia sauti za jamii zinazotegemea rasilimali hizo. Mahojiano na wasimamizi wa shamba yanaonesha namna watu wanavyoathiri na kuathiriwa na mazingira yao, ikiwemo matumizi ya ardhi, maji na rasilimali nyingine za asili. Kupitia simulizi za wahusika, kipindi husaidia kufichua changamoto za kimazingira na suluhisho zinazotokana na uzoefu wa jamii. Hivyo, mikakati ya mahojiano inakuwa chombo cha kujenga ufahamu wa ikolojia kwa kuonesha kuwa uhifadhi wa mazingira unahitaji ushiriki wa jamii na kuzingatia maarifa yanayotokana na maisha halisi.

Kauli hii ina lingana na utafiti wa Vaughan na Johns (2021) wa *Beyond Frame Analysis: Environmental Video Messaging* kwa kuwa yote yanaonesha umuhimu wa matumizi ya mawasiliano ya kuona na sauti katika kufikisha ujumbe wa mazingira kwa hadhira. Utafiti wa Vaughan na Johns unaeleza kuwa video za mazingira hazipaswi kuchunguzwa kwa kuangalia ujumbe unaowasilishwa pekee, bali pia namna mikakati ya uwasilishaji inavyotumika kujenga uelewa na kuhusisha wanajamii. Utafiti wa Vaughan na Johns unaeleza kuwa video za mazingira hazipaswi kuchambuliwa kwa kuangalia maudhui pekee, bali pia namna mbinu za uwasilishaji zinavyotumika kujenga uelewa na kushirikisha jamii. Vivyo hivyo, katika *Citizen Planet* kuhusu jamii ya Tiaty, matumizi ya mahojiano yanawapa wanajamii nafasi ya kueleza uzoefu wao kuhusu urejeshaji wa ardhi iliyoharibika na juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kupitia sauti za jamii, ujumbe wa uhifadhi unakuwa na uhalisia zaidi kwa sababu unatokana na watu wanaokabili changamoto za mazingira na kushiriki moja kwa moja katika kuzitatua. Mbinu hii huongeza uaminifu, uhalisia na ukaribu wa ujumbe, kwa kuwa jamii haionyeshwi tu kama waathirika wa uharibifu wa mazingira, bali pia kama sehemu ya suluhisho. Aidha, mahojiano yanawezesha *Citizen Planet* kuwasilisha maarifa na uzoefu wa eneo husika ambalo linaweza kutopatikana katika maelezo ya kitaalamu pekee. Hivyo, uhusiano kati ya utafiti wa Vaughan na Johns (2021) na maudhui ya jamii ya Tiaty unaonesha kuwa mahojiano ni mkakati muhimu wa mawasiliano ya mazingira unaounganisha taarifa za kisayansi na uzoefu wa jamii**,** na hivyo kufanya ujumbe wa uhifadhi kuwa rahisi kueleweka, wenye uhalisia na wenye uwezo wa kuhamasisha ushiriki katika urejeshaji wa mazingira.

> *https://www.kenyamoja.com/video/citizen-planet-tiaty-community-restores-degraded-land-amid-climate-crisis-citizen-tv-428742?*

4.3.5 Mikakati ya Matumizi ya Taswira na Video

Matumizi ya taswira na video katika mawasiliano ya kijamii ni mkakati muhimu wa kuwasilisha ujumbe kwa njia inayoonekana na kueleweka kwa urahisi na hadhira mbalimbali. Taswira kama picha, michoro na video husaidia kuonesha uhalisia wa matukio, mazingira au changamoto fulani kuliko maneno pekee. Kupitia video, watazamaji huweza kuona moja kwa moja matendo, mahojiano, na matokeo ya matukio yanayowasilishwa, jambo linaloongeza uelewa, ushawishi na kumbukumbu ya kile kinachowasilishwa. Mkakati huu pia huongeza mvuto wa mawasiliano kwa sababu unachanganya sauti na picha, hivyo kufanya ujumbe kuwa hai na wa kuvutia zaidi. Katika muktadha wa elimu na uhamasishaji wa jamii, matumizi ya taswira na video huchangia

kwa kiasi kikubwa kuelimisha, kubadilisha mitazamo na kuhamasisha hatua za vitendo kwa hadhira.

M-12-V-SSU

Mfano wa *Shamba Shape-Up* – Series 15, Episode 18, Dairy Cows, Brush Cutter and Shamba ni Biz Drama eneo la Kaloleni, Kilifi County, mhusika mkuu Jonathan, mkulima mwenye shamba ekari 8.

> *"Kipindi kinatumia taswira na maonyesho ya vitendo kuwaonesha watazamaji namna wataalamu wanavyotekeleza mbinu za kuboresha ufugaji wa ng'ombe na matumizi ya mashine ya brush cutter katika maandalizi ya ardhi na udhibiti wa magugu. Uwasilishaji huu wa kuona huwezesha watazamaji kuelewa kwa urahisi mchakato wa utekelezaji wa mbinu hizo katika mazingira halisi ya shamba."*

Nukuu hii inaonesha kuwa matumizi ya taswira na maonyesho ya vitendo ni mkakati muhimu wa mawasiliano katika *Shamba Shape-Up*. Badala ya kutegemea maelezo ya maneno pekee, kipindi huwaonesha wakulima hatua za utekelezaji wa mbinu za kilimo na ufugaji katika mazingira halisi ya shamba. Katika Series 15, Episode 18, kwa mfano, wataalamu wanaonesha kwa vitendo namna ya kuboresha usimamizi wa ng'ombe pamoja na matumizi ya brush cutter katika maandalizi ya ardhi na udhibiti wa magugu. Kwa hivyo, taswira huongeza uelewekaji, uhalisia na mvuto wa ujumbe**,** kwa sababu mtazamaji anaweza kuona moja kwa moja namna mbinu inayofundishwa inavyotekelezwa. Hii huifanya elimu ya kilimo kuwa ya vitendo zaidi na kumwezesha mtazamaji kuhusisha maarifa anayoyaona na mazingira yake mwenyewe. Aidha, matumizi ya taswira yanaendana na muundo wa *Shamba Shape-Up* wa kuleta wataalamu katika mashamba halisi na kuonesha suluhisho kupitia maelezo na maonyesho.

Aidha, matumizi ya taswira na video katika nukuu hii ni mkakati muhimu wa mawasiliano kwa sababu huonesha kwa vitendo namna mbinu bora za ufugaji wa ng'ombe na matumizi ya mashine ya brush cutter yanavyotekelezwa katika mazingira halisi ya shamba. Kuonesha ng'ombe, mabanda ya mifugo, vifaa vya ufugaji pamoja na mashine ya brush cutter huwasaidia watazamaji kuelewa kwa urahisi uhusiano kati ya matumizi ya teknolojia, usimamizi bora wa mifugo na uendelevu wa shughuli za kilimo. Mikakati hii huongeza uaminifu na uelewekaji wa ujumbe**,** kwa kuwa hadhira haiishii kusikia maelezo ya wataalamu bali pia huona namna mbinu hizo zinavyotumika. Kwa mtazamo huo, matumizi ya taswira za shughuli za ufugaji na

uendeshaji wa brush cutter huifanya elimu ya kilimo kuwa ya vitendo, ya kuvutia na rahisi kukumbukwa, huku ikiwezesha kutambua manufaa ya kutumia teknolojia na mbinu bora katika kuboresha uzalishaji na usimamizi wa rasilimali za shamba.

Kwa upande wa Nadharia ya Uhakiki Ikolojia**,** nukuu kuhusu ufugaji wa ng'ombe na matumizi ya mashine ya brush cutter inaonesha uhusiano kati ya shughuli za binadamu, matumizi ya rasilimali za ardhi na uhifadhi wa mazingira**.** Nadharia hii inasisitiza kuwa shughuli za uzalishaji zinapaswa kuzingatia uwiano kati ya mahitaji ya binadamu na uwezo wa mazingira kuendelea kujirejesha. Katika nukuu hii, usimamizi bora wa ng'ombe pamoja na matumizi sahihi ya brush cutter vinaweza kuonesha namna teknolojia inavyoweza kutumika kuboresha shughuli za kilimo na ufugaji bila kuongeza uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo, matumizi ya brush cutter katika kudhibiti magugu na kuandaa maeneo ya kilimo yanapofanywa kwa usimamizi unaofaa yanaweza kusaidia matumizi bora ya ardhi, wakati ufugaji unaosimamiwa vizuri unaweza kupunguza shinikizo kwenye malisho na rasilimali za asili. Hivyo, nukuu hii inaendana na Nadharia ya Uhakiki Ikolojia kwa kuonesha umuhimu wa kutafuta uwiano kati ya uzalishaji wa binadamu, matumizi ya teknolojia na ulinzi wa mazingira**,** ili shughuli za kilimo na ufugaji ziwe endelevu kwa sasa na kwa vizazi vijavyo.

Pia, kauli hii inaungwa mkono na utafiti wa Vaughan na Johns (2021) kuhusu *Beyond Frame Analysis: Environmental Video Messaging*, unaosisitiza umuhimu wa taswira na video katika kuwasilisha ujumbe wa mazingira kwa hadhira. Utafiti huo unaonesha kuwa video za mazingira hazijengwi na maelezo ya maneno pekee, bali pia na namna picha, mandhari na matukio halisi vinavyopangwa ili kujenga uelewa kuhusu uhusiano kati ya binadamu na mazingira. Vivyo hivyo, katika nukuu hii, matumizi ya taswira kupitia kuonesha ng'ombe, mazingira ya ufugaji, mabanda pamoja na matumizi ya mashine ya brush cutte**r** huwasaidia watazamaji kuona kwa vitendo namna mbinu na teknolojia zinavyotumika katika shughuli za kilimo na ufugaji. Taswira za matumizi ya brush cutter zinaifanya taarifa kuhusu udhibiti wa magugu na usimamizi wa shamba iwe rahisi kueleweka, wakati picha za mifugo na mazingira ya shamba zinaonesha kwa uhalisia namna usimamizi bora wa mifugo unavyoweza kufanyika. Kwa hivyo, matumizi haya ya taswira huongeza uelewekaji, uhalisia na mvuto wa ujumbe**,** kwa sababu hadhira haishii kusikia ushauri wa wataalamu bali pia wanaona utekelezaji wake katika mazingira halisi. Hivyo, kama Vaughan na Johns (2021) wanavyosisitiza nguvu ya ujumbe wa video katika kujenga maana kuhusu mazingira, *Shamba Shape-Up* hutumia taswira za ufugaji na matumizi ya brush cutter kama nyenzo ya kuunganisha maarifa ya kitaalamu, teknolojia na uzoefu wa wakulima**,**

na hivyo kuwasilisha ujumbe wa kilimo na matumizi endelevu ya rasilimali kwa njia inayoonekana na rahisi kueleweka.

https://www.kenyamoja.com/video/citizen-planet-lake-victoria-farmers-adopt-durable-eco-friendly-plastic-fish-cages-citizen-tv?

4.4 Hitimisho

Sura hii ilijadili kwa kina malengo matatu ya utafiti huu huku ikijibu maswali ambayo utafiti ulilenga kuyatafutia majibu kuhusu uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini kenya. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa vipindi hivi vina mchango mkubwa katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira, yakiwemo upandaji wa miti, uhifadhi wa misitu na vyanzo vya maji, usimamizi bora wa taka, matumizi endelevu ya ardhi, pamoja na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, utafiti umeonyesha kuwa juhudi za uhifadhi wa mazingira hukabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile ukataji miti ovyo, uchafuzi wa mazingira, ongezeko la shughuli za kibinadamu zinazoharibu mazingira, uhaba wa rasilimali, ukosefu wa uhamasishaji wa kutosha na utekelezaji hafifu wa sheria za mazingira. Vilevile, matokeo yamebaini kuwa vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* hutumia mikakati mbalimbali ya kimawasiliano kama mahojiano na wataalamu, maonyesho ya vitendo, simulizi za washiriki, matumizi ya picha na video, pamoja na lugha rahisi na mifano halisi ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Kwa ujumla, utafiti umehitimisha kuwa Runinga ya Citizen ni chombo muhimu katika kukuza uelewa wa jamii, kuhamasisha ushiriki wa wananchi, na kuendeleza juhudi za uhifadhi wa mazingira kwa maendeleo endelevu.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Sura hii ni muhtasari wa tasnifu yote inayohusu uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika Runinga ya Citizen nchini kenya. Sura ya kwanza iliwasilisha usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti. Sura ya pili ilijadili mapitio ya maandishi yanayohusiana na uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira pamoja na msingi wa nadharia iliyoongoza utafiti huu. Sura ya tatu ilieleza mbinu za utafiti zilizotumika, zikiwemo muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na mbinu za usampulishaji, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, vifaa kwa ukusanyaji data pamoja na masuala ya uhalali, uthabiti na maadili ya utafiti. Sura ya nne iliwasilisha na kuchanganua data zilizokusanywa kuhusu mchango wa vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* katika kuelimisha, kuhamasisha na kuathiri mtazamo wa uhifadhi wa mazingira. Sura ya tano inatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti, mahitimisho na mapendekezo kwa wadau wa vyombo vya habari na uhifadhi wa mazingira nchini Kenya.

5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulichanganua mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya, kwa kulenga kubainisha masuala ya uhifadhi wa mazingira, changamoto za kimazingira zinazoibuliwa na mikakati ya

kimawasiliano inayotumika katika kuwasilisha ujumbe wa mazingira. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia ya Glotfelty na Fromm (1996), iliyosaidia kuchanganua uhusiano kati ya binadamu na mazingira, athari za shughuli za binadamu kwa mazingira na umuhimu wa uhifadhi. Matokeo yalionesha kuwa vipindi hivyo vinawasilisha masuala mbalimbali ya mazingira na kutumia mbinu kama mahojiano ya wataalamu, maonyesho ya vitendo, picha na simulizi katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi. Mchango wa utafiti huu ni kuongeza maarifa kuhusu namna mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira yanavyowasilishwa katika vipindi teule vya televisheni nchini Kenya, pamoja na kuonesha namna Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia inavyoweza kutumika katika kuchanganua maudhui yanayohusu uhusiano kati ya binadamu na mazingira. Aidha, utafiti huu unatoa msingi wa kitaaluma kwa tafiti zijazo kuhusu maudhui**,** uwakilishi wa mazingira na mikakati ya mawasiliano katika vipindi vya televisheni vinavyohusu uhifadhi wa mazingira.

5.1.1. Masuala ya Uhifadhi wa Mazingira katika Kipindi cha *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet*

Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vinawasilisha masuala ya uhifadhi wa mazingira kwa mitazamo inayotofautiana lakini inayokamilishana. *Shamba Shape-Up* ilijikita zaidi katika uhifadhi wa udongo na maji, kilimo endelevu, kilimo mesto cha miti na mazao, matumizi ya mbolea za kikaboni, usimamizi endelevu wa mifugo na uhifadhi wa bioanuwai**.** Kwa upande mwingine, *Citizen Planet* iliangazia zaidi uhifadhi wa misitu na vyanzo vya maji, bioanuwai, usimamizi wa taka, uchafuzi wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za asili**.** Hivyo, utafiti umebaini kuwa mawasiliano ya uhifadhi katika vipindi hivi yanahusisha maeneo mbalimbali ya mazingira, kuanzia rasilimali zinazotegemewa katika uzalishaji wa kilimo hadi mifumo mipana ya ikolojia.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia, matokeo yanaonesha kuwa vipindi hivi haviwasilishi mazingira kama mandhari ya shughuli za binadamu pekee, bali vinaonesha uhusiano na utegemeano kati ya binadamu na mazingira**.** Kwa mfano, uhifadhi wa udongo, maji, misitu na bioanuwai unaoneshwa kuwa unahusiana moja kwa moja na uzalishaji na ustawi wa jamii. Mchango wa utafiti katika lengo hili ni kubainisha na kuweka wazi masuala mahususi ya uhifadhi yanayowasilishwa katika vipindi hivi**,** huku nadharia ikisaidia kutafsiri namna masuala hayo yanavyojenga uhusiano kati ya shughuli za binadamu, matumizi ya rasilimali na uendelevu

wa mifumo ya ikolojia. Hivyo, utafiti unaongeza maarifa kuhusu mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika televisheni ya Kenya.

5.1.2. Changamoto Zinazoibuka Kutokana na Kutohifadhi Mazingira katika Vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet.*

Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vinaonesha changamoto zinazotokana na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali na shughuli za binadamu zinazoharibu mazingira. Katika *Shamba Shape-Up*, changamoto zilizopewa uzito ni mmomonyoko wa udongo, kupungua kwa rutuba ya ardhi, ukame na uhaba wa maji**,** ambazo huathiri uzalishaji wa kilimo na ustawi wa jamii. *Citizen Planet*, kwa upande mwingine, ilionesha zaidi ukataji wa miti, uharibifu wa misitu, uchafuzi wa mazingira na upotevu wa bioanuwai**,** pamoja na madhara yake kwa mifumo ya ikolojia na rasilimali za asili.

Aidha, vipindi vyote viwili vilionesha mabadiliko ya tabianchi kama changamoto inayohusishwa na uharibifu wa mazingira, ikidhihirishwa kupitia ukame, mafuriko na mabadiliko yasiyotabirika ya hali ya hewa. Kwa mtazamo wa Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia, matokeo haya yanaonesha uhusiano wa karibu kati ya shughuli za binadamu na afya ya mifumo ya ikolojia, ambapo uharibifu wa mazingira huathiri kwa wakati mmoja udongo, maji, bioanuwai na maisha ya jamii**.** Mchango wa utafiti katika lengo hili ni kuweka wazi namna vipindi teule vya *Citizen* vinavyowasilisha uhusiano huo na kuibua changamoto za kimazingira katika muktadha wa Kenya.

5.1.3. Mikakati ya Kimawasiliano Inayotumiwa katika Vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet.*

Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* hutumia mikakati mbalimbali ya kimawasiliano na kisanaa katika kuwasilisha ujumbe wa uhifadhi wa mazingira. Katika *Shamba Shape-Up*, mikakati iliyojitokeza zaidi ni mahojiano, maonyesho ya vitendo, vielelezo vya kuona, lugha rahisi na maelezo ya hatua kwa hatua. Wataalamu na wakulima hutoa maarifa kuhusu changamoto za mazingira, huku mbinu za uhifadhi wa udongo, maji, miti na kilimo endelevu zikionyeshwa moja kwa moja katika mazingira halisi ya mashamba. Kwa upande wa *Citizen Planet*, utafiti ulibaini matumizi ya ripoti maalumu, ushuhuda wa wanajamii, maelezo ya wataalamu, takwimu na vielelezo vya kuona. Kipindi hutumia picha na video za maeneo yaliyoathirika na yale yaliyohifadhiwa ili kuonesha hali ya mazingira na juhudi za

uhifadhi. Mikakati hii huunganisha taarifa za kitaalamu na uzoefu wa jamii, hivyo kuwezesha masuala ya mazingira kuwasilishwa kwa mtazamo wa kimuktadha na wenye uhalisia.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia, mikakati hii inaonesha uhusiano kati ya binadamu, shughuli zao na mazingira**,** hasa namna vitendo vya binadamu vinavyoweza kuchangia uharibifu au uhifadhi wa mifumo ya ikolojia. Mchango wa utafiti katika lengo hili ni kubainisha kuwa mawasiliano ya uhifadhi katika vipindi teule vya *Citizen* hujengwa kupitia ushahidi wa kitaalamu, uzoefu wa jamii, maonyesho ya vitendo na vielelezo vya kuona**,** badala ya kutegemea maelezo ya maneno pekee.

5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Sura hii inawasilisha mapendekezo ya utafiti yaliyotokana na matokeo ya uchambuzi wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* vya Runinga ya Citizen nchini Kenya. Kwa kuzingatia masuala ya uhifadhi, changamoto za kimazingira na mikakati ya kimawasiliano iliyobainishwa katika utafiti, sura hii inapendekeza hatua zinazoweza kuchukuliwa na watayarishaji wa vipindi, Runinga ya Citizen**,** serikali na taasisi za mazingira, pamoja na watafiti wa baadaye**.** Mapendekezo haya yanazingatia pia mtazamo wa Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia**,** hususan umuhimu wa kutambua uhusiano na utegemeano kati ya binadamu na mazingira na kuimarisha mawasiliano yanayounga mkono uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za asili.

Mtafiti anapendekeza kwamba Runinga ya Citizen na watayarishaji wa vipindi vya mazingira**,** waendelee kuimarisha maudhui ya uhifadhi wa mazingira. Hii ni katika *Shamba Shape-Up* na *Citizen Planet* kwa kuzingatia kwa uwiano masuala kama uhifadhi wa udongo na maji, misitu, bioanuwai, usimamizi wa taka na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, watayarishaji wanapaswa kuendeleza matumizi ya mahojiano ya wataalamu, maonyesho ya vitendo, vielelezo vya kuona, ushuhuda wa jamii na ripoti za maeneo halisi ili kuwasilisha uhusiano kati ya shughuli za binadamu na mazingira kwa uhalisia zaidi. Pendekezo hili linaendana na Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia, inayosisitiza uchunguzi wa uhusiano na utegemeano kati ya binadamu na mazingira.

Pia, serikali na taasisi zinazohusika na mazingira**,** inapendekezwa kuimarisha ushirikiano na vyombo vya habari katika kuandaa na kusambaza maudhui sahihi ya kimazingira. Wataalamu wa mazingira wanaweza kushirikishwa katika vipindi vya televisheni ili kutoa taarifa kuhusu changamoto za mazingira na mbinu za kuzitatua. Ushirikiano huu unaweza kuimarisha

uwasilishaji wa masuala kama mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa misitu, uchafuzi wa mazingira na uhifadhi wa vyanzo vya maji. Hili linaendana na mtazamo wa Uhakiki-Ikolojia unaotilia mkazo wajibu wa binadamu na taasisi katika kulinda na kurejesha mifumo ya ikolojia.

Aidha, kwa watafiti wengine, inapendekezwa tafiti zijazo zichunguze vipindi na vyombo vingine vya habari ili kupanua uelewa wa mawasiliano ya uhifadhi wa mazingira nchini Kenya. Tafiti hizo zinaweza kuchanganua redio, magazeti, mitandao ya kijamii na majukwaa ya kidijitali, pamoja na kulinganisha namna vyombo mbalimbali vinavyowasilisha masuala ya mazingira. Aidha, kwa kuwa utafiti huu ulijikita katika uchanganuzi wa maudhui**,** tafiti zijazo zinaweza kutumia mbinu nyingine kuchunguza namna ujumbe wa mazingira unavyopokelewa na kutafsiriwa katika miktadha mbalimbali. Hata hivyo, utafiti huo unaweza kuendelea kutumia Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia kuchanganua namna mawasiliano yanavyojenga maana kuhusu mazingira, matumizi ya rasilimali na wajibu wa binadamu katika uhifadhi.

MAREJELEO

Ademosu, I., Aondoover, E. M., Bodunde, H. A., & Sotiloye, B. (2026). Symbolic representations of the environment using texts and visuals in three environmental programs on Nigerian television stations. *Eurasian Journal of Science and Environmental Education, 6*(1), 15–22. https://doi.org/10.30935/ejsee/17877

African Development Bank. (2022). *African economic outlook 2022: Supporting climate resilience and a just energy transition in Africa*. African Development Bank.

Agalo, R. A., Day, P., Ronoh, L., & Otieno, M. (2024). Media framing of climate change contents in news coverage in Kenya. *International Journal of Professional Practice, 12*(4). https://doi.org/10.71274/ijpp.v12i4.476

Bashir, M. A., & Wanyonyi, E. (2024). Winning space for conservation: The growth of wildlife conservancies in Kenya. *Frontiers in Conservation Science, 5*, 1385959. https://doi.org/10.3389/fcosc.2024.1385959

Buell, L. (1995). *The environmental imagination: Thoreau, nature writing, and the formation of American culture*. Harvard University Press.

Chemarum, S. C. (2023). *Coverage of environmental issues by the Kenyan media: A case study of Citizen Television* [Master's dissertation, Aga Khan University]. Aga Khan University Institutional Repository. Aga Khan University Institutional Repository

Christie, K. S., Gilbert, S. L., Brown, C. L., Hatfield, M., & Hanson, L. (2016). Unmanned aircraft systems in wildlife research: Current and future applications of a transformative technology. *Frontiers in Ecology and the Environment, 14*(5), 241–251. https://doi.org/10.1002/fee.1281

Cohn, R. M., Mbeyu, R., Sarange, C., Mbogholi, F., Cheupe, C., Cheupe, J., Wamukota, A., Kamau, E., & Treviño, M. (2023). Carrier bag storytelling with coastal Kenyan families: Sharing food, illustrations, and knowledge for tangible environmental justice impacts. *Frontiers in Communication, 8*, 1173512. https://doi.org/10.3389/fcomm.2023.1173512

Cox, R. (2013). *Environmental communication and the public sphere* (3rd ed.). Sage.

Glotfelty, C., & Fromm, H. (Eds.). (1996). *The ecocriticism reader: Landmarks in literary ecology*. University of Georgia Press.

Guenther, L., Jörges, S., Mahl, D., & Brüggemann, M. (2024). Framing as a bridging concept for climate change communication: A systematic review based on 25 years of literature. *Communication Research, 51*(4), 367–391. https://doi.org/10.1177/00936502221137165

Hansen, A. (1991). The media and the social construction of the environment. *Media, Culture & Society, 13*(4), 443–458. https://doi.org/10.1177/016344391013004002

Hansen, A., & Machin, D. (2013). Researching visual environmental communication. *Environmental Communication, 7*(2), 151–168. https://doi.org/10.1080/17524032.2013.785441

Heise, U. K. (2008). *Sense of place and sense of planet: The environmental imagination of the global*. Oxford University Press. https://doi.org/10.1093/acprof:oso/9780195335637.001.0001

Hoppe, I., Dörpmund, F., Weigel, C., Loos, A., Garschagen, M., Kox, T., Volke, S., Appell, J. E., & Neverla, I. (2026). Climate change on television reaches the engaged but misses distant audiences. *Nature Climate Change, 16*, 288–296. https://doi.org/10.1038/s41558-026-02575-3

Intergovernmental Panel on Climate Change. (2021). *Climate change 2021: The physical science basis: Contribution of Working Group I to the Sixth Assessment Report of the*

Intergovernmental Panel on Climate Change. Cambridge University Press. https://doi.org/10.1017/9781009157896

Intergovernmental Panel on Climate Change. (2021). *Climate change 2021: Impacts, adaptation and vulnerability*. Cambridge University Press.

Kaul, L., Schrögel, P., & Humm, C. (2020). Environmental science communication for a young audience: A case study on the #EarthOvershootDay campaign on YouTube. *Frontiers in Communication, 5*, 601177. https://doi.org/10.3389/fcomm.2020.601177

Kitula, S. M., & Ubaga, E. M. (2026). Social media as a mechanism for communicating climate change and sustainability to the youth in Kenya: A systematic literature review [Conference abstract]. In *Programme & book of abstracts 2026* (p. 166). Kenyatta University.

Langat, G. K. (2021). *Communicating agricultural information using electronic media: The case of "Shamba Shape-Up" programme on Citizen Television in Kenya* [Master's thesis].

Lesorogol, C., & Lesorogol, P. (2024). Community-based wildlife conservation on pastoral lands in Kenya: A new logic of production with implications for the future of pastoralism. *Human Ecology, 52*, 15–29. https://doi.org/10.1007/s10745-024-00482-9

Maathai, W. (2004, December 10). Trees for democracy. *The New York Times*.

Marles, V. (2022). *Shamba Shape-Up Series 12: Impact of viewing on farmers' knowledge, attitudes and practices*. Mediae.

McPhearson, T., Kabisch, N., & Frantzeskaki, N. (2023). Nature-based solutions for sustainable, resilient, and equitable cities. In T. McPhearson, N. Kabisch, & N. Frantzeskaki (Eds.), *Nature-based solutions for cities* (pp. 1–11). Edward Elgar Publishing. https://doi.org/10.4337/9781800376762.00008

Mediae. (2020). *Shamba Shape-Up Series 10: Knowledge, attitudes and practices survey report*. Mediae.

Mediae. (2021). *Shamba Shape-Up Series 11: Knowledge, attitudes and practices report*. Mediae.

Mediae. (2022). *Shamba Shape-Up Series 12: Impact of viewing on farmers' knowledge, attitudes and practices*. Mediae.

Mediae. (2024). *Shamba Shape-Up Series 14: Knowledge, attitude and practice (KAP) report*. Mediae.

Monyenye, S. K., Muchunku, I. G., & Njeru, A. K. (2023). Analysis of Citizen Television's framing of GMO-related stories for public awareness in Kenya. *International Journal of Research in Engineering, Science and Management, 6*(9), 88–100.

Muigai, P., Agevi, H., Otuoma, J., Muyekho, F. N., Onyango, C. A., & Ayaga, G. (2023). Trade-offs in tree species selection and carbon offset on farms adjacent to Kakamega-Nandi Forest Ecosystem in Kenya. *Tropical and Subtropical Agroecosystems, 26*(3). https://doi.org/10.56369/tsaes.4774

Mutoro, N., Saerys-Foy, J., Moturi, A., Pfeiffer, L., Marker, L., & Wykstra, M. (2026). Effectiveness of using different presentation methods on cheetah conservation awareness and education in Kenya. *Frontiers in Communication, 11*, 1701321. https://doi.org/10.3389/fcomm.2026.1701321

Narura, A. K., Ssenku, J. E., Kudamba, A., Okurut, S. A., Namuli, A., Nansikombi, N., Nakizito, J., Kafeero, H. M., & Walusansa, A. (2024). The environmental conservation strategies used in secondary schools align with guidelines of United Nations Environmental Program: Evidence from a cross-sectional study in a city setting. *Asian Journal of Environment & Ecology, 23*(7), 200–230. https://doi.org/10.9734/ajee/2024/v23i7575

Obonyo, O. A., Agevi, H., & Tsingalia, M. H. (2023). Above-ground carbon stocks and its functional relationship with tree species diversity: The case of Kakamega and North Nandi Forests, Kenya. *Scientific Reports, 13*, 20921. https://doi.org/10.1038/s41598-023-47871-6

Olago, D. O., Downing, T. A., Githiora, Y., Borgemeister, C., Kamau, J., Kuiper, G., Koné, N. A., & Omuombo, C. (2024). Nature-based solutions in the savanna belt of Africa:

Insights from a systematic review. *Nature-Based Solutions, 6,* 100154. https://doi.org/10.1016/j.nbsj.2024.100154

Ong'ong'a, D. O. (2024). Caring for water, plastics, and trees: Community radio and digital media in Kenya's environmental movements. *Environmental Communication, 18*(1–2), 210–215. https://doi.org/10.1080/17524032.2023.2296845

Ouma Rasowo, J., Nyonje, B., Olendi, R., Orina, P., & Odongo, S. (2024). Towards environmental sustainability: Further evidences from decarbonization projects in Kenya's Blue Economy. *Frontiers in Marine Science, 11*, 1239862. https://doi.org/10.3389/fmars.2024.1239862

Petersen, M., & Nüsser, M. (2022). Using an unmanned aerial system to analyse environmental impacts of charcoal production on tropical savanna ecosystems in northwestern Kenya. *Environmental Monitoring and Assessment, 194*, 620. https://doi.org/10.1007/s10661-022-10241-2

Salawu, A. (2021). Introduction: Towards the development and sustainability of African language media. In A. Salawu (Ed.), *African language media: Development, economics and management* (pp. 1–12). Routledge. https://doi.org/10.4324/9781003004738

Shobande, O. A., & Asongu, S. A. (2022). The critical role of education and ICT in promoting environmental sustainability in Eastern and Southern Africa: A panel VAR approach. *Technological Forecasting and Social Change, 179*, 121480. https://doi.org/10.1016/j.techfore.2022.121480

Siyao, P. O., & Sife, A. S. (2021). Sources of climate change information used by newspaper journalists in Tanzania. *IFLA Journal, 47*(1), 5–19. https://doi.org/10.1177/0340035220985163

Tella, D. O. (2024). The use of social media in communicating environmental governance: A review of two social media platforms in South Africa and Kenya. *Ayika: Journal of Environment and Politics in Africa, 6*(1), 68–83. https://doi.org/10.69778/2664-3022/6.1/a4

Tshabangu, T., & Salawu, A. (2021). Indigenous-language media research in Africa: Gains, losses, towards a new research agenda. *African Journalism Studies*, *43*(1), 1–16. https://doi.org/10.1080/23743670.2021.1998787

United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization. (2021, October 11). *Global Media and Information Literacy Week: Media and Information Literacy for the Public Good*. UNESCO

United Nations Environment Programme. (2019). *Global environment outlook 6: Healthy planet, healthy people*. Cambridge University Press.

United Nations Environment Programme. (2021). *GEO-6 for youth*. United Nations Environment Programme.

Vaughan, H. N., & Johns, L. (2021). Beyond frame analysis: Formal analysis and genre typology in the communication study of short-form environmental video messaging. *Journal of Environmental Media, 2*(1), 55–78. https://doi.org/10.1386/jem_00040_1

Vyas, S., Burra, D. D., Calvin, K., Kirwa, L., Rottmann, S., & Ramirez-Villegas, J. (2024). *Impact of Shamba Shape-Up and iShamba on livestock and climate resilience*. CGIAR Initiative on Livestock and Climate, Technical Report.

Wefwafwa, J. A. (2025). TV portrayal and people's perceptions on indigenous environmental conservation in Kenya. *African Journalism Studies, 46*(3), 239–257. https://doi.org/10.1080/23743670.2025.2527062

Xu, Y., Sun, H., & Zhu, J. (2023). *Revive, restore, revitalize: An eco-economic methodology for Maasai Mara*. arXiv. https://arxiv.org/abs/2309.07165

VIAMBATISHO

Kiambatisho I: Kibali cha Utafiti cha Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki

THE CATHOLIC UNIVERSITY OF EASTERN AFRICA

AMECEA

02 /06/26

To whom it may concern

RE: NJAU WAMBUI JOYCE 1063428

It is our pleasure to inform you that Njau Wambui Joyce is a student in our Department of Languages, Literature and Communication undertaking a Masters of Arts in Kiswahili and Communication. She defended her proposal entitled: UCHUNGUZI WA NAFASI YA RUNINGA YA CITIZEN KATIKA UHIFADHI WA MAZINGIRA NCHINI KENYA: MIFANO VIPINDI VYA SHAMBA SHAPE-UP NA CITIZEN PLANET. She is due to collect data and I therefore request that she is accorded the necessary assistance.

Yours faithfully

Dr. Rose Mavisi
HoD Languages,Literature and Communication
Catholic University of Eastern Africa

THE CATHOLIC UNIVERSITY OF EASTERN AFRICA (CUEA) P.O. Box 62157 00200 Nairobi – KENYA
Tel: 020-2825811-5, 8890023-4, Fax: 8891084, Email: admin@cuea.edu, Website: www.cuea.edu
Founded in 1984 by AMECEA (Association of the Member Episcopal Conference in Eastern Africa)

Kiambatisho II: Kibali cha Utafiti cha NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 475648

Date of Issue: 17/June/2026

RESEARCH LICENSE



This is to Certify that Sr.. JOYCE WAMBUI NJAU of Catholic University of Eastern Africa, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Nairobi on the topic: UCHUNGUZI WA NAFASI YA RUNINGA YA CITIZEN KATIKA UHIFADHI WA MAZINGIRA NCHINI KENYA:MIFANO VIPINDI VYA SHAMBA SHAPE UP NA CITIZEN PLANET for the period ending : 17/June/2027.

License No: NACOSTI/P/26/4190934

475648

Applicant Identification Number

Ag. Director General
NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY &
INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

See overleaf for conditions